# Kuhudumia Ushirika

## Kuwaza upya juu ya uhusiano kati ya Ukuu (wa ki-Eklesia) na Usawazishaji

**Utafiti wa Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo**

**Taasisi ya Ikiumeneki ya Huffington Taasisi ya Marymount**

**Chuo Kikuu cha Loyola Marymount**

**Los Angeles, CA**

**2018**

**Yaliyomo**

Utangulizi/Kielelezo

Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo: Historia fupi ya asili yake na maendeleo kwa miaka 15 ya kwanza

Kuanzishwa kwa Kikundi cha Irineo

Miaka kumi ya kwanza

Kutengeneza utafiti wa pamoja

Muundo na yaliyomo kwenye utafiti wa pamoja

Utafiti

I. Utangulizi

Kujielewa kwa Kikundi cha Irineo na malengo yake

Jinsi ya utafiti wetu wa pamoja

II. Tafakari za Hisia za tafsiri ya kina
1. Umuhimu wa wa tafsiri ya kina kwa mazungumzo ya Ki-Ikiumeniki
2. Utafsiri wa kitheolojia wa lugha ya theolojia
3. Tafsiri ya kina ya mafundisho ya undani
4. Utafsiri wa kitheolojia wa kanuni
5. Umuhimu wa mambo yasiyo ya theolojia
6. Umuhimu wa historia kwa theolojia
III. Uchunguzi wa Historia
7. Kipindi cha Kanisa la Kwanza (karne ya 1 - 8)
8. Kipindi cha kutengwa (karne ya 9 - 15)
9. Kipindi cha ukiri (karne ya 16 - 18)
10. Kipindi cha usumbufu wa Ekklesia (karne ya 19)
11. Kipindi cha uamsho wa Ekklesia (Karne ya 20 -21)
IV. Makadirio ya kimfumo
12. Jamii / Ushirika kama msingi wa ekklesia
13. Mamlaka kanisani katika huduma ya jamii
14. Tafsiri ya kitheolojia ya ukuu wa Ki-ekklesia
15. Utafsiri wa kitheolojia wa usawazishaji
16. Ukuu wa Ki-ekklesia na Usawazishaji kwa huduma ya ushirika
V. Hitimisho
Muktasari
Maono ya siku za usoni

Kiambatanishi

**Kielelezo/Utangulizi**

Kwa muda mrefu pamekuwa na maongezi kuhusua "mazungumzo ya upendo na ukweli" kati ya Wa-Orthodoksi na Wa-Katoliki. Tangu miaka ya 1960, baada ya miaka Zaidi ya elfu moja ya utengano, imewezekana tena kukaribiana kwa dhati, kujuana vyema, na kukuza uaminifu. Kwa msingi huu, iliwezekana kufunguliwa kwa mizigo ya vizuizi kadhaa vya kihistoria na kuweza kuanzishwa kwa majadiliano ya kitheolojia ya kweli. Tangu wakati huo kumekuwa na maendeleo makubwa. Tunajua kwamba mengi yanatuunganisha kuliko yanayotutenganisha, na hata makanisa yetu huitana “dada". Hata hivyo, kunazo shida kubwa bado katika uhusiano wetu, na mara kwa mara zingine mpya huibuka.

Kwa kuzingatia hili, tunapaswa kufahamu kuwa sisi sote tunawajibika kwa utengano huo, sio kwa sababu sisi Wakristo wa kisasa tumeusababisha, ila kwa sababu tunajihisi nyumbani katika utengano huu - kwa sababu tumekuwa na faraja sana katika mila yetu wenyewe, na kwa sababu hatuwa husishi wale wasio kama sisi. Kwa hivyo, mchakato wa kurejesha umoja katika Ukristo, unahitaji wongofu wa kibinafsi kwa kila mmoja wetu, ambao huanza moyoni mwa kila mtu na hudumu katika maisha yote. Uongofu huu unaashiria badiliko la ndani kuelekea Kristo na utimilifu wa amri zake, na hatimaye kufikia upendo. Kama asemavyo Mtakatifu Isaka wa Siria, Yeeyote ambaye, kwa neema ya Mungu, anapata moyo kamili wa upendo au moyo wa huruma, hatatenganishwa na chochote na mtu yeyote, na atakua amebeba ubinadamu wote na ulimwengu wote.

Hamna shaka kuwa kuna Wakristo wengi ambao wamepata moyo wa huruma kupitia sala na utawa, huku pia wakibeba kwa uvumilivu msalaba wa shida za kila siku. Ndani ya mioyo yao, tayari wanadumu katika umoja wa kisaikolojia, upitao utengano wowote ule wa madhehebu ama mwingineo. Walakini, katika ufahamu wa dhambi ya mgawanyiko, makanisa yetu hayasiti kupendekeza maombi na utawa kwa waaminifu kama njia ya umoja wa ndani wa kila Mkristo, lakini pia kupitia mazungumzo ya kitheolojia na kwa msaada wa maombi hayo, wanajaribu kupata tena umoja wa imani ya kanisa lililo moja.

Kwa kufanya hivyo, tunafahamu upungufu ya dhana zetu za kitheolojia, ambazo kwamba hazipaswi kuwekwa dhahiri, kwa sababu tukifanya vile tunamfanya Mungu kuwa mpungufu katika istilahi na dhana zetu. Mungu hawezi kuelezeka kamwe; hawezi kuteuliwa kwa maneno na yuko juu zaidi ya mifano yote ya mawazo. Kulingana na Vladimir Lossky akiwanenea wanafunzi wake, muundo wa mawazo wowote ule kitheolojia ambao tunatumia kuelezea na kueneza imani unapaswa kusitishwa mara tu baada ya matumizi yake, ili tusije tukamfanya Mungu kuwa mfungwa wa mfano wetu wa dhana.

Tangu mwaka wa 2004, Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo limenuia kutafuta kwa uhuru na kwa wazi na kujadili na kutafakari juu ya shida na changamoto zilizopo kati ya makanisa haya mawili. Kwa bahati nzuri, kufuatia matokeo ya kipindi cha mazungumzo ya kibinafsi na majadiliano ya kitaaluma katika miaka ya hivi karibuni, hati ya utafiti wa sasa imefafanuliwa. Somo hili lililoitwa "Kutumikia Ushirika", linajaribu kwa njia kadhaa "kufikiria tena uhusiano kati ya Ukuu (wa Ekklesia) na Usawazishaji". Msingi wa muhimu ni ukweli kwamba hati hii haijadili kwa upeo wa kihistoria wala ya kimfumo tu, lakini njia zote mbili zinahusishwa juu ya mtazamo wa utafsiri wa kina wa theologia.

Tunatumai kuwa utafiti huu utakuwa ishara ya kutia moyo na mchango mzuri kwa uelewano mwemai ndani na baina ya makanisa yetu. Maridhiano yanahitajika sana, haswa leo, ambapo

moyo na akili zinahitajika ili kufikia maendeleo ya uponyaji yanayoaminika katika "mazungumzo ya upendo na ukweli". Kwa hayo, tunaomba baraka tele za Mwenyezi Mungu.

| | |
|---|---|
| Dkt Gerhard Feige | Dkt Serafim Joanta |
| Askofu wa Magdeburg | Askofu wa Ujerumani, |
| Rais-Mwenza wa Kikundi cha Mtk Irineo | Uropa ya Kati na kaskazini |
| Wa Ki-katoliki | Rais-Mwenza wa Kikundi cha Mtk |
| | Irineo Wa Ki-Orthodoksi |

**Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo:**
**Historia fupi ya chanzi na maendeleo yake katika miaka ya kwanza 15**
Johannes Oeldemann

Mnamo Oktoba 18, 2018, Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo lilipitishaa hati yake ya kwanza ya mtazamo mmoja, ambayo sasa inachapishwa katika kijitabu hiki. Ni matokeo ya mchakato mrefu wa majadiliano ambao ulianza karibu miaka 15 iliyopita, asili na kozi yake itaorodheshwa hapa kwa ufupi ili iwe rahisi kuiweka hati mahala pake pa nyakati na kuelewa historia yake.

Katika mwaka wa 2003, mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki yalikumbana na shida kubwa. Shida hii iliibuka mwishoni mwa miaka ya 1980 wakati Makanisa ya Katoliki ya Mashariki, haswa katika nchi hizo ambazo hapo awali zilikuwa chini ya utawala wa Kikomunisti, ziliweza kupata uhuru wa kuabudu an hata kujenga upya makanisa yao. Wakati wa miaka ya 1990, mjadala juu ya "Juhudi za umoja usioondoa waadhifa ya Papa wa Roma" na "Ushawishi wa Ufuasi" ulitawala mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki. Tume ya kimataifa ya Mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki ya ilijadili mada hizi katika vikao vyake katika Freising (1990) na Balamand (1993), lakini taarifa zilizopitishwa hapo zilikumbwa na pingamizi kwa pande zote kutoka kwa Orthodoksi na upande Wakatoliki uliowakilisha “umoja utakaodumisha waadhifa wa Papa wa Roma”. Baada ya pengo la miaka saba, Tume ya Kimataifa ya Mazungumzo ya Kitheolojia kati ya Makanisa ya Katoliki ya Roma na Makanisa ya Orthodoksi ilikutana mnamo Julai 2000 kwa kikao chake cha nane Mjini Baltimore (Amerika). Kardinali Walter Kasper, ambaye wakati huo alikuwa katibu wa Baraza la Maalum La Ofisi ya Papa wa Roma la Kukuza Umoja wa Wakristo, akiwaza nyuma kidogo, alikumbuka kuwa, "Wakati wa mwaka wa 2000 huko Baltimore, Tume ilijaribu kushughulikia suala hili ngumu tena, hii ilisababisha mvurutano mkuu na kuelekea kuanguka kwa mazungumzo ". Tume ilitawanyika bila kukubaliana juu ya utaratibu wowote zaidi na hatma ya mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki hayakuwa na uhakika wa usoni.

Kuharibika zaidi kwa uhusiano, haswa kati ya Roma na Moscow, kulitokea katikati yam waka wa 2002 wakati Roma ilipotangaza kuinuliwa kwa tawala nne za Kitume kwa safu ya Dayosisi, tawala ambazo Kanisa Katoliki la Roma Katoliki lilianzisha katika Nchi ya Urusi mnamo

mwaka wa 1991 na 1999. "Udhaifu katika sera ya upashaji wa habari ya Mji wa Roma kuhusiana na Upatriaka wa Moscow na kosa la makadirio ya umuhimu wa hatua hii kwa upande wa Urusi yalisababisha kuenea kwa mashtaka kutoka kila upande zote na mzozo uliozidi kuwa mkubwa", ambao ilikuwa mzigo mwingine zaidi kwa uhusiano kati ya Wa-Orthodoksi na Wa-Katoliki. Msururu wa mazungumzo kati ya Wakatoliki na Wa-Orthodoksi ulikuwa katika hatari ya kuvunjika na mazungumzo pia yangeweza kukatika chini ya kiwango kulichonuiwa na Tume Kuu ya Mazungumzo.

**Kuanzilishwa kwa kikundi cha Irineo**

Katika hali hii, kwa mwaliko wa chuo cha Ikiumenikii cha Johann-Adam-Moehler, wataalam sita walikutana mjini Paderborn mnamo Machi 13, 2003 kutafakari juu ya hatma ya mazungumzo ya Wa-Orthodoksi-Wa-Katoliki. Nukulu za majadiliano hayo zinasema, "Kwa kuzingatia mchakato wa sasa katika mazungumzo rasmi kati ya Makanisa ya Orthodoksi na Katoliki, ni muhimu kuzingatia kwa pamoja ni kwa njia ipi mazungumzo ya kitheolojia kati ya Orthodoksi na Katoliki yanaweza kupewa msukumo mpya". Baadhi ya waliohudhuria mazungumzo haya ya awali walikuwa Thomas Bremer, Basilius Groen, Antoine Lambrechts, Johannes Oeldemann, Rudolf Prokschi, na Wolfgang Thönissen. Ilikubaliwa "kuunda mkutano wa mazungumzo juu ya kiwango cha Uorthodoksi wote ambacho kinaweza kujadili shida zilizopo za kitheolojia na vile vile maswali ya jumla ya utafsiri wa Ki-theologia." Wakati wa majadiliano, wazo liliibuka kuanzisha kikundi cha utenda kazi cha wanatheolojia wa Wa-Orthodoksi na Wa-Katoliki. "Kikundi cha utendakazi cha kudumu na cha aina hii, kikiungana na washiriki sawa kadri iwezekanavyo, kinaweza kuwa taasisi iwezayo kushughulikia maswala magumu katika mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki wakati ambapo washirika wa jopo hilo wanapofahamiana zaidi," kama yasemavyo maelezo ya mkutano wa Paderbon. Mnamo 2003, waanzilishi waliweza kupata idhini ya Askofu wa Serbia Ignatije (Midić) wa Braničevo na Askofu msaidizi wa Magdeburg, Dkt Gerhard Feige, marais-weza wa kikundi kilichopendekezwa cha utendakazi. Kwa kushauriana kwa karibu na wasimamizi hawa wawili, wanatheolojia 24 walialikwa kwenye kikao cha mwanzo, kilichounda jopo hili la utendakazi, 12 Wa-Orthodoksi na 12 Wa-Katoliki.

Katika kikao chake cha kwanza, ambacho kilifanyika kuanzia Juni tarehe 23 hadi tarehe 27 2004 huko Paderborn, kazi ya kwanza ya washirika ilikuwa kukusanya na kutafiti mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki katika ngazi ya ulimwengu na katika muktadha tofauti wa kikanda. Zaidi ya hayo, mifano Zaidi ya vikundi tendakazi ziliwasilishwa, kama vile "Ökumenischer Arbeitskreisangelischer und katholischer Theologen" (Kikosi cha utendakazi cha Wanatheolojia wa-protestanti na wa-Katoliki) huko Ujerumani, ambacho pia hujulikana kama "Jaeger-Stählin-Kreis", na "Groupe des Dombes" huko Ufaransa. Enzo Bianchi aliripoti juu ya mchakato wa kidini huko Bose na Askofu Ignatije na Askofu Msaidizi Feige walijaribu kuunda muhtasari wa matarajio ya usoni ya mazungumzo ya Orthodoksix na Katoliki. Mwisho wa mkutano wa Paderborn, washiriki walikubaliana kuanzisha kikundi cha utendakazi kitakachodumu na wakaamua kukipa jina la " Kikundi cha utendakazi cha Orthodoksi na Katoliki". Maoni ya kuchagua Mt. Irineo wa Lyons kama mlinzi wa kiroho yalitolewa na washiriki kadhaa wa Orthodoksi. St. Irineo alionekana anafaa kwa sababu yeye ni baba wa kanisa anayeheshimika Mashariki na Magharibi na wasifu wake - akija kutoka Mashariki (Asia Minor) na kuhudumu kama Askofu huko Magharibi (Lyons) - ni mfano wa viunganishi vya kiroho na vya kiakili kati ya makanisa ya Mashariki na Magharibi ambavyo kikundi cha utendakazi kazi kilitarajia kukuza kupitia majadiliano yake.

Baadhi ya waanzilishi mabao bado ni washirika kwa kikundi cha Irineo hadi wa leo ni, kwa upande wa Orthodoksi, Nikolas Loudovikos, Paul Meyendorff, Vladan Perišić na Mariyan Stoyadinov, na kwa upande wa Katoliki kunao, Askofu Gerhard Feige (ambaye ni askofu wa Madgeburg tangu mwaka wa 2005), Thomas Bremer, Basilius Groen, Hervé Legrand, Johannes Oeldemann, Rudolf Prokschi, Ronald Roberson, na Wolfgang Thönissen. Leo hii, kikundi cha Irineo kinao washirika 13 wana-theolojia wa-Orthodoksi na 13 Wa-Katoliki, ambao wote wanatoka nchi kumi na sita tofauti, zikiwemo, Argentina, Austria, Bulgaria, Ufaransa, Ujerumani, Uingereza, Ugiriki, Italia, Lebanon, Malta, Uholanzi, Rumania, Urusi, Serbia, Ukrania na Amerika (Tazama orodha ya washirika mwisho wa hati). Washirika wa kikundi hiki hawteuliwi na Kanisa lao wenyewe ila huwa wanachaguliwa kadri ya upeo wao wa Ki-theolojia. Kwa mfano, panapojiuzulu mshirika awaye yule, uteuzi wa mshirika mpya hufanywa kwa kura ya pamoja ya kikundi cha utendakazi. Kwa hivyo, Kikundi cha Irineo sio tume rasmi ya mazungumzo na hujitizama kama kikundi cha mazungumzo yasiyo rasmi, ila ile ambayo inakutana kwa kusudi la kukuza mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki kwenye ngazi ya kimataifa.

***Miaka ya kwanza kumi***

Kufuatia mkutano wa kwanza huko Paderborn, mkutano wa pili wa Kikundi cha Irineo ulifanyika kwa mwaliko wa Kanisa la Ugiriki mnamo Novemba 2005 kwenye Monasteri ya Penteli huko Athina. Wakati wa kuchagua mahala pa mikutano yake, kikundi hiki kimekuwa kikitilia maanani kukutana kila wakati kwa mpangilio wa aidha kwa Katoliki kisha kwa Orthodoksi ama kwa Orthodoksi kisha kwa Katoliki. Katika mkutano huo wa Athina, washiriki wa Kikundi cha Irineo walikadiriaia uhusiano kati ya kanisa la parokia na kanisa la ulimwengu wote kupitia kwa mtazamo wa Kikanisa wa Katoliki na Orthodoksi, na pia kukagua swali la jinsi makanisa mengine ya Kikristo yanavyozingatiwa katika mtazamo wa kikanisa wa Orthodoksi na Katoliki. Kwenye kila mada ndogo, kulikuwa na hotuba kutoka pande za Orthodoksi na Katoliki ambazo zilifanya iwezekane kulinganisha na kujadili jinsi kila kanisa lilivyo jiwasilisha lenyewe na lilivyoonekana kutoka upande wa mwenziwe.

Mkutano wa tatu wa kila mwaka wa Kikundi cha Irineo ulifanyika mwishoni mwa Novemba mwaka wa 2006 katika Monasteri ya Chevetogne kule Ubeljiji. Swala kuu katika mkutano huu lilikuwa funzo na mazoea ya ukuu wa Ekklesia wakati wa milenia ya kwanza. Swala hili halikuyazamwa au kuzingatiwa tu katika hotuba kadhaa zilizogusia uhusiano kati ya Patriaketi za Kanisa la Kwanza, na kadhalika haki ya rufaa na umuhimu wa Sinodi, ila pia kwa uchunguzi wa pamoja wa asili zake (kama vile. Kanuni za Baraza la Sardika). Tangia mwanzoni, kikundi hiki cha utendakazi kazi kiliona ikiwa muhimu kutoangalia mawazo ya nadharia ya ukuu ki-kanisa pekee, kama ilivyo katika kanuni za Mabaraza ya Kanisa la Awali, lakini pia kuchunguza mazoea juu ya ukuu wa ki-kanisa kama ilivyoonyeshwa kupitia mawasiliano, ziara za heshima kwa pande zote, na pia ukumbusho katika Liturgia.

Kwa mwaliko wa rais mwenza wa Orthodox, Askofu Ignatije wa Braničevo, Kikundi cha Irineo kilikusanyika kwa mkutano wake wa nne mapema Novemba 2007 huko Serbia. Baada ya ufunguzi wa Chuo cha Theolojia cha Orthodoksi huko Belgrade, vipindi vya kazi vilifanyika kwenye Monasteri ya Pokajnica karibu na Velika Plana katika dayosisi ya Askofu Ignatije. Wakifuatilia kwa mpangilio wa nyakati kuanzia majadiliano huko Chevetogne, washiriki wa kikundi hicho walichunguza mafundisho na mazoea ya ukuu wa ki-kanisa katika Zama za Kati. Lengo kuu lilikuwa ni maendeleo yanayohusiana na Mageuzi ya Gregori na mzozo kati ya

upapa na mshikamano huko Magharibi, na pia Halmashauri za Mabaraza ya umoja za Lyons na Ferrara-Florence. Katika mkutano huu, Kikundi cha utendakazi kilipitisha njia ya kujadili hotuba zake katika vikundi kwa lugha ya hotuba, ambapo kila kikundi cha lugha kilikariri muhtasari wa mambo mapya yaliyojitokeza katika hoja ambazo baadaye ziliwasilishwa kwa kikao ziweze kujadiliwa. Mada za makubaliano basi ziliingizwa kwa ujumbe kutoka kwa kila mkutano wa kila mwaka na kuchapishwa kwa lugha tano (Kiingereza, Ufaransa, Kijerumani, Kiigiriki, na Kirusi) kwenye wavuti ya Taasisi ya Moehler na pia kutumwa kwa viongozi wa kanisa walio na jukumu la mijadala ya mazungumzo ya Kikristo.

Mkutano wa tano wa kila mwaka wa kikundi cha Irineo ulifanyika mnamo Novemba mwaka wa 2008 huko Vienna kwa msaada wa Shirika la Pro Oriente. Katika kikao hiki, mada ilikuwa mafundisho na mazoea ya ukuu (wa-kikanisa) katika nyakati za leo. Lengo lilikuwa juu ya ukuzaji wa ukuu (wa-kikanisa) wa upapa kufuatia Baraza la Trent na pia kazi za mwanzo za Mapatriaka wa Konstantinopoli katika umilki wa Ottoman na ya Mapatriaka wa Moscow katika milki ya Urusi. Katika mkutano huu, kwa mara ya kwanza kulikuwa na mafundisho ya hadhara jioni ambapo Job Getcha na Hervé Legrand waliwasilisha hati kuhusu mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki. Kufuatia mkutano wa Vienna, kazi ya Kikundi cha Irineo ilivutia shauku pana, na mazungumzo yake yalichapishwa baadaye katika nakala kadhaa za kiingereza, Kifaransa, na Kijerumani.

Mwanzoni mwa Novemba mwaka wa 2009, kikao cha mkutano wa sita cha Kikundi h airineo kilifanyika kwa mwaliko wa Kanisa la Orthodoksi la Ukrania katika Patriaketi ya Moscow mjini Kiev. Katika mkutano kwenye kwenye makao ya shule ya Theolojia katika Monasteri ya Mahandaki ya Kiev, kwa ara ya kwanza kikundi kilishughulikia kwa kina Baraza la Kwanza la Vatikani. Hati mbali mbali zinaangazia muktadha wa kihistoria wa Baraza hilo la Vatikani kutoka kwa maoni ya kikanisa, kitamaduni, na kisiasa. Zaidi ya hayo, kupitia njia ya kusoma hati za asili pamoja, washirika wa kikundi walijitahidi kuelewa maana sahihi na ujumbe uliokusudiwa wa ufafanuzi wa Baraza. Ratiba ya mkutano pia ilijumuisha kukutana na mkuu wa Kanisa la Orthodox la Ukrania, Metropoliti Volodymyr (Sabodan).

Katika mkutano wa saba wa kila mwaka mnamo Novemba mwaka wa 2010, ambao Askofu Gerhard Feige, kama rais mwenza wa Katoliki, alikuwa amealika kikundi hicho mjini Magdeburg, majadiliano juu ya Baraza la Kwanza la Vatikani yaliendelea. Katika hafla hii, kikundi kilichunguza mapokezi ya ndani ya Baraza hilo kwa Katoliki na itikio za Orthodoksi kwa maamuzi ya Baraza hilo la Vatikani. Katika kikao hicho mjini Magdeburg, Metropoliti Youhanna (Yazigi) kutoka kwa Patriaketi ya Kanisa la Orthodoksi la Antiokia alikuwepo kwa mara ya kwanza kama rais-mwenza mpya wa Orthodoksi. Ila kwa bahati mbaya, alibidiwa kuachana na jukumu hilo baada ya miaka mitatu tu wakati alipochaguliwa kama Patriaka wa kanisa lake.

Mkutano wa nane wa Kundi la Irineo, uliofanyika mnamo Novemba mwaka wa 2011 katika Chuo Kikuu cha Theolojia cha Orthodoksi huko St. Petersburg kwa mwaliko wa Kanisa la Orthodoksi la Urusi, ulijihusisha tena na tafsiri za Baraza la kwanza la Vaican na itikio za Orthodoksi kwayo. Ilionekana wazi katika mchakato huo kwamba ni muhimu sana kuelewa Baraza la Kwanza la Vatikani kwa kutumia vyombo vya njia ya kihistoria ili kwenda zaidi ya athari za mara kwa mara za kupepesa za pande zote mbili mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20. Kikundi pia kiliarifiwa juu ya mapendekezo yanayohusu ukuu (wa ki-eklesia)wa upapa ambayo yalitolewa na vikundi vingine vya masomo ya Ekiumenikii

(Kikundi cha Ushauri wa Theolojia ya Orthodoksi-Katoliki huko Amerika Kaskazini, Kikundi cha Farfa Sabina cha masomo ya Lutheran-Katoliki).

Kwenye mkutano wa tisa wa kila mwaka, uliofanyika mapema mwezi wa Novemba mwaka wa 2012 kwa mwaliko wa Jamii ya Ekiumenikii ya Bose katika Monasteri yao iliyopo Italia Kasikazini, washirika wa kikundi walitizama kwa mara ya kwanza karne ya 20. Waka jihusisha na Barala la nyumbani la Kanisa la Orthodoksi la Urusi, ya mwaka wa 1917/18 na pia wakajihusisha na Baraza la Pili la Vatikani. Katika uhusiano huu, lengo la upande wa Orthodoksi lilikuwa juu ya kushiriki kwa mapadre na watu katika baraza la Urusi na uhusiano kati ya baraza na Patraika. Kikundi pia kilichunguza swali la jinsi ufafanuzi wa Baraza la Kwanza la Vatikani ulipokelewa katika hati za Baraza la pili la Vatikani. Ilionekana kuwa yenye manufaa kuwa kwa majadiliano kila uwasilishaji wa Orthodoksi alifuatwa na mwitikio wa Katoliki na kinyume vilevile.

***Kutengeneza masomo ya kawaida***

Mnamo mwezi Novemba mwaka wa 2013, Kikundi cha Irineo kilikusanyika kwa mkutano wake wa kumi wa kila mwaka huko Thesaloniki kwenye makao ya shule ya Theologia ya Chuo Kikuu ambacho katibu mwenza wa upande wa Orthodoksi, Nikolaos Loudovikos, anafundisha. Baada ya kumaliza uchambuzi wa kihistoria, kikundi hicho sasa kilijitolea juhudi zake kwa mambo ya utafsiri wa Ki-theologia na ya kihistoria ya mazungumzo hayo theolojia. Hoja moja muhimu ilikuwa kufafanua uhusiano kati ya historia na theolojia, ambapo karatasi zilitolewa na Askofu Gerhard Feige na Job Getcha, ambaye alichukua jukumu la rais mwenza wa Orthodox kufuatia kutawazwa kwake kuwa Askofu mwishoni mwa mwezi Novemba mwaka wa 2013. Zaidi ya hayo, palikuwa na majadiliano juu ya mapokeo ya Orthodox kuhusiana na Baraza la pili la Vatikani na juu ya wazo la ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji katika theolojia ya kisasa ya Orthodoksi. Palitolewa muhtasari wa kwanzo wa matokeo ya kazi hiyo ya miaka kumi ya kwanza ambao uliwasilishwa Thesaloniki, na uamuzi ulifanywa ili kutoa uchunguzi wa pamoja juu ya uhusiano kati ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji.

Mkutano wa kumi na moja wa Kikundi cha Irineo ulifanyika mnamo Novemba mwaka wa 2014 kwenye Seminari ya Dayosisi Kuu ya Rabat nchini Malta. Mada kuu ya mkutano huu ilikuwa kutazama ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji katika kanisa za Orthodoksi kwa kuwa tume ya matayarisho, ambayo iliundwa mara ya kwa kwa minajili ya mkutano huo, iligundua kuwa mada hii ilikua hauikupewa nafasi ifaayo na Kikundi cha utendakazi katika mijadala yao hadi kufikia wakati huo. Mada hii ilichunguzwa kwa kuzingatia uhusiano baina ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji katika millenia ya kwanza kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, kikundi kilijadili hati kutoka Konstantinopoli na Moscow ambazo zilikuwa zimechapishwa kuhusu ukuu (wa ki-kanisa). Wakati wa kikao huko Malta, kamati ya watu wanne iliteuliwa ya kuandaa rasimu na kukabidhiwa kazi zaidi juu ya masomo ya pamoja. Washiriki wa Orthodox walikuwa Assaad Elias Kattan na Vladimir Khulap na Wakatoliki walikuwa Edward Farrugia na Johannes Oeldemann.

Katika mkutano wake mnamo Juni mwaka wa 2015, kwa msingi wa majibu kutoka kwa kikundi cha utendakazi kuhusu kuanzishwa kwa utafiti huo ambao ulikuwa umejadiliwa huko Malta, kamati ya kurasimu ilitoa toleo la kwanza la hati ambayo sasa inachapishwa. Rasimu hii ilijadiliwa kwa undani kwa mara ya kwanza katika mkutano wa kumi na mbili wa mwaka uliofanyika kwa mwaliko wa Patriaka wa Ekiumeniki mwanzoni mwa Novemba mwaka wa

2015 katika Shule ya Theolojia ya Halki kwenye kisiwa cha Heybeliada karibu na mji wa Istanbul. Katika mkutano huu, Karatasi za utafiti pia zilitolewa juu ya maswala kadhaa ambayo hayakushughulikiwa vya kutosha katika rasimu ya kwanza ya uchunguzi, kwa mfano, umuhimu wa kanuni ya kanisa la kitaifa katika Kanisa la Orthodoksi, kueleweka kwa mamlaka katika Kanisa, na wazo la ushirika / koinonia na umuhimu wake kwa umoja wa Ekklesia.

Kwa miaka miwili iliyopita, kazi ya utafiti wa pamoja ulibugia muda mwingi zaidi. Kamati ya kurasimu ilikutana mara mbili kila mwaka, mara moja Roma na mara moja Paderborn, ili kutambua mapengo, kusambaza kazi, na kuingiza nadharia/mada za ziada. Wakati wa mkutano wa kumi na tatu wa mwaka, ambao ulifanyika mapema Novemba, 2016 katika mwaliko wa Jumuiya ya waumini wa Taizé nchini Ufaransa, lengo kuu la mjadala lilikuwa kwenye maandishi ya utafiti wa pamoja. Zaidi ya hayo, kikundi cah utendakazi kazi kilichunguza utafsiri wa Kitheolojia wa Mafundisho ya kidini na kueleweka wa mamlaka katika Kanisa.

Katika mkutano wa kumi na nne wa mwanzoni mwa Oktoba 2017 katika Monasteri ya Caraiman kwa mwaliko wa Kanisa la Orthodoksi la Rumania, Kikundi cha Irineo kwa mara nyingine kilifanya kazi juu utafiti wa pamoja. Ili kujaza mapengo ambayo yalikuwepo bado, washiriki waliangalia majukumu ya Patriaketi za Mashariki katika milenia ya kwanza, jukumu la mtume Petro katika utamaduni wa Kanisa, na haki ya rufaa katika kanisa la Mashariki na la Magharibi. Katika miezi iliyofuata, kamati ya kurasimu nakala iliingiza marekebisho ya mwisho na ikatuma toleo lililokamilika la utafiti huo kwa washiriki wote kwa upekuzi wao wa mwisho.

Mnamo Oktoba 18, 2018, katika muktadha wa mkutano wake wa kumi na tano wa mwaka ambao ulifanyika katika Jumba la Dayosisi ya Mariatrost ya dayosisi ya Katoliki ya Graz-Seckau, Kikundi cha Irineo kilijadili maandishi hayo kwa mara ya mwisho na kuyakubali bila pingamizi. Kwa mara ya kwanza, mkutano huo ongozwa kwa pamoja na Askofu Gerhard Feige pamoja na rais-mwenza mpya wa mlengo wa Orthodoksi, Metropoliti Serafim (Joantă) wa Ujerumani, Katikati na Kaskazini mwa Ulaya ambaye alikuwa amechukua jukumu hili kutoka kwa Askofu Mkuu Job aliyekuwa ameteuliwa kuwa rais mwenza wa Tume rasmi ya Mazungumzo ya Kimataifa wakati huo. Jioni ya Oktoba 18, kulikuwa na uwasilishaji rasmi wa utafiti wakati wa mkutano wa hadhara ulioandaliwa katika Meerscheinschlössl ya Graz na Chuo cha Theolojia cha Chuo Kikuu cha Graz kwa kushirikiana na Sehemu ya Graz ya Pro Oriente Foundation.

***Muundo na yaliyomo kwenye utafiti wa pamoja***

Utafiti wa pamoja mabao sasa umechapishwa unakadilia uhusiano baina ya ukuu (wa-ki-kanisa) na usawazishaji katika kanisa. Kwa hivyo, hati ya Kikundi cha Irineo inahusika na somo sawa na Tume rasmi ya Mazungumzo ya Kimataifa. Washiriki wa Kikundi cha Irineo wanauhakika kwamba maswala ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji hutimiza jukumu lao wakati tu "wanahudumia ushirika", kama jina la utafiti wao wa pamoja lionyeshavyo. Mada ndogo inaelezea haja ya "kuwaza upya kuhusu uhusiano baina ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji ". Kwa nini kuuwaza upya? Je! Kuna njia ipi mpya katika utafiti huu? Kwanza, kuwa kwamba, katika hati hii, ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji hauzingatiwi kihistoria au kimfumo tu, ila njia hizo mbili zimejumuishwa kwa msingi wa tafakari za utafsiri wa theologia.

Kwa hivyo "Tafakari za utafsiri wa ki-theologia " zinaunda sehemu kuu ya hati hio. Baada ya tafakari za kimsingi juu ya umuhimu wa utafsiri wa ki-theologia kwa mazungumzo ya

Ikiumeniki, inatoa maoni juu ya utafsiri wa lugha ya kitheolojia, ya mafundisho ya kidini, na ya kanuni. Kwenye tamati, sura ya utafsiri wa theologia inazungumzia ushawishi wa mambo yasiyo ya kitheolojia na umuhimu wa historia kwa theolojia. Wakati wa majadiliano yao, washirika wa Kikundi cha Irineo walizidi kufahamu kuwa, kuelewana kwa kina kungetokana na kila upande kuweza kuchichunguza kuhusu tafsiri zao wenyewe za historia, na hitimisho zitokanazo na tafsiri hizo. Kwa hivyo sura juu ya utafsiri wa theologia ni ya muhimu sana kwa hati nzima. Tafakari za utafsiri wa ki-theologia huenda kuwa ndio sehemu ya ubunifu zaidi ya utafiti wote kwa sababu hadi sasa hakuna kitu kinachoweza kulinganishwa pamoja kilichoandaliwa kwa pamoja na wanatheolojia wa Orthodoksi na Katoliki.

Sura ya pili na ndefu zaidi ya hati imebeba "Uchunguzi wa Kihistoria" juu ya kukua kwa uhusiano kati ya ukuu (wa-ki-kanisa) na usawazishaji. Kichwa chake kiliundwa kwa makusudi kwa uangalifu sana. Kundi la Irineo halidai kuwasilisha ufahamu mpya kabisa katika historia, lakini limetoa muhtasari wa matokeo muhimu zaidi ya utafiti wa kihistoria wa miongo ya hivi karibuni na imeibua "maoni" kutoka kwake kuhusu kueleweka kwa ukuu (wa-ki-kanisa) na usawazishaji ambao unatofautiana katika sehemu kadhaa kutoka maoni yaliyopitishwa mapema na ubaguzi ulioenea. Hii inahusia vipindi vyote viwili vya Kanisa la Kwanza, wakati ukuu (wa-ki-kanisa) na usawazishaji "zilisimama katika mvutano mmoja kwa mwingine" (§ 7), na kwa karne zilizofuata ambazo, kupitia "matokeo ya mchakato mrefu wa kutengana" (§ 8), zilisababisha utengano kati ya Mashariki ya Uigiriki na Magharibi ya Kilatini. Kuanzia karne ya 16, kulikuwa na "miundo ya vikundi vilivyoambatana na ukiri sawa" (§ 9) na vya "Mambo yaliyohusu Kanisa pekee" jambo ambalo lilisababisha Wakatoliki wote na Orthodoksi kuuliza "kana kwamba yawezekana jamii iliyo katika utengano kutumika kama chombo cha wokovu" (§ 9.10)

Karne ya 19 iliwasilisha changamoto maalum kwa maelezo ya pamoja ya historia hii; imeelezewa katika utafiti huo kama kipindi cha "**mwingiliano wa ki-kanisa**". Katika Kanisa la Katoliki, changamoto mpya ki-kanisa, kisiasa na kiamsomo zilisababisha kuzingatia ofisi ya upapa, na hii ilifikia kilele katika ufafanuzi wa Baraza la Kwanza la Vatikani kuhusu kutokuweza kukosa na kuhusu maoneo ya ukuu (wa ki-eklesia)wa Papa. Utafiti uliyotolewa na Kikundi cha Irineo una tafsiri iliyo na msingi mzuri wa ufafanuzi wa Baraza la I kwa msingi wa uchunguzi wa pamoja wa hati asili na inabainisha kwa upande mmoja kwamba Mababa wa Baraza hawakutaka kumfanya papa " Mfalme kikamilifu ”(§ 10.7), na kwa upande mwingine kwamba" tafsiri kubwa " ya nyumaye haikua aminifu kwa ufafanuzi wa fafanuzi za Balaza hilo (§ 10.10). Utafiti huo pia una ukumbusho kwamba, wakati wa karne ya 19 kwa upande wa Orthodox vile vile, kwa mzozo juu ya Ufunuo na uundaji wa uhuru kwa, makanisa ya kitaifa, mabadiliko makubwa yalifanyika ambayo bado yanaathiri mazungumzo baina ya Orthodoksi na Katoliki hadi wa leo.

Sura ya kihistoria ya utafiti wa pamoja inahitimisha na maelezo kuhusu "kuibuka upya kwa dini" katika karne ya 20 na 21 ambayo inahusishwa na maendeleo ya ekaristi ya dini kwa upande wa Orthodoksi na kugunduliwa upya kwa Mababa wa Kanisa pamoja na harakati za liturgia kwa kanisa la Katoliki. Baraza la pili la Vatikani lilifungua mlango kwa mazungumzo ya kidini na likakaribishwa na wanatheolojia wa Kanisa la Orthodoksi "kama hatua nzuri katika mwelekeo wa **ushirikiano**" (§ 11.14). Mchakato wa maandalizi ya Baraza la Uorthodoksi wotekwa upande wa Orthodoksi ulishuhudia "juhudi kubwa ya kutumia usawazishaji katika nadharia na pia mazoea" (§ 11.6). Kwa kuona ukweli bayana kwamba hili halikufanikiwa na Baraza la Kriti kwa njia iliyotarajiwa, pamoja na uchunguzi wa ugumu wa kuimarisha

usawazishaji katika Kanisa la Katoliki chini ya taswira ya Papa Francis, iliezekeza Kikundi cha Irineo kusema hivi mwishoni mwa sura ya historia, "Kwa hivyo, Waorthodoksi na Wakatoliki wote wanakabiliwa na changamoto ya kujumuisha ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji, na itakuwa muhimu na yenye manufaa kwa makanisa yote mawili kushughulikia maswala haya kwa pamoja, ili kufikia suluhisho linalokubalika kwa wote" (§ 11.15).

Sehemu ya tatu ya hati hiyo ina "Makadirio ya kimfumo" juu ya mada kuu. Kuanzia na maelezo ya pamoja ya kueleweka kwa "ushirika" (koinonia / communio), hati hiyo kwanza inaelezea **kubuliwa** kwa mamlaka katika Kanisa ambayo lazima kila mara yawe katika huduma ya jamii, bila kujali kama inatekelezwa katika minajili ya ngazi za ukasisi au njia ya usawa. Kueleweka kwa kitheolojia kuhusu ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji kuna zingatiwa katika sehemu mbili ndogo, kabla ya hitimisho kusisitiza utangamano wa ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji katika huduma ya jamii. Washirika wa kikundi tendakazi wanasisitiza "usawa wa asili" na "mshikamano" wa kanuni za ngazi za ukasisi na usawa katika Kanisa (§ 16) na wanaamini kuwa "mtu hawezi kuelewa Ukuu (wa ki-eklesia)bila Usawazishajii, wala kushughulika na usawazishaji huku akipuuza Ukuu (wa Ki-kanisa)"(§ 16.3).

Hitimisho la mwisho linatoa muhtasari wa hoja muhimu zaidi na linatoa "maono ya siku za usoni" ambapo washirika wa Kikundi cha Irineo wanaomba njia ipatikane ya "kukabili misimamo fulani ya awali na kuunganisha mambo muhimu ambayo yamehifadhiwa katika tamaduni zote mbili kwa ufahamu wa pamoja wa ukuu (wa ki-eklesia)”(§ 17.8). Hii inaonyesha imani yao kwamba "kugeukia historia ya awali sio suluhisho, iwe ni kwa Orthodoksi au kwa Wakatoliki" (”17.10). Aidha kile kinachohitajika, ni "suluhisho la pamoja, linalokubalika kwa makanisa yote mawili" suluhisho ambalo "linaweza kujibu mahitaji ya karne ya 21" na "linalo egemea kwenye makuu ya pande zote mbili" (§ 17.12). Suluhisho kama hilo, kama maoni ya mwisho ya utafiti yanavyosema, linaweza kufanikiwa tu ikiwa mazungumzo hayawachiwi wanateolojia wa masomo peke yao lakini pia hushilikisha maaskofu na makasisi na, na pia vilevile, waaminifu kwa pande zote mbili.

Kwa hivyo washirika wa Kikundi cha Irineo wanatumaini kwamba kutakuwa na mapokezi mapana ya utafiti wao, sio tu katika duru za masomo ya kitheolojia, bali pia katika mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki katika ngazi za kimataifa, kitaifa na kikanda. Nakala iliyochapishwa hivi majuzi juu ya kazi ya Kikundi kufikia sasa hivi inaelezea Kikundi cha pamoja cha utendakazi cha Orthodoksi na Katoliki cha cha Mtakatifu Irineo kama "aina ya jopo-la-kimawazo kwa mazungumzo ya kitaifa ya Katoliki na Orthodoksi.” Ikiwa kikundi hiki kinataka kuyapa haki madai haya, Kundi litahitaji kuendelea kushughulikia maswala ya kina ambayo yanaendelea kuwa mzigo kwenye mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki, ila kwa njia iliyositirika kuliko njia dhahiri. Kufuatia kububalika kwa hati za Ravenna (2007) na Chieti (2016), Tume ya Mazungumzo ya Kimataifa iko katika mchakato wa kuingia kwenye wamu mpya ya mazungumzo. Kufuatia mzozo unaoendelea kuwa mkubwa kati ya Patriaketi za Konstantinopoli na Moscow juu ya Ukrenia, mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki yamo kwenye hatari ya kukumbwa na janga lingine. Kundi la Irineo lilianzishwa miaka 15 iliyopita kwa sababu ya mzozo katika mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki. Kwa hivyo, kwa wakati huu wa sasa, itaonekana kwamba kuendelea kwake kuna maana na ni muhimu ili kuendeleza mazungumzo, yaliyo huru iwezekanavyo kutokana na maendeleo ya leo katika siasa za kanisa.

**Utafiti**

## *I. Utangulizi*

Kwa zaidi ya mwongo mmoja, uhusiano kati ya ukuu (wa ki-eklesia) na usawazishaji umekuwa ni kiini cha mazungumzo ya kitheolojia kati ya Wakatoliki na Wa-Orthodoksi. Tangu kutolewa kwa hati ya Jumuiya ya Pamoja ya Mazungumzo ya Theolojia kati ya Kanisa la Orthodoksi na Kanisa Katoliki ambayo ilihusu "Matokeo ya Ki-ekklesia na ya Ki-kanuni ya Maumbile ya Ki-Sakaramenti ya kanisa: Ushirika wa Ekklesia, Ushirikiano na Mamlaka" (Ravenna 2007), majadiliano kati ya wanatheolojia wa Katoliki na wa Orthodoksi yamehusia jinsi ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji, kama maneno yanayolingana, hufanya kazi katika viwango tofauti, ambavyo ni vya nyumbani, kikanda, na kwa ulimwengu wote. Hati ya juzi kabisa ya tume hiyo iliyohusu " ukuu (wa ki-eklesia) na usawazishaji wakati wa Milenia ya kwanza: Kuelekea Kuelewana katika Huduma ya Umoja wa Kanisa" (Chieti 2016) ilifikiria upya baadhi ya mambo haya, ila bado ni hatua moja tu kuelekea maelewano ya pamoja. ya uhusiano kati ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji.

Walakini, swali kuhusu uhusiano kati ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji sio jambo jipya. iliashiriwa kwa kiwango fulani katika mapokezano ya theolojia na kidini wakati wa milenia ya kwanza. Katika milenia ya pili, iliathiri mazungumzo kati ya wanatheolojia wa Mashariki na Magharibi ambayo mara nyingi yalijawa na ushawishi wa usomi. Tangu kutengana kwao, Wakatoliki na Wa-Orthodoksi wameibua aina tofauti za utumiaji wa mamlaka, kibinafsi na kwa pamoja. Hii ilisababisha pande zote mbili ziwe na mafundisho na mazoea yaliyoegemea upande mmoja. Hata hivyo, bado uhusiano kati ya jamii ya maaskofu na mkuu wao sio wa kitabia: aina tofauti za kutumia ukuu katika Kanisa la Katoliki baada ya Vatikani I (1869-70) huonyesha kwamba wazo lile lile la ukuu linaweza kutekelezwa kwa njia tofauti, ilihali katika Kanisa la Orthodox ushirikiano wa kinara wa kwanza na maaskofu wake bado haukuwa wa asili. Zaidi ya hayo, mazungumzo kati ya makanisa yetu yameangazia juu ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji kama vitengo vinavyotumiwa sana kwa uongozi wa kanisa. Walakini ni muhimu pia kuvitafakari kwenye mfumo mkubwa wa watu wa Mungu na katika vipaji vyao vingi.

Kuwaza tena juu ya uhusiano kati ya ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji sio kazi ya mazungumzo kati ya waOrthodox na waKatoliki tu lakini ni changamoto kwa mijadala ya kanisa binafsi vile vile, kama Sinodi ya Maaskofu Katoliki huko Roma (2015 na 2016) na Baraza la Orthodoksi huko Krete (2016) zilivyoonyesha. Kinyume na msingi huu, Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo kinawasilisha uchunguzi huu - wakitumaini kwamba utatoa hisia mpya kuelekea kuwaza upya kuhusu uhusiano baina ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji.

**Kujielewa kwa Kikundi cha Irineo na malengo yake**

Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo lilianzishwa mwaka wa 2004 kule Paderborn, Ujerumani, wakati ambapo mazungumzo rasmi ya kimataifa kati ya waorthodoksi na wakatoliki kilikuwa kikikumbana na shida. Kikundi cha Irineo kinao washirika 13 wana-theolojia wa-Orthodoksi na 13 Wa-Katoliki, ambao wote wanatoka nchi tofauti (zikiwemo, Argentina, Austria, Bulgaria, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Italia, Lebanon, Malta, Uholanzi, Rumania, Urusi, Serbia, Ukrania, Uingereza na Amerika). Washirika wa Kikundi cha Utendakazi hawateuliwi na makanisa yao, ila wanaalikwa kwa msingi wa ustadi wao wa kitheolojia. Kwa hivyo, Kundi la Irineo sio tume rasmi ya mazungumzo, lakini ni kikundi cha wataalam kisicho

rasmi, kinachokutana kwaa kusudi la kusaidia mazungumzo ya Orthodoksi-Katoliki kwenye ngazi ya kimataifa.

Kama kikundi cha kimataifa kilicho na uku wa lugha na upana wa kitamaduni, washiriki wa Kikundi cha Ireneo wanaona kuwa ni kazi yao kuchunguza tofauti zilizopo katika fikra na mazoea ya kanisa, psmoja na njia za kufikiria na kufanya theolojia. Wanajaribu kuelewa shida za sasa na kuona jinsi makanisa yote mawili yanavyoweza kutajilshana kwa "kubadilishana kwa zawadi". Wanatumai kuwa kwa njia hii wataweza kukuza uelewano katika makanisa yao, na wamejitolea kuhusika kwa kibinafsi katika juhudi hii.

**Jinsi ya utafiti wetu wa pamoja**

Hati ya sasa ni mazao ya juhudi ya pamoja iliyofanywa na washirika wa Kikundi cha Irineo kwa zaidi ya miaka kadhaa. Kazi hii ni uchunguzi hasa wa mambo kadhaa ambayo kwa upana yanahusia utafsiri wa Ki-tholojia ya kihistoria, na ya kimfumo katika njia wa mawasilisho, majibu yake, na uundaji wa mada za pamoja. Tunauhakika kwamba maswali ambayo bado hayajasuluhishwa kati ya Makanisa ya Katoliki na Orthodoksi yanaweza kutatuliwa kwa kutangamana kwa utafsiri wa Ki-theolojia, historia, na mfumo. Kwa jambo hili, tunafahamu kuwa utafiti wetu bila shaka ulikua haba, haswa katika sehemu yake ya kihistoria.

Hati hii inawasilisha mazingatio kulingana na ratba hii njia tatu kupitia kwa taarifa kumi na sita za pamoja. Kila moja yao inaambatana na maoni ambayo yanalenga kuonyesha wasiwasi wake mkuu kwa msaada wa mifano, pamoja na kuelezea maneno yaliyotumika, kubaini maendeleo, na kuunda maswali wazi. Hati hiyo ya sasa imehamasishwa na jaribio la kutoa mtazamo wa kawaida wa uhusiano baina ya ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji, na kuweza kutoa maelezo ya pamoja kuhusu miseto tofauti.

## *II. Tafakari za Utafsiri Ki-theolojia*

### 1. Umuhimu wa utafsiri wa ki-theolojia kwa mazungumzo ya Ki-Ikiumeniki

*Kauli ya Pamoja: Uendelezaji wa utafsiri wa ki-theolojia umeleta kuingizwa kwa dhana za u-historia na utamaduni wa kijamii kama changamoto za kudumu za kitheolojia. Kila mjadala una mazingira ya kihistoria na huwekwa katika hali ya kijamii na mila. Kwa hivyo, kila mazungumzo ya kitheolojia lazima izingatie tofauti za lugha, njia za kufikiria, na msisitizo maalum wa kila tamaduni. Katika juhudi zetu za kukuza maelewano ya heshima, tunahitaji kuweka maneno ya mbeleni katika muktadha wao wa kihistoria na epuka kuyasoma kwa njia ya nyakati. Kwa njia hii, tunaweza kuja karibu kuelewa kauli kama zilivyokusudiwa, na dhamana yao ya kudumu inaweza kutambuliwa. Hii inahitaji kuwaza upya mara kwa mara tamaduni tofauti ambazo kwa upande wake zinaelezea utajiri wa imani na sio za kipekee kibinafsi.*

**1.1** Utafsiri wa Ki-theolojia unaongelea ufafanuzi. Ukristo unaweza kuelezewa kuwa wa utafsiri wa theolojia, kwa kadiri inavyofafanua tafsiri ya kutosha ya maandiko ya bibilia (taz. Rom 7: 6 na 2 Pet 3:16) na vile vile vipengele vya imani, maandishi ya Mababa wa Kanisa, na maneno mengine ya imani ya Kikristo. Hasa, utafiti muhimu wa Bibilia umepinga njia za jadi za kutazama Maandiko na kufungua mitazamo mipya kwa Wa-Orthodoksi na Wakatoliki pamoja.

**1.2** Wa- Orthodoksi na Wakatoliki wanaamini kwamba Maandishi Matakatifu lazima yatafsiriwe ndani ya Tamaduni, ambayo kwa hivyo hutumika kama funguo la utafsiri wa theolojia. Njia hii ya utafsiri wa theolojia inakuwa thabiti katika liturugia, maisha ya kiroho, na utumishi (*diakonia*). Mwelekeo wa utafsiri wa theolojia wa mazungumzo yetu unaashiria juhudi za kutafsiri maneno yaliyo mengi ya Tamaduni. Tuna hakika, kwa kila upande wetu, kwamba ufahamu wa kile Tamaduni ilicho, hutegemea kuelewa wa kila upande jinsi mwenzetu katika mazungumzo anatazama na kukabiri sehemu tofauti za tamaduni hiyo.

**1.3** Kudumishwa kwa lengo kamili hakuwezekani, kwani ufafanuzi wowote ule umewekwa mahala pake katika historia. Hata hivyo, fahamu murwa yaweza kufunua ubaguzi na chuki iliyo fichika ambazo huelekewa tafsiri duni. Kwa mfano, kuondoka hisia za utafsiri wa theolojia wa karne ya ishirini kutoka kwa elekezo la ukuu wa kanisa na kiini cha kanisa pekee na kuendea ukanisa wa ushirika (taz. sura ya 11 na 12) unafanya iwe rahisi kuona na kujiepusha na maoni ya nyakati wakati wa kusoma majibizano ya hapo awali, na pia kutambua ndani yao mambo yasiyokuwa ya kitheolojia.

**1.4** Wazo la mapokezi ni la msingi kwa mazungumzo ya Ki-Ikiumeniki. Mapokezi yanapaswa kuzingatia kanuni ambayo kilicho kizima na zilivyo kwa sehemu hutafsiri kila mmoja kwa usawa. Ni jambo la maana sana, kwa mfano, kwamba kauli za Vatikani I kuhusu kutokosea kwa Papa na ukuu (wa ki-kanisa), jambo ambalo bado linaleta kizuizi kikuu kwa mazungumzo baina ya Orthodoksi na Katoliki, ziunganishwe katika ukanisa wote na utamaduni wa Kanisa la Katoliki, haswa katika mwanga wa Vatikani II (cf. §§ 11.10 - 11.11). kwa upande wa Orthodoksi, imekubalika kwa upana leo hii kwamba Ukanisa wa Ukaristia unasaidia kuelewa ukanisa wa Kanisa la Kale.

**1.5** Swali la jinsi tunavyoshughulikia vitambulisho vyetu vya binafsi leo linahitaji kuelezewa zaidi, kwani hizi zimetofautiana sana na wakati mwingine zimepigwa vibaya hata katika mwendo historia. Ni muhimu tukiwa hapa tukadirie picha tulizo nazo za wenzetu, na ikiwa picha hizi zinahusiana na jinsi washirika wetu kwenye mazungumzo wanajiona.

## 2. Utafsiri wa kitheolojia wa lugha ya theolojia

*Kauli ya Pamoja: Kwenye mazungumzo huwa mara nyingi tunatumia maneno ambayo yana maana tofauti katika tamaduni zetu. Kueleweka kwa maneno haya kumebaridika kwa nyakati. Kwa kawaida huwa na maana Zaidi ya moja na mara nyingi hutafsiriwa tofauti na watu mbali mbali. Kwa hivyo, mazungumzo kati ya Wa-Orthodoksi na Wakatoliki yanahitaji uwazi wa kutosha kuhusu maana ya maneno fulani. Zaidi ya hayo, maneno yanapotafsiriwa kwa lugha tofauti, yanaweza kufikisha kielezi tofauti.*

**2.1** Tafakari yetu ya kitheolojia imefaidika kutoka kwa uzoefu wa Ki-ikiumeniki ambao umeleta katika mazungumzo njia mbali mbali za fikira za Kikristo. Hizi kwa upande wake, kwa wakati, zimeibuka kwa mwelekeo tofauti. Kwa kudumisha haya akilini kunawezesha uelewaji kati ya fikra tofauti za kitheolojia, na husaidia kuondokana na upinzani na mapingo yaliyopo sasa kwa kadiri yanavyoweza kuhusishwa na kutokuelewana na utovu wa kweli kwa njia dhana tofauti zinavyoeleweka. Ufafanuzi wa njia fulani ya fikra ni moja ya kazi muhimu zaidi katika mazungumzo ya Ikiumeniki.

**2.2** Tofauti za ki-mila na kihistoria mara nyingi huwa sababu ya maoni ya kitheolojia na mapokezi yao. Tafsiri ya maoni ya Kiyunani kwa Kilatini na kinyume chake yalikuwa mabadiliko ya kugeuzwa kwenda kwa nyanja nyingine za kitamaduni zilizokuwa na vipaumbele tofauti vya kitheolojia. Hii ilisababisha msukumo tofauti, kwa mfano, maana tofauti za maneno *mysterion* na *sacramentum* au *protos* na *primus* zinavyoonyesha. Tatizo la tafsiri bado zinaathiri lugha za kisasa, ambapo kwa mfano dhana ya "kutokosea kwa Papa" kunatolewa katika lugha mbalimbali na maana mbalimbali (kwa mfano "kutokuwa na dhambi" katika Urusi, "uhuru kutokana na makosa" katika Kigiriki).

**2.3** Kwa uelewaji bora, lazima tugundue ukweli kwamba maneno sawa wakati mwingine yanaelezea mambo ambayo yana tofauti. Mawazo yanayotumiwa na pande zote mbili lakini yanaashiria kweli zinazotofautiana, iwe katika mwendo wa historia au katika zama fulani, ni lazima yafafanuliwe. Hii ni kweli haswa kwa dhana za kikanisa zinazojulikana kama ukatoliki, ukuu (wa ki-kanisa), usawazishaji, muungano wa pamoja, na mshikamano. Kwa hivyo, wazo la *sobornost* katika siku zetu linaweza kueleweka kwa maana ya ukatoliki na mshikamano, lakini linapata muundo haswa kwa hali ya kifalsafa na ya theolojia ya Urusi ya karne ya 19 na 20. Vivyo hivyo, lazima mtu atahadhari kuelewa dhana ya ukuu (wa ki-eklesia)katika maana ya ujumuishaji au wazo la usawazishaji katika maana ya kutojumulisha.

**2.4** Itasaidia sana kukuza pamoja glossaria inayoelezea dhana muhimu za ki-kanisa na kuelekeza hisia za maana tofauti zinazojitokeza wakati wazo linapoonyeshwa kwa Kigiriki au Kilatini, kwa mfano maneno yaliyotumiwa na Baraza la Kwanza la Vatikani kama *potestas immediata* na *plenitudo potestatis* au maneno ya kigiriki *presbeia tes times* na *taxis*.

**3. Utafsiri wa kitheolojia wa mafundisho ya undani**

Kauli ya Pamoja: *tafsiri ya theolojia inayohusu mafundisho ya undani inatilia maanani ukweli kwamba mtu lazima atofautishe kati ya muundo wa fundisho la undani ("kinachosemwa") na taarifa iliyokusudiwa ("kilichomaanishwa"). Ijapokuwa mafundisho ya undani taarifa za mafundisho ya kanisa yasoyoweza kubadilika ama kugeuka, zina muundo wa kihistoria kwa maana kwamba ni athari za changamoto maalum za kitheolojia au za kichungaji katika muktadha halisi na kwa lugha fulani. Kwa hivyo, miundo ya mafundisho ya undani yanao uhaba ki-rasmi na katika yaliyomo ndani yake, kwa sababu hayawezi kuwa usemi kamili wa kile wanachoshuhudia na kujaribu kutafsiri. Hii inalingana na asili ya theolojia ijaribuyo kumweleza Mungu, ambayo inaweza tu kulinganisha na kuelezea siri ya Mungu na kazi yake.*

**3.1** Kanisa halijawahi jaribu kuelezea imani yake kikamilifu na kwa undani wote. Badala yake, mafundisho ya undani yanapaswa kueleweka kama mipaka (*horoi*) ambayo kanisa lilihisi kulazimika kuweka wakati maswali ya ukweli yalipingwa, ili kulinda vyema hazina ya imani iliyohifadhiwa kifuani mwake. Kwa kufanya hivyo, wanatheolojia wengi walikuwa wanajua kuwa yaliyomo kwenye ufunuo ni makuu zaidi kuliko uelewaji wa mwanadamu na kwa hivyo huzidi maoni hayo ambayo hujaribu kuyaelezea. Kama alivyosema Maximus Muungama (ca. 580-662): "Siri kubwa ya kufanyika mtu kwa Mwana wa Mungu daima itabaki kuwa siri".

**3.2** Utengenezaji wa mafundisho ya undani (*dogmas*) kila wakati hunuia muundo fulani wa kuelewa na huingizwa katika muktadha wa utafsiri. Ndio maana mafundisho ya undani hayafai kueleweka tu ki maneno bali yaeleweke pia dhidi ya msingi wa hali ambayo walitoka na nia ya ujumbe wao (taz. §§ 10.1 - 10.9). Utumiaji thabiti wa njia hii katika mazungumzo ya ikiumeniki

imeonekana kuwa na manufaa sana na imeonyesha kuwa mtu anaweza kukubaliana juu ya mada yenyewe, licha ya kutumia maoni mengine wakati mwingine. Kwa njia hii, mazungumzo ya hivi majuzi kati ya Wakaldonia na wasio Wakaldonia yameonyesha kwamba pande zote mbili zimetumia maneno na dhana tofauti kuelezea kimsingi imani ile ile ya Ukristo.

**3.3** Ingawa Kanisa la Orthodoksi na Kanisa la Katoliki haziwezi kushikiria maelewano sawa ya mafundisho, tamaduni zote mbili zinatofautisha, kwa njia tofauti, kati ya mafundisho ya undani (dogmas), mafundisho yanayokubaliwa kwa jumla, na maoni yasiyokuwa ya dhati ya kitheolojia. Juu ya hayo, Vatikani II inazungumza juu ya "uongozi wa ukweli" ili kujibu jinsi mafundisho yanahusiana na msingi wa imani ya Kikristo, wazo ambalo, kwa kiwango Fulani, linalingana na maoni ya wanatheolojia wa Orthodox pia, kama vile Vasilij V. Bolotov (1854-1900). Kwa kukuza tafakari ya kawaida juu ya maumbile ya taarifa za mafundisho, mtu anaweza kutarajia kuchangia kushinda shida zinazokumba tathmini ya mafundisho yaliyoshikiliwa na tamaduni moja pekee.

**3.4** Ni jukumu la utafsiri wa ki-thelojia wa mafundisho ya ndani kukagua uelezaji na utamkaji tofauti (*anaptyxis*) wa urithi wa kimitume katika historia yote, kwa kuzingatia muktadha uliohusika, na kutambua ni kwa kiwango ngapi miundo hii mipya ni maneno halali ya imani kama ilivyoainishwa katika hati za asili.

**3.5** Kazi ya utafsiri wa kitheolojia juu ya amana ya Imani ya Kanisa na juu maneno ya mafundisho ya indani inaweza keulekea ufahamu mpya. Fahamu hizi ni muhimu zaidi mradi zinahusiana wokovu wa wanadamu. Na kwa hivyo, kazi ya utafsiri wa kitheolojia kwa mafundisho ya undani haijumuishi tu kiwango cha nadharia, lakini pia inaweza kusaidia kutathmini maisha na mazoea ya Kanisa.

## 4. Utafsiri wa kitheolojia wa kanuni

Kauli ya Pamoja: *Kanuni za kanisa mara nyingi ukanisa. Kama vile mafundisho ya undani lazima ziwe zikitafsiriwa kwa muktadha wao. Wakatoliki na Wa-Orthodoksi huchukua mitazamo tofauti ya kanuni na wana elewa tofauti uhusiano kati ya sheria za kanisa na mafundisho ya kanisa na mazoea. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwa na majadiliano ya kina ya utafsiri wa kitheolojia wa kanuni - ndani ya kila kanisa na kati ya Orthodoksi na Katoliki. Hali mpya ya kanisa katika milenia ya tatu inahitaji kutafakari zaidi juu ya jinsi kanuni za Kanisa la Kwanza zinaweza kutumika katika ulimwengu wa utandawazi.*

**4.1** Kwa kuzingatia mgawanyiko wetu na uwezekano wa kuishinda, tunapaswa kuzingatia mwelekeo wa kanuni. Sheria za Kanuni mara nyingi zina ushawishi mkubwa juu ya maisha ya kanisa kuliko mafundisho ya undani. Walakini, hata katika milenia ya kwanza msimamo wa kanuni haukuwa sawa na ukweli wa kihistoria. Kwa hivyo, maaskofu walihamishwa kutoka jiji moja kwenda lingine licha ya Kanuni 15 ya Nikea I. Katika milenia ya pili Makanisa ya Orthodoksi na Katoliki walielewa na kutumia kanuni kwa njia tofauti. Ambapo wakati Waorthodoksi walijiweka tu kwa maoni juu ya kanuni zilizokuwepo tayari na wakaunda sheria mpya za kanuni kwa kiwango cha makanisa yao ya mitaani, Wakatoliki waliunda mfumo uliowekwa wa sheria za kanisa ambao kwa sehemu ulikuzwa ukiwa huru kutoka kwa ukanisa.

**4.2** Sababu moja ya utengano kati ya Mashariki na Magharibi ilikuwa kupotea kwa mfumo wa pamoja wa mawazo kuhusu kanuni. Kwa mfano, Mfalme Mkuu Justinian wa pili, kupitia

kanuni za Baraza la Pili huko Trullo, linalojulikana kama *Quinisext* (691-92), miongoni mwa mambo mengine, alilenga kufananisha matumizi na mazoea ya kanuni ya Roma kuwa sawa na ile ya Konstantinopoli pasipo kujali tamaduni za kudumu za hapo awali. Walakini, zile zilizoitwa "kanuni za kupinga Urumi" hazikuchochewa na uadui kuelekea Roma, ila zilitaka kuunda upya usawa ulio bora katika milki mmoja. Kwa upande mwingine, Mageuzi ya Gregori huko Roma yalikuwa sababu ambayo ilisababisha mtazamo wa mipaka kwa ukuu (wa ki-eklesia)kwa kusitiza jukumu la Askofu wa Roma, ambalo halikueleweka kabisa kwa Wabizantini (cf. 8,4).

**4.3** Kwa ujumla, Kanuni zina uzito mkubwa wa kitheolojia katika Kanisa la Orthodoksi; hata hivyo, kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya kihistoria, umuhimu wazo, ama wa baadhi yazo unaondoshwa au kutengwa kama usio maana katika ulimwengu wa leo. Kwa kuzingatia hitaji la kutumia kanuni katika U-Orthodoksi leo, mtu anaweza kuzungumza kuhusu "ngazi za kanuni", yaani kanuni zote kutokuwa na umuhimu sawa. Nikolaj Afanas'ev (1893-1966) alizungumza juu ya ujumbe wao wa kudumu; alisema: "Ukweli wa mafundisho ya theolojia wa kanuni hauwezi kubadilishwa; matumizi na yaliyomo ndani ya kanuni ndio tu yawezayo kubadilishwa na uwepo wa Kanisa katika hitoria".

**4.4** Kwa Kanisa la Katoliki, sheria ya kanuni inayotumika kwa sasa ni Codex *iuris canonici* ya 1983 (kwa Kanisa la Kilatini) na Codex *canonum ecclesiarum orientalium* ya 1990 (kwa Makanisa ya Katoliki ya Mashariki). Kanuni za mabaraza ya Ikiumeniki sasa zinatumika kama *fontes*, hivyo ni kusema, hati za asili, ambapo sheria ya sasa ya kanuni inapata muundo; kwa mfano, kanuni ya 4 ya Nikea I (325), ambayo inasema kwamba maaskofu watatu lazima wawepo katiak uteuzi wa Askofu, ingali inatumika. Pamoja na hayo, kanuni kadhaa za kanisa la awali zimejumuishwa katika mazoea ya kisasa ya liturugia, kwa mfano kanuni ya 20 ya Nikea I (325) kuhusu "*gonyklisia*," ambayo ni kwamba mtu hawapaswi kupiga magoti wakati wa msimu wa Pasaka au siku ya Jumapili. Sheria hii bado inazingatiwa na Wakatoliki wa mtindo wa Bizantini.

## 5. Umuhimu wa mambo yasiyo ya theolojia

Kauli ya pamoja: Sababu za kutengana kwa makanisa yetu hazikuwa tu za kitheolojia, bali pia zilikuwa na kisiasa, kijamii, kimila, kisaikolojia, na mielekezo mingine. Kwa kweli, sababu za kisiasa na kimila zilisababisha sana maendeleo ya miundo ya kidini huko Mashariki na Magharibi. Kwa hivyo, katika kuchunguza sababu na athari za mgawanyiko, jukumu la mambo haya lazima lizingatiwe na kutathminiwa kitheolojia. Hasa, hii inahitaji mbinu pana ambayo pia inazingatia mambo haya ambayo yana umuhimu mchache wa mafundisho ya kitheolojia, ila bado yanaathiri mazoea na utendaji wa makanisa. Mambo kama haya bado yanachangia ugumu katika mazungumzo rasmi ya kitheolojia kati ya makanisa yetu.

**5.1** Kanisa sio la kimungu tu, bali pia la kibinadamu. Hii ndio sababu inaweza kuelezewa sio tu kwa maana nyembamba kwa maneno ya kitheolojia, lakini pia kwa hali ya kijamii na nyinginezo. Kwa kweli, kanisa kwenye historia, ililazimika kuchukua maeneo makubwa ya uwajibikaji ambayo yalihitaji muundo mpya wa mipangilio ya uongozi. Kwa kuwa muktadha wa kijamii na kisiasa ulikuwa tofauti baina ya Magharibi na Mashariki, mifano tofauti ya kidini iliibuka ambayo inapaswa kueleweka kama iliyotoa majibu ya changamoto za enzi iliyolingana. Mara nyingi tafsiri yao ya kitheolojia na uamuzi wa kanuni ulikuja tu baadaye na lazima uonekane kama maelezo ya kihistoria yasioafikiana ya wakati wao.

**5.2** Haifai mtu kuboresha mifano ya zamani kwa kuwekelea mtazamo wa miundo ya baadaye kwenye nyakati za awali, wala kukataa kabisa yaliyopita kwa kuzingatia kila kitu ndani yake kama kisicho maana kwa sasa ikiwa sio hatari kwa maendeleo. Kuelekea kusudi hili, mbinu nyingi zilizoandaliwa na sayansi za kibinadamu kama za sosiolojia, anthropolojia, na saikolojia zinaweza kuwa na msaada mkubwa. Zaidi ya hayo, sababu za kitheolojia na zisizo za theolojia zinastahili kuunganishwa kwa njia yenye usawa, na misimamo ya upande mmoja inapaswa kuepukwa. Kwa kufanya hivyo, mtazamo wa mtu wa kibinafsi wa ukiri haustahili kuelea juu ya kazi ya wasomi ya historia ya kanisa na mafundisho yake (taz. 6.3).

**5.3** Katika mazungumzo ya Orthodoksi na Katolik, kuna mtindo mkubwa wa kukadiria sana milenia ya kwanza. Walakini, katika miaka 506 kati ya 337 na 843 kulikuwa na miaka 217 ya utengano kati ya Roma na Konstantinopoli, kwa hivyo, mtu hewezi kuzungumzia tu juu ya "Kanisa lisilogawanyika" la milenia ya kwanza. Walakini, uzoefu wa milenia ya kwanza unaweza kuwa wa kusisimua sana katika kuunda upya ushirika kati ya makanisa yetu (taz. Sura ya 7).

**5.4** Ingawa kwa njia tofauti na kwa kiwango tofauti, makanisa katika Mashariki na Magharibi mara nyingi yalikuwa yanakabiliwa na jaribu la kuunganisha na uongozi wa kanisa na wa kidunia katika taasisi zake. Wakati mwingine miundo ilishurutishwa kwa kanisa na serikali (taz. §§ 9.8 na 10.2). Changamoto kama vile utumiaji wa nguvu za ulimwengu, tabia ya kudumisha katikati au kujumlisha, pamoja na sisitizo kali juu ya tambulisho la kitaifa, inaweza kuzingatiwa katika Mashariki na Magharibi. Mara nyingi hii imeimarisha mamlaka ya ukuu (wa ki-eklesia)kwa gharama dhidi ya ngazi za usawazishaji. Ingawa nyakati zingine nyingi usawazishaji ulichukua nafasi ya nyuma, haikuwahi kabisa kutoka kwa ufahamu wa kanisa kama kanuni ya kitheolojia. Miundo ya usawa ya aina moja au nyingine ilikuwepo katika maisha ya kanisa kila wakati.

**5.5** Aina za ukuu na usa wa ki-kanisa zimeibuka kwa karne nyingi. Zimo na zitaendelea kubadilika ili kuambatana na mabadiliko mapya kama utandawazi, mabadiliko ya jiografia, na muundo mpya wa mamlaka ya kisiasa, bila kufuata roho ya ulimwengu huu (taz. Rom 12: 2). Hii inamaanisha juhudi ya kila mara ya kurekebisha na kumfanya upya miundo ya kanisa, kwa uaminifu kwa utambulisho wa msingi wa kanisa kama Mwili wa Kristo na kwa utiifu wa misheni yake chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu.

## 6. Umuhimu wa historia kwa theolojia

Kauli ya pamoja: Imani ya Kikristo haiwezekani kuwazika bila kumbukumbu ya historia, kwa sababu ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo ulifanyika kwa wakati maalum wa kihistoria. Kama Yesu wa Nazareti, Mwana wa Mungu ana hadithi ya kibinadamu. Kitendo cha Mungu cha kuokoa wanadamu hakitendeki mbali na wakati na nafasi, ila katikati ya historia ya wanadamu. Kwa hivyo, kujitambua, theolojia, na kuhubiri kwa kanisa pia kumetiwa alama na historia. Utafiti juu ya historia ya kanisa unahitajika kuthamini zaidi jukumu la mambo ya kihistoria, kijamii na kitamaduni katika maendeleo ya theolojia, haswa ambapo maswala ya mgawanyiko yanahusika. Utafiti wa pamoja na uwasilishaji wa pamoja wa historia inayotokana na hili inaweza kutoa muundo wa kuelewa maswali ya kitheolojia yenye utata.

**6.1** Historia ya kanisa inajishughulisha na mienendo ya jumla na iliyo haswa katika Ukristo. Hii inajumuisha kuchunguza maisha ya kanisa katika mafundisho ake ya kitheolojia, ya mfano (imani), liturujia, kanuni, kiroho na mielekeo ya maadili. Zaidi ya hayo, historia ya kanisa hutumia njia sawa na hati za asili vingi kama taaluma zingine za kihistoria, mara nyingi kwa kushirikiana nazo kwa karibu.

**6.2** Kama mfuasi, historia ya kanisa ina umuhimu mkubwa wa kitheolojia. Inazua maswali juu ya tamaduni, mwendelezo, na mabadiliko kanisani, muundo na theolojia yake, na kuwezesha ufafanuzi muhimu wa kumbukumbu za kanisa. Uchunguzi wa kihistoria pia unaweza kusaidia kutia mpaka kati ya enzi ambazo Wakristo walibaki waaminifu kwa injili na wakati, kwa kujua au bila kujua, waliiibatilisha. Historia ya kanisa kwa hivyo inachangia sana katika ukanisa ulio na uwajibikaji.

**6.3** Utafiti katika historia ya kanisa haupaswi kukabiriwa na ushawishi wa kuhalalisha historia ya ukiri wa mtu binafsi au taifa, lakini unapaswa kujadili kwa kina utamaduni wa mtu na tamaduni zingine kulingana na wajionavyo wenyewe. Badala ya kwenda kwa upendeleo na ubaguzi, wanatheolojia wanategemewa kusoma ni ya kiasi kipi kilicho kwenye mafundisho na mazoea ya mwenzi wao wa mazungumzo ili kukuza mazungumzo halisi katika roho ya upendo na ukweli.

**6.4** Hivi majuzi, utafiti wa historia ya kanisa na theolojia uliosawazishwa na tafsiri ya -kitheologia umeleta maoni zaidi yaliyofichika ya masuala yenye utata yanayogawanya makanisa. Mfano thabiti wa hii ni pamoja na: kazi juu ya mtafaruku kumhusu Kristo juu ya maamuzi ya Baraza ya Efeso mwaka wa 431 na Kalcedoni mwaka wa 451 (taz. § 3.2); tathmini mpya ya janga la 1054 (taz. § 8.3); makubaliano ya mwaka wa 1999 kati ya Wakatoliki na Walutheri juu ya kanuni za msingi za mafundisho ya kuhesabiwa haki; au uwasilishaji wa pamoja wa historia ya Marekebisho katika hati ya mwaka wa 2013 na tume ya mazungumzo ya kimataifa ya Wa-Katoliki na Wa-Lutheri. Mfano hii inaonyesha kuwa inawezekana kuelezea historia katika ukiri uliotangamana.

**6.5** Maelezo ya pamoja ya historia, kama ilivyojaribia katika utafiti wa huu sasa, ni muhimu kwa uponyaji wa kumbukumbu. Kwa washiriki wa Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo, juhudi kama hii ni hitaji la lazima la kurudisha ushirika kamili kati ya makanisa yao.

## ***III. Maoni ya Ki-Historia***

### **7. Kipindi cha Kanisa la Kwanza (karne ya 1 - 8)**

Kauli ya Pamoja: *Katika kipindi kabla ya Baraza la Ikiumeniki la Kwanza la Nikea (mwaka wa 325), misingi ya kanisa iliundwa, pamoja na uongozi wa Maaskofu, uongozi wa ngazi tatu, na baraza za mitaa, na pia kukubalika kwa orodha ya Maandiko Matakatifu. Kwa sababu hii, enzi iliyotangulia Nikea ina umuhimu kwa kanisa hadi leo hii. Masuala ambayo yaliyokuwa na utata wakati huo (k.v. tarehe ya Pasaka, kubatizwa tena kwa waasi wa kweli na walio katika utengano) na jaribio la suluhisho lao bado linaweza kutupatia ufahamu wa kushughulikia tofauti za kanisa leo. Katika enzi ya mabaraza ya Ikiumeniki (karne ya 4 - 8), kanisa lilifanyika kanisa la kifalme, kwa kiwango fulani lilfafanuliwa kwenye safu za miundo ya serikali. Hii ilikuwa na athari kwenye mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya kanisa. Mfalme Mkuu*

*alichukua jukumu muhimu katika kuita mikutano ya mabaraza ya ikiumeniki na kutekeleza maamuzi yao. Kama sheria ya jumla, katika kila mkoa Askofu wa mji wa mkoa alisimamia sinodi ya maaskofu na vile vile uchaguzi wa maaskofu na kutawazwa kwao. Katika kipindi hicho Patriaketi zile tano za kale, zilizoitwa "kikundi cha Tano", zilikuwa na jukumu muhimu, haswa katika Mashariki. Askofu wa Roma alikuwa na kazi muhimu, lakini majukumu yake yalitafsiriwa tofauti katika Mashariki na Magharibi. Katika kipindi hiki chote, ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji zilikita katika mvutano wa ubunifu na kila mmoja. Ijapokuwa Mashariki na Magharibi zilielewa mabo haya mawili kwa njia tofauti, uhusiano wa pande zote wa ukuu (wa ki-eklesia)na usawazishaji hata hivyo unajithibitisha kuwa mfano mzuri ambao unaweza kututia motisha njiani mwetumwa kurejesho umoja wa kanisa.*

**7.1** Aina kadhaa tofauti za ukuu au "uongozi" katika makanisa ya mitaani na kikanda yanaibuka katika karne kadhaa za kwanza za Ukristo. Hizi ni pamoja na ukuu wa Askofu mmoja katika kanisa la mtaa flani - kawaida ulikua mji ulio na eneo linalouzunguka - ambalo lilikubaliwa sana katika katikati ya karne ya tatu; ukuu wa Askofu wa mji mkuu (metropoliti) kati ya maaskofu wa mkoa fulani; na baadaye, ukuu wa Askofu wa kituo kikuu cha Jiji Kuu (Roma, Alexandiria, Antiokia, Konstantinopoli, na kwa muda miji zingine kama *Carthage*, Thesalonike, *Milan*, na *Ravenna*) zilizokuwa kati ya makanisa ya "dayosisi" za kisiasa au mkoa wa kifalme (tangia wakati wa mageuzi ya *Diocletian*). Baadhi ya hizi (pamoja na Yerusalemu kama kitovu cha Hija) ziliitwa "Patriaketi" katika mchakato ulioanza katikati mwa karne ya tano (taz. 7.8). Utawala huu wa umetropoli na upatriaka ulitekelezwa kwa kusimamia sinodi za mitaa na za kikanda, na vile vile juu ya kuwekwa kwa maaskofu wa mtaa au wa jiji na kuwa kama upeo wa rufaa katika kesi zinazohusu maaskofu ambao walikuwa wameshughulikiwa hapo awali.

**7.2** Umaarufu wa Rumi kama mahali ambapo Petro na Paulo walifundisha, waliuawa, na palipo na makaburi yao, ulianzisha fahari ya jiji hilo tangu mwanzo, bila kukataa kwamba mitume hao wawili walikuja huko kwa sababu ulikuwa mji mkuu wa ufalme. Ignatio wa Antiokia alilielezea Kanisa la Roma kama lile "linaloongoza kwa upendo" (*prokathēmenē tēs agapēs*). Msimamo wa Roma unaonyeshwa na barua ya kwanza ya Clement kwa Wakorintho, inayosomwa kila mwaka katika liturujia ya Jumapili huko Korintho, juu ya ushuhuda wa Askofu wake Dionysio (ca. 170). Mwisho wa karne ya pili, cheo cha Roma kilikuwa kimeongezeka hadi kwamba Askofu wake Victor I alipojaribu kuwaondoa *Quartodecimans* kwa kuadhimisha Pasaka mbali na ile wengine ilichukua ustadi wote wa upatanishi wa *Polycrates* wa Efeso na Ireneo wa Lioni kuzuia. Andiko zisilozidi mwaka wa 216, kwenye kaburi la Abercio, Askofu wa Hieropoli huko *Phrygia*, linasema kwamba "mchungaji msafi ... aliyetumwa Roma, ili nione ufalme na kumwona malkia akiwa na vazi la dhahabu na viatu vya dhahabu". Cyprian (d. 258) aliunda usemi kwa Roma kama kanisa "ambalo ukuhani wote huanzia", na "*Kathedra Petri*", ambayo, maaskofu wote huketi, na hivyo kuleta kuegemea kwa Askofu wa Kirumi na maaskofu wengine kama mkusanyiko. Kanuni za Sardika ( mwaka wa 343) ziliwapa maaskofu haki ya kukata rufaa kwa Roma (taz. § 7.3). Wazo la "*Roma locuta, causa finita*", linaloegemezwa kutokana na Agastini (d. 430), halikufuatwa na maaskofu wa *Carthage* katika kesi ya Apiario, aliyehukumiwa mara mbili nao, mara mbili aakondolewa lawama na Roma, hadi akahukumiwa kabisa na *Carthage* (418), ambayo alikataza kasisi wa kawaidai kukata rufaa kwa Roma juu ya uchungu wa kutengwa kidini. Uthamini mzito zaidi kwa Roma ulitoka kwa mwanatheolojia mkuu wa Bizantini, wa karne ya 7, Maximos Muungama, ambaye katika muktadha wa ubishani wa *monothelite* aliita "kanisa takatifu zaidi

la Warumi" kama lisilo la kwanza tu kati ya makanisa yote, litoalo mamlaka ya kufunga na kufungua, lakini pia alisema kwamba Wakristo wote wanapaswa kutazama kanisa hili kama "jua la mwangaza wa milele".

**7.3** Jaribio moja la maana na lenye utata la karne ya nne la kuunganisha baraza jipya la ulimwengu lilikuwa Baraza la Sardika (au Serdica; leo Sofia), lililoitwa na Mfalme Konstantio wa II mnamo mwaka wa 343 kwa matumaini ya kuponya kuongezeka zaidi kwa mgawanyiko dhidi ya mapokezi ya imani ya Nikea. Kwa woga kuwa wangetawaliwa na maaskofu wa Kilatino waliozungumza Kilatini ambao walikuwa na nia ya kumrekebisha Athanasio aliye fukuzwa uhamishoni, maaskofu wa Ugiriki hatimaye walikataa kukutana katika baraza la jumla, na badala yake wakahamia Filipopolis huko *Thrace* (leo Plovdiv). Baraza la Magharibi lilitoa mpangilio wa kanuni kuhusu muundo wa kanisa na nidhamu. Kanuni ya 3 ya mkusanyiko wa Ugiriki ilithibitisha haki ya Askofu yeyote ambaye alikuwa ameondolewa na sinodi yake ya mkoa kukata rufaa kwa Askofu wa Roma, ambaye angeweza kuamuru kesi hiyo ifanyike upya. Ingawa Baraza la Sardika hapo awali halikutambuliwa mashariki, kanuni ya 3 baadaye ilichukuliwa kwenye orodha ya 2 ya Baraza ya Pili huko Trullo / Quinisext (691-92), iliyochukuliwa na Orthodoksi kuwa mwendelezo wa Baraza la 5 na la 6 la Ikumeniki. Kwazajili ya mapokezi yao na *Quinisext*, kanuni za Sardika zilifanyika sehemu muhimu ya Kanuni kuu ya Kanisa la Orthodoksi. Kwa kweli, kulikuwa na visa vya kurudia kwa rufaa kwa Askofu wa Kirumi katika mambo ya mafundisho ya theologia na ya utendaji katika milenia ya kwanza, kama vile katika kesi ya Yohana Krisistomu (d. 407), Kirilo wa Alexandria (d. 444), na Theodoro Mstudi (d. 826). Katika milenia ya pili, mtaalam mashuhuri wa Bizantini Theodoro Balsamoni (ca. 1120-98) alitambua katika maoni yake juu ya kanuni ya 3 ya Sardika haki ya kukata rufaa kwa papa wa Kirumi, akitumia haki hii haswa kwa MPatriaka wa Konstantinopoli.

**7.4** Katika miaka ya hivi majuzi, wanatheolojia kadhaa wa Orthodoksi na Katoliki wameelekeza Kanuni ya 34 ya Ki-mitume, ambayo ni sehemu ya mkusanyiko mkubwa wa sheria za liturgia za kutoka kwa Kanisa la Antiokia ambalo lilianzia karne ya 4, kama mfano wa mwingiliano tata wa wa ukuu na umoja wa Uongozi wa pamoja ambao unaonyesha utumiaji bora wa mamlaka ya kanisa. "Kanuni za Kitume" ni kazi ya mwandishi au waandishi wasiojulikana (c. 300) na zilirekodiwa katika lugha tofauti za Mashariki (*Syriac*, *Coptic*, *Ethiopia* na Kiarabu). Zaidi ya hayo, zilipata mamlaka katika Magharibi kwa kuwa Dionisio *Exiguus* (d. Kabla ya 556) alizishirikisha katika mkusanyiko wake wa kanuni. Kanuni ya 34, ambayo labda iliandikwa na wasanifu wa Jumuiya ya Kimitume, ambayo kanuni themanini za Kitume zinaunda sehemu yake ya mwisho, inawakilisha wasiwasi ulioenea kuhusu usawa katika uongozi wa uaskofu ambao uliashiria miongo kadhaa mwishoni ya ubishi wa karne ya nne kuhusu Utatu. Inaashiria kwamba "maaskofu wa kila eneo" - ikimaanisha kila mkoa wa kisiasa - wanapaswa kutambua mamlaka ya "yule anayeshika nafasi ya kwanza kati yao" - yaani Askofu wao wa jiji kuu - na hawapaswi "kufanya jambo lolote la maana (*perittos*) bila ya idhini yake (*gnome*) ", lakini kwamba yeye pia hafai kufanya chochote" bila idhini ya wote". Kanuni hii inasisitiza kuwa, lengo kuu la kila kazi ya Askofu, inapaswa kuwa yale tu yanayohusu kanisa lake la mtaa (*parokia*). Pamoja na Kanuni zingine za ki-mitume, Kanuni ya 34 haikutajwa na kugusiwa sana na wanatheolojia hadi hivi majuzi. Inavyoonekana kwa kutegemea kanuni ya 7 ya Nikea (mwaka wa 325) na kanuni ya 9 ya Sinodi ya Antiokia ya mwaka wa 341, ilionyesha wasiwasi ulioendelea wa kanisa la karne ya nne katika majimbo ya Mashariki kuhusu kuzuia ukuu wa mafundisho na mamlaka ya utawala kwa viongozi wa kanisa wenye nguvu ambao ulishikilia sana mwasho wa kitheologia wa karne ya nne.

**7.5** Jukumu la Askofu wa Roma lazima lionekana katika nyanja tofauti za ushawishi ambapo alifanya maamuzi madhubuti na alielezea vyema tamaduni ya kanisa. Katika Italia ya kati, inaeleweka kuwa, alikuwa Askofu mkuu wa mji mkuu wa kale, na aliita na kutawala sinodi za mji huo. Katika *Italia Suburbicaria* (iliyojumulisha Italia ya kati na Kusini, Sisilia, Korsika, na Sardinia) alitumia utawala wa Metropoliti mkuu, kwa lugha ya baadaye, mamlaka ya Patriaka. Katika karne ya nne, haswa kwa kujibu mzozo wa Arius, nyanja hii ya uongozi iliongezeka polepole kwa sehemu yote ya magharibi ya ufalme wa Kilatini - magharibi mwa ***Rhine***, kusini mwa ***Main*** na ***Danube***, na kuenea hadi mashariki kama Thesalonike na hadi kaskazini kama *Scotland*; hapa maaskofu wa Roma waliwakilishwa mara kwa mara kwenye Sinodi za mkoa, wakitarajia kuambiwa maamuzi ya hizo sinodi, na wangeweza kuulizwa kuhusika kutatua kesi za maamuzi yaliyokataliwa. Tangu wakati wa Papa Damasus (366-84), maaskofu wa Roma walianza kutoa maamuzi, kwa njia ya maandishi ya nyaja za wadhifa, kuhusiana na maswali ya mafundisho na nidhamu ambayo yalitokea katika makanisa kadhaa ya Latini ya magharibi na yaliyokuwa yameletwa kwa kwa utatuzi.

**7.6** Katika makanisa ya Mashariki jukumu la maaskofu wa Roma halikuwa limefafanuliwa vizuri, lakini lilipata umuhimu wakati wa mitafaruku ya kimafundisho katika karne ya nne na ya tano. Mnamo mwaka wa 404 Yohana Krisostomu alituma ombi kwa Papa Innocent wa I, Venerius wa Milan na Chromatio wa Aquilia wampe msaada katika mapambano yake mwenyewe huko Kosnantinopoli. Katika harakati za kwenda kwa Baraza la Efeso (mwaka wa 431), Kirillo wa Alexandria aliunga mkono msaada wa Papa Celestine wa I katika vita vyake dhidi ya Nestori wa Kosnantinopoli. Flavian wa Kosnantinopoli na Theodoret wa Cyrrhus walimwomba Papa Leo wa I, mnamo mwaka wa 449, kwa msingi wa "mamlaka yake ya kitume", afutilie mbali maamuzi kuhusu mafundisho ya Kristo na ya kiutawala yaliyotolewa na sinodi ya Efeso ya mwaka huo huo. Katika kipindi hiki cha vurugu za mivutano kati ya makanisa mitaani, Maaskofu wa Kirumi walikuwa walionekana, kama watetezi wa tamaduni ya kitume, kwa ajili ya uhusiano wao wa Roma. Mfano wa ukweli huu ni kwamba Baraza la kalcedona (mwaka wa 451) lilimshangilia Papa Leo kama sauti ya Petro: "Petro ameongea kupitia Leo". Baada ya kusema hayo, Baraza pia lilikuwa angalifu kusisitiza makubaliano ya Leo na Kirillo: "Kwa kweli na ucha Mungu Leo alifundisha, na ndivyo alivyofundisha Kirillo".

**7.7** Jukumu muhimu la Askofu wa Roma katika muundo wa mafundisho katika maandishi ya viongozi wakuu kama vile Leo wa I na Grigori mkuu halikuonekana kama la kushindana na mamlaka ya maaskofu wa mitaa na wa kikanda au sinodi katika Kanisa la Magharibi, ila lilikuwa la kusisitiza, kukuza, na kuelekeza kazi zao. Wote wawili; Leo na Grigori waliwasihi mara kwa mara Maaskofu wa maeneo ya Magharibi kuhakikisha kuwa Sinodi za mitaa na za kikanda zinakutana mara kwa mara na kufuata utaratibu wa kanuni; Grigori alikuwa akiita sinodi ya maaskofu kutoka Italia *Suburbicaria* (taz. 7.5) huko Roma kila miaka mitano. Wote wawili waliona kusudi la Sinodi za mitaa na za kikanda likiwa ni kupitisha uamuzi wa mamlaka juu ya maswala ya nidhamu na mafundisho; kazi yao wenyewe ilikuwa kuarifiwa kuhusu maamuzi haya, kuyathibitisha, na kuingilia kati katika kesi ambazo uongozi wa mitaa hauwezi kufikia suluhisho mwafaka. Leo - aliyejitambulisha na Petro sana - aliona jukumu lake mwenyewe juu ya yote kama lile la kutangaza wazi imani ya kimitume na mazoea ambayo yalikuwa yamekubaliwa katika makanisa yote tangu enzi za mitume. Wakati wa mitafarku, ilikuwa ni jukumu la mabaraza ya kikanda na ya kiukimeniki kufafanua imani hiyo waziwazi; nalo jukumu la papa lilikuwa "kuweka wazi kile unachojua na kuhubiri kile unachoamini".

Kama vile Leo alivyowaandikia maaskofu kwenye Sinodi ya mtaa kule kalcedoni mnamo mwaka wa 453, kwamba "Je! Enyi mliotawazwa munaweza kutambua kuwa mimi, kwa neema ya Mungu wetu, ni mlezi wa imani ya Katoliki na sheria za mababu zetu?" Kazi yake haikuwa kuelezea imani yake mwenyewe, ila kuweka sambamba imani ya kimitume.

**7.8** Kuanzia pale mwanzoni, kanisa la Mashariki lilikaribia swali la ukuu wa kanisa kupitia mlengo wa uhusiano kati ya patriaketi kuu. Roma ilipewa kipaombele Zaidi ya patriaketi kama vile Aleksandria na Antiokia lakini haikuangaliwa sana Mashariki kama kuwa na mfumo maalum wa mamlaka katika mambo yote. Kanuni za Nikea zilifuata wadhifa wa jimbo hilo, likiongozwa na Askofu wa jiji kuu, kama kawaida, lakini walitambua na kukubali ukweli kwamba mashauri ya Roma, Aleksandria, na Antiokia yalibeba mamlaka ya ziada na haki za kwanza katika maamuzi. Nikea pia huipa Yerusalemu, kwa msingi wa kitamaduni, mahali pa heshima baada ya patriaketi hizi kubwa. Roma na Aleksandria kwa kawaida hutambuliwa kama patriaketi kuu za Magharibi na Mashariki mtawaliwa - kwa mfano katika amri ya Theodosius *'Cunctos populos'* (mwaka wa 380). Lakini mabadiliko makubwa yalianzishwa kwa Konstantinopoli kama Roma Mpya, na kuwa mji mkuu wa ufalme wa Kikristo ulioibuka. Baraza la pili la Ikiumeniki (mwaka wa 381) liliinua Konstantinopoli mahali pa pili baada ya Roma kwa misingi ya kisiasa, mwinuko uliokataliwa na kupingwa na Roma na Aleksandria. Kalcedoni ilienda zaidi katika kutwaa mamlaka ziada kwa Constantinopoli na kufafanua hali yake kama sawa na ile ya Roma isipokuwa katika suala la upeo - tena kwa misingi ya kisiasa. Kwa kuondolewa kwa Yerusalemu kutoka kwa mamlaka ya Kaisari Maritima, mfumo wa falme tano (sheria ya patriaketi tano wa zamani), uliundwa kikamilifu na kikanuni. Utawala huo wa Patriaketi tano unathibitishwa zaidi katika sheria ya Justinia na Baraza la Pili huko Trullo. Hiyo likisemwa, operesheni ya muundo huu wa utawala wa patriaketi tano ilidhoofishwa na mgawanyiko wa Wakaldonia, ambao uligonga Aleksandria na Antiokia kwa nguvu sana. Ushindi wa Waarabu pia ulidhoofisha utawala huo wa patriaketi tano zaidi, ukipunguza sana uwezo wa milango ya Antiokia, Aleksandria, na Yerusalemu wa kutoa mshtumu wowote wa vitendo kwa Roma na Konstantinopoli. Kufikia karne ya nane ilikuwa wazi kwamba utawala huo wa Patriaketi tano ulikuwa imeamua katika mazoea umoja uliojumulisha Roma na Konstantinopoli. Mizozo iliyofuata kati ya Mashariki na Magharibi ilikuwa kwa kiasi fulani matokeo ya Roma na Konstantinopoli kuibuka kama vigogo walioshindana kwa maoni tofauti ya uku (wa kikanisa).

**7.9** Mababa wa kanisa hutupatia ufahamu muhimu juu ya maswali ya ukuu (wa Kikanisa) na usawazishaji. Kwa mfano, Maximo Muungama anapendekeza kwa mfano wake wa binafsi kwamba dhana hizi kwa kweli hazihusu kila mmoja inapohusisha kanisa kwa kiwango cha ulimwengu. Alimhimiza Papa Martin wa I kuita Baraza la *Lateran* la mwaka wa 649 ambalo lilishutumu ubinafsi wa mtazamo kumhusu yesu na ulilichukua sehemu kubwa katika kuchangia maamuzi ya baraza hilo. Kuongezea kwa hayo, kama baba aliyesifika katika makanisa ya Magharibi na Mashariki, kushiriki kwake kunaonyesha kwamba hakuna awaye yule aliye na umiliki binafsi wa ukweli katika kanisa.

**7.10** Katika matendo ya Baraza la Nikea la II (mwaka wa 787), katika kikao cha sita, tunapata makataa kuhusu Baraza la Hiereia mwaka wa (754), ambalo, wakati likishutumu usujudu wa Ikona, lilijifanya kuwa la Kiekiumeniki: “Vipi tena! baraza hili ni 'kubwa' na la Kiekiumeniki’, kwa maana wale wanaosimamia makanisa mengine yote hawakulikubali wala kuliitikia ila badala yake walilitupilia mbali kwa hukumu la kutengwa na Kanisa? Haikuwa na ushirikiano

wa Papa wa Warumi wa wakati huo na makasisi wake, aidha kwa kutumia mwakilishi wake au barua ya idhini, kama ilivyo kwa sheria katika mabaraza. Wala haikuwa na idhini ya Mapatriaka wa Mashariki, hiyo ni ya Aleksandria, ya Antiokia, na Jiji Takatifu, au la makasisi na maaskofu wao". Hapa mtu anaona kwamba msimamo wa papa ulitofautishwa kabisa na ule wa Mapatriaka wengine na kwamba idhini yake ya baraza ilichukua uzito maalum. Ni Dhahiri kwamba Baraza la Konstantinopoli la I (mwaka wa 381) lilikusanyiswa na Mfalme Mkuu kama baraza la mkoa na likapata hadhi ya Kiekiumeniki kwa sababu imani yake baadaye "ilipokelewa" na Baraza la Kalcedoni, wakati maaskofu wa Kirumi, haswa Papa Hormisdas (d. 523) baada ya azimio la mgawanyiko wa Schacian, pia alikubali maamuzi yake ya mafundisho ya kidini mnamo mwaka wa 519, ila akasita kukubali kanuni zake, kwa sababu ya kanuni 3 iliyoipa Konstantinopoli ngazi ya pili ya ukuu baada ya Roma. Wakati Leo wa I alikataa kuidhinisha Kalcedoni kwa sababu ya kanuni ya 28, ambayo ilipeana mamlaka kubwa ya utawala kwa Konstantinopoli, Mfalme mkuu Marcian hata hivyo alimhimiza kuridhia baraza kwa ujumla, kwa sababu msimamo mbadala ungefanya mamlaka yake yahatarishwe.

**7.11** Maoni haya yanaashiria kuwa hadi karne ya 8 hakukuwa na muundo iuliokubalika kwa jumla kueleza uhusiano kati ya Ukuu (wa Kikanisa) na Usawazishaji katika kiwango cha ulimwengu mzima. Ukuu (wa Kikanisa) na Usawazishaji katika Kanisa la kwanza zilitokea, kuonyesha shida za nyakati zao. Zilikuwa zinatendeka, ila hazikutiwa muhuri. Hakuna muundo wowote unaonekana kuwa umekubaliwa ulimwenguni kote. Licha ya ukweli kwamba mabaraza hayo saba ya Ikiumeniki yalitambuliwa na Roma na Patriaketi za Mashariki, uhusiano kati ya ukuu wa Askofu wa Roma na mamlaka ya baraza la kiekiumeniki lilibaki bila kufafanuliwa. Ili kuelewa jinsi ukuu (wa kikanisa) ulipata kielelezo katika mabaraza ya kiekiumeniki, ni muhimu kuzingatia muktadha fulani wa kila kesi, pamoja na mamlaka ya kifalme, migogoro ya mafundisho, na tofauti za kitamaduni.

**7.12** Kutokuwepo kwa ufafanuzi wazi kwa uhusiano kati ya ukuu wa askofu wa Roma na mabaraza ya Ekiumeniki hakumaanishi kwamba hakukuwa na mwingiliano wa ubunifu kati ya ukuu (wa kikanisa) na usawazishaji. Kwa kweli mwingiliano huu kwa mara nyingi ulisaidia makanisa kuendelea kuwa waaminifu kwa Injili. Kwa hivyo, mababa wa mabaraza ya Ekiumeniki - hata ingawa hawakuwahi kuuliza pahala maalum pa Roma na Askofu wake - hawakujibu semi za mara kwa mara za magharibi ambazo zilitaka kuelewa ukuu huu kwa njia ya upana, na kwa hivyo walitoa rekebisho la *silentio* kwa sauti hizi.

## 8. Kipindi cha kutengwa (karne ya 9 - 15)

Kauli ya Pamoja*: Kutatika kwa uhusiano kati ya Mashariki ya Uyunani na Magharibi ya Kilatini yalikuwa matokeo ya mchakato mrefu kwa ajili ya utengano mrefu ambao ulifanyika kati ya karne ya 9 na 15. Hii ilikuwa, kwanza kabisa, imedhamiriwa kitamaduni: kwamba wakati Latini ilieleweka kwa ugumu katika Milki ya Roma ya Mashariki iliyotawaliwa na Uyunani, Yunani haikueleweka hata kidogo huko Magharibi. Pili, kwa hali ya kisiasa, kuondolewa kwa eneo la* Illyricum *ya Mashariki kutoka kwa mamlaka ya upapa na kupotea kwa maeneo yaliyotawaliwa na Bizantini nchini Italia kulisababisha kuondoka kwa wa maaskofu wa Roma kutoka kwa Milki ya Karolingi na kuenea kwa kutoamini kwao dhidi ya watawala wa Bizantini. Tatu, kutoka kwa mtazamo wa kiutawala, Askofu wa Roma alizidi kuchukua nyadhifa ambazo awali zilitekelezwa katika ngazi ya mkoa. Katika nafasi ya nne, kitheolojia, vita dhidi ya Ikona mle Bizantini ilizidisha kuongezeka kwa pengo kati ya Konstantinopoli na Roma. Zaidi ya hayo, utata wa Filioque ulitazamwa na Patriaka Photius*

*wa Konstantinopoli (810-893) kama jabo la kugawanya Kanisa. Kuanzishwa kwa miundo ya kiutawala ya Kilatini baada ya kutekwa kwa Yerusalemu na wanamgambo mnamo 1099 na kuangushwa kwa Konstantinopoli mnamo 1204 kulisababisha pengo kati ya Mashariki na Magharibi kupanuka zaidi. Jaribio la kurejesha umoja, mwanzoni kati ya Walatini na Wabizantini na baadaye ikijumuisha makanisa mengine ya Mashariki, halikuweza kuziba pengo hili. Hata hivyo, hali ya mwingine kama kanisa haikuingiliwa. Baadaye, kushtumiwa kwa ushirikiano huko Magharibi kulisababisha wanatheolojia wengi kuwa na tuhuma ya usawazishaji kwa muda mrefu.*

**8.1** Tabia ya uhasama ya watawala kadhaa wa Bizantini kuhusu Ikona na uhamishaji wa maeneo ya upapa huko Italia Kusini na Illyricum ya Mashariki kuwa chini ya mamlaka ya Patriaketi ya Konstantinopoli ilichangia kugeuka kwa mitazamo ya mapapa kutoka kwa Bizantini kuelekea kwa milki ya waFranki. Kuwekwa taji kwa *Charlemagne* kama Mfalme Mkuu na Leo III Siku ya Krismasi katika mwaka 800 kulileta mvutano wa kisiasa kati ya Konstantinopoli na Roma. Kwa kweli, hakukuwa tena na milki moja lakini mbili na watawala wawili. Mgawanyiko wa kisiasa kati ya Roma na Konstantinopoli ulikuwa utangulizi wa mgawanyiko wa kanisa baadaye.

**8.2** Baada ya Nikea ya II (mwaka wa 787), wanatheolojia wa *Carolingian,* walianzisha mabishano na "Wayunani" juu ya heshima kwa Ikona, ingawa walifanya hivi bila ruhusa kutoka Roma. Kutoelewana kulizidishwa na tafsiri ya Kilatini ya kwanza ya *Acta synodalia*, ambayo ilishindwa kutofautisha vizuri kati ya "uabudu" (*latreía*) na "heshima" (*proskýnesis*). Ya mwisho iliashiriwa kimakosa kama "uabudu" badala ya "heshima". Kisha, mnamo mapema kama mwaka wa 807, mtafaruku mkuu wa kwanza juu ya *Filioque* yalizuka kati ya watawa wa Kiyunani na Kilatini huko Yerusalemu. Hii ilikuja kupata kielekezo chini ya Photios, ambaye alitawazwa Patriaka wa Konstantinopoli mnamo mwaka wa 858. Walakini, sio daraja zote zilizochomwa. Kwa mfano, tafsiri za kwanza za Kilatini za kazi zilizodhaniwa kuwa za Dionysios na za Maximos Muungama zilitengenezwa wakati wa kipindi hiki cha *Carolingian* na Johannes Scotus Eriugena (mwaka wa. 810-77). Zaidi ya hayo, Baraza la Konstantinopoli mnamo 879-80 lilifanikiwa kurejesha ushirika kati ya Roma na Konstantinopoli kwa kumrejeshea Photios kama Patriaka.

**8.3** Mgogoro wa mwaka wa 1054, ambao mara nyingi na uliwasilishwa kimakosa kama chanzo dhahiri cha kuvunjika kwa uhusiano kati ya Roma na Konstantinopoli, ulihusiana na mambo mawili: (a) kuenea kwa Wanomardi (*Normans)* kuingia Italia ya Kusini, kuliharibu muungano wa kisiasa kati ya Roma na Konstantinopoli; (b) Kufuatia kutengwa kwa Armenia na Bizantini mwanzoni mwa karne ya 11, mzozo juu ya utumiaji wa mikate isiyotiwa chachu (*azymes*) kwenye Ukaristia uliibuka tena, na kabla ya muda mrefu pambano hili likaenea hadi kujumuisha Kanisa la Roma, ambalo pia lilitumia mkate usiotiwa chachu. Roma. Hivyo basi, ilimtuma mjumbe Kardinali Humbert wa Silva Candida asafiri kwenda Konstantinopoli kusuluhisha masuala haya mawili ambayo yalikuwa na mzozo. Huko walikutana na upinzani wa dhati wa Patriaka Mikaeli Cerularius. Utovu wa maafikiano baina ya pande zote mbili ulisababisha kuondoana kwenye ukaristia na ushirika wa Kanisa (*Anathema)* kwa pande zote mbili. *Anathema* hii, inapaswa kuzingatiwa kuwa ilihusu tu watu binafsi *(Kardinali Humbert na Patriaka Mikaeli*) na sio Makanisa ya Konstantinopoli na Roma kwa ujumla. Kufikia wakati huo, Leo Wa Tisa (IX), papa ambaye alikuwa ametuma ujumbe wa Warumi, alikuwa amekwisha kufa. Hadi wa leo bado kuna mjadalawa kana kwamba mjumbe huyo wa Roma

alikuwa na haki ya kuendelea. Wakati eneo la *Bari* lilipotekwa na Wanomani (*Normans*) mnamo 1071, Wabizantini walipoteza eneo lao la mwisho la kijeshi nchini Italia, na Roma ikatupilia mbali tumaini lolote la msaada wa kijeshi kutoka kwa Konstantinopoli dhidi ya Wamamani (Normans). Jaribio la Patriaka Petro wa tatu (III) wa Antiokia (mwaka wa 1052-56) la kutafuta patanisho wakati wa mzozo huo halikufaulu.

**8.4** Kwa kuambatana na msingi huu, nyadhifa za ukuu wa Askofu wa Roma zilibadilika kimsingi wakati wa Zama za Kati. Mwisho wa Milki ya Warumi eneo la Magharibi mwaka wa 476 uliliunda utovu wa mamlaka ambao ulijazwa na papa, ambaye kwa hilo aliweza kujidhihirisha kama mweza wa pekee katika mzozo wa Magharibi. Katika mzozo wa uwekezaji (mwishoni mwa karne ya 11 - mapema karne ya 12) kati ya upapa na milki ya Ujerumani, papa alishinda ushindi dhahiri kiasi kwamba jukumu la ustawi wa kiroho wa watu lilikatishwa kutoka kwa mikono ya mfalme mkuu. Maandishi ya *Dictatus papae* (mwaka wa 1075), hati isiyo rasmi ambayo muktadha wake wa kweli haswa bado haueleweki, unaonyesha maendeleo haya. Katika mapendekezo yake 27, inampatia papa mamlaka kuu zaidi kuliko hapo awali, pamoja na haki ya kumuondoa Mfalme mkuu. Ingawa Mageuzi ya Gregori (aliyepewa jina la Papa Gregori wa Saba (VII), (mwaka wa 1073-85) yalilenga kumaliza ufisadi wa kidini, udhalilishaji katika ukasisi na kuingiliwa kwa maisha ya kanisa kwa mfalme mkuu, hati ya *Dictatus* ni mfano wa jinsi mambo kadhaa yawezavyo kuegemea upande mmoja wa mageuzi. Maendeleo haya yanaeleweka kuibua hasira kwa Wabizantini.

**8.5** Kampeni za wanamgambo zilikuwa matokeo ya maendeleo ya kisiasa, kitamaduni na kitheolojia wakati wa karne ya 11 hadi 13 ambazo pia zilileta kujielewa upya kwa mapapa wa Roma. Hapo awali zilikusudiwa kutoa usaidizi wa kijeshi kwa Wabizantini chini ya Mfalme mkuu Alexios wa kwanza (I) (mwaka wa 1081 hadi 1118), ila muda usio mrefu zikawa kifaa cha nguvu cha kukuza uongozi wa upapa na kitambulisho sahihi cha Kanisa la Magharibi. **Uanzishwaji** wa majimbo ya wanamgambo na ukuzaji ya miundo sambamba ya kikanuni, pamoja na kuteuliwa kwa Mapatriaka wa Kilatino huko Yerusalemu, Antiokia, na Konstantinopoli, kulihusiana na uhamasishaji wa upinzani kati ya Wabizantini na Walatini. Kuvurgwa na kusindwa kwa Konstantinopoli mnamo mwaka wa 1204 wakati wa Vita vya Nne vya wanamgambo ulisababisha uhasama wa ndani kwa ndani wa Wabizantini kwa Waroma. kupelekwa kwa Mapatriaka na Wafalme wa Bizantini uhamishoni (ambapo waliishi Nikea hadi kutwaliwa tena kwa Konstantinopoli mnamo mwaka wa 1261) na kuwa kwamba Walatini walitwaa makanisa na Monastiri muhimu za Konstantinopoli (chini ya Mapatriaka wao) kulionekana kuzidisha mgawanyiko huo.

**8.6** Kujiamini zaidi kwa mapapa wa Waroma kulionekana pia katika mabaraza ya zamani ya kanisa la Magharibi. Mabaraza manne ya kwanza ambayo yalifanyikia *Lateran* (miaka ya 1123, 1139, 1179 na 1215) yanaweza kuitwa "mabaraza ya upapa". Hati Maalum ya Papa *Unam Sanctam* ya (mwaka wa 1302) ya Papa Boniface wa Saba (VIII) ilitafsiri nadharia ya "panga-mbili" kumaanisha kwamba wachungaji walikuwa na "upanga wa kiroho" wakati serikali ililazimika kushikilia "upanga wa kidunia" kwa ajili kanisa. Hati Maalum ya Papa ilichochea majibu ya kijeshi kutoka kwa Philipo wa nne (IV) aliyekua mtawala wa Ufaransa, ambaye askari wake walishambulia papa huko *Anagni* (mwaka wa 1303). Katika enzi hii, papa aliingilia kati mara nyingi wakati palitokea shida katika kanisa la mtaa, bila hata ya kusubiri rufaa. Upeo wake kuwa "*vicarius Christi*" (*Vika wa Kristo*) ulitakiwa kumweka juu ya maaskofu, lakini bila kubadilisha hali yao kama maaskofu.

**8.7** Kati ya mambo ambayo yalisababisha mgawanyiko kati ya Waorthodoksi na Wakatoliki, mtu hapaswi kupuuza shida za mamlaka ya kimipaka ya Ekklesia (taz. § 8.1) hilo likiwa pamoja na tofauti za kimafundisho ya kiteknolojia na Kiliturgia kama vile kipengee cha *Filioque* na swali la chachu. Baraza la *Lyons* la pili (II) mnamo mwaka wa 1274, likionyesha hofu ya Mfalme mkuu wa Bizantini Mikaeli wa nane (VIII) Palaiologos kuhusu makaazi mapya ya Kilatino katika Konstantinopoli baada ya mwaka wa 1261, halikufanikiwa kuunda tena umoja wa kanisa kwa sababu haikujadili mjadala mzito na haikupokelewa na Lanisa la Orthodosi.

**8.8** Baraza la *Constance* la kipindi cha (1414 hadi 1418) linaweza kueleweka kama itikio la hali ambayo kanisa la Magharibi lilijikuta wakati huo – lilipojipata limegawanyika dhidi ya "utii" mara tatu ambapo hakuna watakatifu au wanatheolojia, wala wakuu wa Wakatoliki wala daraja na msululu wa waaminifu walijua ni nani papa halisi. Kinachojulikana kama "ushikamano" kilikua kama majibu kwa mgawanyiko wa Magharibi kati ya miaka ya (1378 hadi 1417). Ilikuwa ni njia ya kitheolojia iliyokusudiwa kushinda shida kubwa zinazotokana na msukumo juu ya ukuu wa upapa na, kwa hivyo, ilisisitiza ukuu wa mabaraza juu ya ukuu wa mapapa. Ijapokuwa kuondolewa mamlakani na baraza kwa mapapa wawili wapinzani (John XXIII na Benedict XIII), na kujiuzulu kwa Papa Gregory XII, hakujawahi hojiwa, utendaji wa mshikamano, ulioeleweka kama ukuu wa msingi wa baraza la kidini juu ya papa ulikataliwa mbali. Uhalisi sahihi wa Amri za baraza la *Contance* bado una ubishi hadi wa leo. Papa aliyechaguliwa na baraza hili mnamo mwaka wa 1417, Martin wa tano (V), mara moja alichukua hatua dhidi ya ushikamano mnamo mwaka wa 1418, na mrithi wake, Eugene wan ne (IV) wa mwaka wa (1431-47), alifanya vile vile kwa nguvu zaidi. Kwa kushangaza, nguvu ya upapa ilipewa nguvu na Wayunani, ambao walichagua kujadiliana na kikundi kikuu cha Eugene IV kilichopinga mshikamano katika Baraza la *Ferrara-Florence* wala sio na Baraza la *Basle*. Mshikamano bila shaka ulihukumiwa tu mnamo mwaka wa 1516 na Baraza la Tano la *Lateran*, ambalo liliamua "kwamba Papa wa Roma aliyepo tu, ndiye mwenye mamlaka juu ya halmashauri zote, ndiye aliye na haki kamili na nguvu ya kuitisha, kuhamisha, na kusitisha vikao vya mabaraza". Mjadala juu ya mshikamano unaonyesha kuwa dhana na usawazishaji ulikuwepo ndani ya Kanisa la Katoliki; lakini kwa sababu ya mabishano haya ilikuwa imedharauliwa kwa muda mrefu.

**8.9** Kwenye baraza la *Ferrara-Florence* (mwaka wa 1438-39), Wayunani na Wa-Latini walijihusisha kwa kiwango sawa na kwa njia hii walitambuana kila mmoja kama makanisa, bila kupingwa. Umoja ulikubaliwa mnamo Julai mwaka wa 1439. Wakati wa baraza lilo hilo umoja wa muda mfupi uliafikiwa na makanisa ya Mashariki kama vile Warmeni na Wa-Kopti. Utangazaji wa Agizo la Muungano mnamo Desemba 12, 1452, huko Hagia Sophia liligawanya wabizantini zaidi na kuongeza uchukizo wa makasisi wa Kiyunani na watu kuelekea Walatini. Wagiriki walitarajia sio tu kuunda muungano na Roma, lakini pia kupokea msaada wa kijeshi dhidi ya Waturuki (*Ottomans*). Jeshi kubwa lililoahidiwa na papa kukutana na changamoto hii lilishindwa na Waturuki huko Varna kwenye Bahari Nyeusi mnamo mwaka wa 1444. Muda mfupi baadaye, Konstantinopoli ilitekwa na Waturuki mnamo Mei 29, 1453. Mnamo mwaka wa 1484, miaka thelathini baada ya kuanguka kwa Konstantinopoli, Mapatriaka wote wote wanne wa Mashariki walijiondoa rasmi kutoka kwa muungano huo. Kwa hivyo, baraza lilishindwa katika jaribio lake la kuunda tena umoja wa kanisa. Hata hivyo, ilitumika kama

kielelezo cha baadaye cha umoja wa hapa na pale na Roma (taz. § 9.10), na kwa sababu hii haswa baraza ilionekana yenye kuzidi kuchukiza kwa Wa-Orthodoksi.

**9. Kipindi cha ukiri/maungamo (karne ya 16 - 18)**

Kauli ya Pamoja: *Baada ya kushindwa kwa Halmashauri ya Muungano wa Lyons II (1274) na Ferrara-Florence (1438/39) na kutekwakwa Konstantinopoli na Waturuki (1453), pande zote mbili zilikita kwa msimamo mgumu, ambao uliimarishwa zaidi na Mageuzi ya Kanisa. Mabishano kati ya Orthodoksi na Katoliki pamoja na yale Waprotestanti yalisababisha kuundwa kwa vitambulisho vya ukiri, ambavyo vilikuwa na upinzano na kila mmoja. Katika "Vitabu maalum" ambavyo viliandikwa wakati huu kufuatia muundo wa maungamo ya Kiprotestanti, wanatheolojia wa Orthodoksi walichukua hoja za Katoliki dhidi ya Waprotestanti na hoja za Waprotestanti dhidi ya Wakatoliki. Kwa kuongezea, "muundo wa sinodi" ulioletwa nchini Urusi na Petro Mkuu uliegemea mifano ya Waprotestanti. Katika Kanisa Katoliki, theolojia ya baada ya Tridentine iliegemea kwa kina wazo la wokovu, ambalo liliimarisha juhudi za kimisheni miongoni mwa Wakristo wengine. Katika baadhi ya maeneo, mapatano y ahapa na pale kati ya Orthodoksi na Roma (Brest, Užhorod, et al.) yalitiwa sahihi. Walakini, ni katika karne ya 18 tu ambapo ushirika wa sakramenti, ambao ulikuwa umebaki kutumika katika maeneo fulani, hatimaye ulikatizwa. Hii ilithibitisha matengano ambayo yalikuwa yamekuwepo kwa karne nyingi.*

**9.1** Wakati wa Mageuzo ya kidini, Walutheri walitafuta msaada kutoka kwa Orthodoksi kama ilivyokuwa, wakati fulani baadaye, kwa Wa-Anglikana. Ingawa Wa Orthodoksi walikataa mapendekezo haya, walianza pia kutoa "vitabu vya maungamo", ambavyo havikuhusu tu vyanzo vya jadi vya Orthodoksi, lakini pia vya Waprotestanti na Wakatoliki. Katika karne ya Ishirini (20), Georges Florovsky (1893-1979) alilaani vikali maendeleo haya kama upotovu (*pseudomorphosis*) - jambo ambalo wanahistoria na wanatheolojia wanaendelea kujadili.

***9.2*** Wakati wa kuibuka kwa Mageuzi, ambayo yalikua tofauti katika nchi mbali mbali za Ulaya, Wakatoliki na waOrthodox walizidi kuzingatia miundo ya maungano iliyo egemea kujielewa. Licha ya shida hii ya kupungua kwa utambulisho wa kanisa kwa njia za ukiri, kipindi hiki pia kilishuhudia maendeleo ya ubunifu katika makanisa haya, haswa katika hali ya kiroho, na pia ushawishi pamoja baina ya Mashariki na Magharibi. Kwa mfano, Ignatius wa Loyola (1491-1556), alionyesha wasiwasi mkubwa kwa kuwa mwaminifu kwa mafundisho ya kiroho ya mababa wa Kiyunani, na Wabollandi waliwatafiti kwa kina mababa na watakatifu wa Mashariki. Wadominika kama vile Jacques Goar (1601-53) na Michel Le Quien (1661-1733) walichangia sana katika kukuza masomo ya Ukristo wa Mashariki ya Kati. Kwa upande wa Mashariki, Nikodemu wa Mlima Mtakatifu (1749-1809) akahariri vitabu vya kipekee vya Kiroho kama vile *The Combat* ya Theatine Lorenzo Scupoli (karne 1530-1610). Nayo *Philokalia*, iliyoandaliwa na Nikodemu wa mlima mtakatifu wakiwa na Makarios wa Korintho (1731-1805), ambayo iliyochapishwa kwa mara ya kwanza huko *Venice* (1782), imekuwa na athari kubwa ingawa zisizotoshana kwenye Mashariki na Magharibi pamoja.

**9.3** Muktadha ambao Wakatoliki na Orthodox walijikuta ulileta na mifumo ya elimu ya juu, kama vile taaluma za Wajesuti kote Ulaya na taaluma ya Peter Moghila kule Kiev. Wakati theolojia katika kipindi hiki ilikuwa ya uandishi, walakini wanatheolojia wa kiwango cha Maximos Margounios Mu-orthodoksi (1549-1602) na Mkatoliki kama Leo Allatius (1586-1669) walionyesha waziwazi kuunganishwa kwa makanisa ya kila mmoja wao.

**9.4** Kawaida waandishi wa mashauri ya Orthodoksi walitumia hoja za Katoliki dhidi ya Waprotestanti, kama vile kwenye mzozo juu ya Ukaristia, na hoja za Waprotestanti dhidi ya Wakatoliki, kama katika hoja zao dhidi ya ukuu wa upapa. Vivyo hivyo, Wakatoliki walitumia hoja za Orthodoksi dhidi ya Waprotestanti; kwa mfano, taarifa ya Nikolaos Cabasilas (1321-92) juu ya uwepo halisi katika Ukaristia ilitajwa na Baraza la *Trent*.

**9.5** Ingawa mamlaka ya upapa ilihojiwa kwa nguvu sana na Wageuzi, Baraza la *Trent* (1545-63) halikujihusisha moja kwa moja na ukuu wa upapa na kwa hivyo liliacha wazi swali la mamlaka ya papa katika ufafanuzi wa mafundisho. Hata hivyo, kwenye mazoea, marekebisho katika maisha ya kanisa yaliyoanzishwa na Baraza la *Trent* na kutekelezwa na mapapa yalisababisha ujumulishaji wa mamlaka ya mafundisho katika Kanisa Katoliki na jukumu la nguvu zaidi kwa Kiti cha Kirumi. Tangu wakati huo uaminifu kwa upapa umeendelea kuwa alama ya kitambulisho cha Kikatoliki.

**9.6** Katika karne ya 16, sehemu ya Italia ya Kusini inayojulikana kama *Magna Graecia* ilikuwa nyumbani kwa makumi ya maelfu ya Wakristo Wabizantini. Baada ya Baraza la *Florence*, Jumuiya hii, ambayo ni pamoja na wakimbizi waliowasili hivi karibuni kutoka *Albania*, iliendelea kuwa Kanisa linalojitegemea ila lililo katika ushirika na Kanisa la Roma. Ilipoteza hali yake ya uhuru kwa sababu ya marekebisho ya nidhamu ya baada ya *Tridentine*, ambayo ilisababisha amri ya *Perverbis Instructio* ya mwaka wa 1596. Kwa sababu ya amri hii, jamii hiyo iliwasilishwa kwa mamlaka ya Askofu wa Kilatino wa eneo hilo. Ijapokuwa alinyimwa Askofu wake, ilidumisha hata hivyo mafundisho yake na makasisi wake. Lakini bila unganisho lake kwa Konstantinopoli na kupoteza uhuru wake, ilipunguzwa kuwa dini inayoweza kuvumiliwa ndani ya Kanisa Katoliki (*ecclesia ritualis*). Ilipewa Askofu asiye na mamlaka ya eneo, anayejulikana kama *ordinant*, aliyekaa huko Roma, na ambaye kazi yake pekee ilikuwa ni kutawaza makasisi na mashemasi katika ibada ya Kibizantini. Maendeleo haya yalitoa mfano wa muundo wa *Uyuniati* (taz. § 9.10).

**9.7** Ukweli kwamba Kanisa Katoliki lilikuwa likipoteza hatua kwa hatua kama wakala wa kisiasa aliteka mchakato huu. Kukataa kushughulika na Waprotestanti kulitenga wawakilishi wa Roma katika mazungumzo ya kumaliza Vita vya Miaka thelathini (1618-48), hivi kwamba hata nchi za Kikatoliki mara nyingi ziliweka matakwa yao wenyewe mbele ya yale ya kanisa hilo. Kanisa Katoliki lilizidi kujitizama kindani ndani, likikuza aina mpya za uabudu kama ibada fulani za Mariamu. Wakati maeneo makubwa huko Ulaya yalipotea kwa Kanisa Katoliki kwa sababu ya Mageuzi, viongozi wa kanisa Katoliki walikuwa wepesi kusisitiza umuhimu wa kueneza Injili bara zilizogunduliwa hivi karibuni.

**9.8** Mwanzoni mwa karne ya 18 katika Urusi, Petro Mkuu alijaribu kuifanya nchi hiyo iwe ya kisasa kulingana na mifano ya Uropa, mchakato ambao uliathiri kanisa kwa njia nyingi. Alitambulisha mfumo wa "sinodi" wa serikali ya kanisa na pia alitaka kuinua kiwango cha elimu cha wachungaji. Hii ilisababisha, kwa upande mmoja, mkusanyiko wa usimamizi wa kanisa katika misingi ya Sinodi (ilioiga miundo ya Waprotestanti badala ya ile ya Kanisa la kale), ambayo masilahi ya serikali yalichukua jukumu kuu. Kwa upande ule mwingine - vivyo hivyo kulingana na mifano ya kanisa la Magharibi - malezi ya theolojia yaliboreshwa, na hivyo kuweka msingi wa mafanikio ya theolojia ya Urusi katika karne ya 19.

**9.9** Katika Milki ya Waturuki, muundo wa *Rum-Millet* ulisababisha kanisa la Orthodoksi kijumulika. Kwa sababu hiyo, enzi ya Waturuki, ilishuhudia ukuzaji wa umuhimu wa Patriaketi ya Ikiumenikii dhidi ya Patriaketi zingine za Orthodoksi, ambayo kwa mujibu wa mazoea ya Uturuki yalitiwa kwa dhati chini ya ukuu wa Patriaka wa Ikiumeniki. Hii ingesababisha athari kubwa kwa kanisa hilo katika karne ya 19, wakati harakati za kitaifa ndani ya Milki ya Uturuki zilipozidi kuwa na nguvu, haswa katika nchi za *Balkan*. Wale Waorthodox ambao hawakuwa Wayunani hawakumuona Patriaka wa Konstantinopoli kama mtu ambaye aliwawakilisha, haswa sio katika juhudi zao za kisiasa kufikia etenguzi wa kitaifa.

**9.10** Katika kipindi hiki chote, majaribio yote ya kuunda tena umoja na Roma katika nchi za Ulaya ya Mashariki yalisababisha ushirika wa hapa na pale tu, ambao uligawanya jamii za wenyeji kuwa Wakatoliki na Waorthodoksi. Waliokuwa wa kwanza kujaribu kurejesha ushirika na Roma walikuwa wa Waorthodoksi katika Jumuiya ya Madola ya *Polish-Lithuania* ambao walichochewa na hamu ya kupata usawa na waheshimiwa wa *Poland*. Mnamo 1595 walipeleka maaskofu wawili kwenda Roma kwa mazungumzo, lakini, ingawa walitia saini makubaliano na Roma, sio maaskofu wote waliyakubali katika Sinodi ya *Brest* (1596), kwa sababu walitarajia kuchukuliwa kwa msingi wa baraza la *Florence*, ila sio hiyo ya *Trent*. Baadaye wakaja Waskoki, Waorthodox ambao walikimbia kutoka kwa utawala wa Uturuki huko *Serbia*. Mnamo mwaka wa 1611 walianzisha Kanisa ndogo la Katoliki Mashariki huko Marča, Croatia, wakikita na ibada yao na kubaki wakishirikiana na Patriaketi ya Orthodoksi ya Peć (*Serbia*) na papa vile vile. Mnamo mwaka wa 1646, kwa roho ile ile ya Muungano wa *Brest*, enzi kuu ya *Mukačevo* (sasa katika Ukrania ya *Transcarpathian*), iliyogawanywa kati ya *Hungary* na *Transylvania*, ilijiunga na Kanisa Katoliki, katika Sinodi ya Užhorod. Mnamo mwaka wa 1700, sehemu ya waumini wanaozungumza Kiromania huko *Transylvania* (mnamo mwaka wa 1918 sehemu ya Rumania) walijiunga na Kanisa Katoliki, kama majibu ya shinikizo kubwa la wakuu wa Kalvini, lakini vivyo hivyo kutiwa moyo na suhawishi wa Wayesuti. Kwa kuzingatia ueklesia wa kina wa ubaguzi ambayo ilikuja kutawala baada ya *Trent* kama majibu ya Mageuzi ya Waprotestanti, Wakatoliki wote na WaoOrthodox walihoji kana kwamba jamii iliyo na utengano inaweza kutumika kama chombo cha wokovu.

**9.11** Katika sehemu zingine za ulimwengu wa Orthodoksi Mashariki, kwa mfano., katika eneo la bahari ya Mediterranean, licha ya mvutano usioweza kuepukika, Waorthodoksi na Wakatoliki walikuwa na nyakati za kuishi kwa amani. Ilikuwa tu mnamo Julai 1729 ambapo *Propaganda fide*, kutaniko la Warumi la wamishonari, likaamuru pasiwepo makubaliano ya mawasiliano yoyote katika sakramenti (*communicatio in sacris)* na Wakristo ambao hawakuwa katika ushirika na Roma. Amri hii ni muhimu kwa sababu inaonyesha kuwa kufikia wakati huo aina fulani ya ushirika wa kiliturujia na sakramenti kati ya Orthodoksi na Katoliki ilikuwa bado iko kwenye mazoea (vinginevyo isingekuwa muhimu kuizuia). Jibu kutoka upande wa Orthodoksi kuhusu amri hiyo ya Warumi lilichapishwa mnamo Julai 1755, wakati mapatriaka wa Konstantinopoli, Alexandria na Yerusalemu walitangaza kwamba walichukulia sakramenti zote nje ya Kanisa la Orthodoksi kama batili na watapokea washirika wote wapya wasiokuwa wa Orthodoksi kupitia kwa njia ya Ubatizo tu. Hata hivyo, Kanisa la Orthodoksi la Urusi, liliendelea kupokea waongofu kutoka Kanisa Katoliki kwa kukiri peke yake.

## 10. Kipindi cha usumbufu wa Ekklesia (karne ya 19)

Kauli ya Pamoja: *Katika karne ya 19 Kanisa la Katoliki Magharibi mwa Ulaya lilipata changamoto kwa njia tatu: kikanisa, haswa kupitia kwa Gallicanism; kisiasa kwa kuongeza udhibiti wa jimbo kwa kanisa; na kielimu kupitia maendeleo ya kisasa ya kisayansi. Mwitikio wa changamoto hizi ulikuwa harakati ya ultramontanist, ambayo ingeweza kutoa umuhimu kupita kiasi kwa ukuu wa upapa, kama inavyoonyeshwa katika ufafanuzi wa Baraza la Kwanza la Vatikani. Walakini, ufahamu wa kutosha wa ufafanuzi wa baraza unapaswa kutokea kwa kusoma maendelezo yake kwa uangalifu, wala sio kutoka kwa tafsiri yake kubwa.*
*Katika karne ya 19, msisitizo juu ya wazo la kitaifa katika nyanja ya kisiasa ulisababisha watu fulani wa Orthodoksi kutilia mkazo kanuni za kikabila dhidi ya eneo, na hivyo kupendelea malezi ya makanisa ya kitaifa. Sinodi ya Mapatriaka wa Orthodoksi wa Mashariki huko Konstantinopoli mnamo mwaka wa 1872 ilijibu kwa kulaani ethnophyletism. Walakini, kanuni ya kikabila ya kiekklesia inaendelea kuwa na athari mbaya kwa ushuhuda wa umoja wa Kanisa la Orthodoksi hadi leo.*

**10.1** Katika *Gallicanism* (kutoka Gaul, maana yake Ufaransa), wazo ambalo hurudi katika karne ya 17, wazo la mshikamano, lililolenga kuweka papa chini ya baraza, lilifufuliwa na kufanywa upya katika karne ya 19 kwa kuweka mkazo juu ya uhuru wa makanisa ya kitaifa. Maoni ya *Gallican*, hasa yaliyoenea huko Ufaransa, yalichukua muundo sawa katika *Febronianism* huko Ujerumani (jina hili lilitokana na *Febronius*, jina la Askofu msaidizi wa Trier, Johann Nikolaus von Hontheim, 1701-90). Kinyume na msingi wa mjadala juu ya mshikamano mwishoni mwa Zama za Kati, mawazo ya *Gallicanism* na *Febronianism* yalilaaniwa na mapapa wa wakati huo.

**10.2** Katika ulimwengu wa kisiasa, Kanisa Katoliki lilijikuta linakabiliwa na mabadiliko ya msingi katika uhusiano kati ya taifa na kanisa, kama vile kuungwa mkono kwa kanisa na taifa huko Ufaransa na milki wa Habsburg (kama matokeo ya "*Josephinism*", jina lililotokana na Mfalme Mkuu Yusufu wa Pili (II), aliyetawala kati ya mwaka wa 1780-90), na tishio la kupoteza Mataifa ya Upapa. Zaidi ya hayo, kanisa hilo lilipingwa na ushawishi wa kuongezeka kwa uhuru, ambao ulihusishwa katika nchi nyingi za Ulaya na msimamo mkali wa serikali na mfumo wa kidunia dhidi ya mifumo ya ukasisi.

**10.3** Changamoto ya kiakili ilikuwa katika maendeleo ya sayansi ya asili ya kisasa, katika ukosoaji wa dini ndani ya falsafa na sanaa, na katika utumiaji wa njia muhimu ya kihistoria kwa Maandiko Matakatifu. Maendeleo ya kisayansi yaliyotolewa katika akiolojia, jiolojia, historia, nk, yalizua maswali juu ya uundaji wa jadi wa imani; kulikuwa na hitaji la haraka la kutafuta njia ya kuionyesha Imani vya kutosha katika hali mpya. Changamoto hii ilihitaji kufikiria upya uhusiano kati ya imani na ushawishi wa fikra.

**10.4** Kujibu changamoto hizi, harakati iliyoitwa *Ultramontanism* iliibuka katika nchi kaskazini mwa Vilima vya *Alps* ambazo zilizidisha ukuu wa upapa. Wafuasi wa harakati hii waliamini kwamba uongozi wa papa, akitawala huko Roma "na zaidi ya vilima" (Ultramontane), ulikuwa wa lazima. Walakini, *Ultramontanism* haikuwa harakati tu ya athari lakini pia inaweza kuzingatiwa kuwa mapokeo ya kanisa kwa vikwazo vya jamii ya kisasa. Kupitia mwelekeo mpya wa kuelekea Roma, kanisa hilo lilikuwa likijaribu kujibu Mapinduzi ya Ufaransa na matokeo yake: kutoweka kwa Milki Takatifu ya Roma, kuchora tena kwa ramani

ya Dayosisi za Ufaransa, na kuondoshwa kwa maaskofu wa hizo Dayosisi zote. Walakini, matokeo haya kwa kweli yalisababisha uimarishaji mkubwa wa nguvu za upapa.

**10.5** Harakati ya *Ultramontane*, iliyoungwa mkono na aina mpya za mawasiliano ambayo iliwezesha matamko ya upapa kupokelewa moja kwa moja na umma mkubwa, iliimarisha uhusiano wa kihemko wa wengi walio waaminifu kwa Askofu wa Roma. Chini ya Grigori wa Kumi na sita (XVI) (1831-46) na Pius wa Tisa (IX) (1846-78) upapa wenyewe ulifanyika mmojawapo wa wahusika wakuu katika harakati za *Ultramontane*. Juu ya hayo, jukumu kuu la Roma liliimarishwa na upanuzi wa umishonari wa wakati huo ambao ulielekeza umuhimu wa mipaka ya kitaifa. Papa alizidi kuwa mtu wa pekee katika kuashiria Kanisa Katoliki, ambalo Wakatoliki wengi ulimwengunikote walijitambulisha kwalo.

**10.6** Maoni fulani ya harakati ya *Ultramontane* yalionyeshwa katika ufafanuzi wa Baraza la Kwanza la Vatikani. Ufafanuzi wa mafundisho ya Vatikani waweza tu kueleweka vizuri kwa kuzingatia muktadha wao wa kihistoria, ambao ulikuwa na ushawishi mkubwa juu ya maandishi yake. Uundaji wa mafundisho ya undani juu ya mamlaka ya ulimwengu na kutoweza kuhitilafiwa unaweza kuonekana kama majibu ya changamoto za wakati huo, ukiendelea tabia ya karne zilizopita ya kujumulisha na kujitahidi dhidi ya uhasama wa ndani wa kanisa na shambulio la kutokuamini lilikuwa likienea kote Ulaya. Kwa sababu ya mabadiliko ya miundo ya kanisa katika karne ya 19 ambayo yalitokana na siasa, Kanisa Katoliki kwenye Baraza la Kwanza la Vatikani liliimarisha mamlaka ya papa ili kuhifadhi umoja wa kanisa hilo katika nyakati ngumu.

**10.7** Kinyume na kueleweka kuliopo kwa Vatikani I, na kulingana na usomaji wa hoja za baraza hilo kwa uangalifu, mafundisho ya undani ya mamlaka ya ulimwengu hayamfanyi papa kuwa mtawala kamili, kwa sababu yeye bado anafungwa na ufunuo wa kimungu na sheria za asili na lazima aheshimu haki za maaskofu na maamuzi ya Mabaraza. Kwa kweli, baraza la Vatikani I halikupendekeza mafundisho kwamba "papa hawezi kuhitilafiwa"; badala yake, kwa ufafanuzi mrefu zaidi ilitaja kuwa ni kwa hali gani papa anaweza kuelezea fundisho la kanisa kwa njia isiyohitilafiwa. Kulingana na kujitambua kwa baraza, taarifa kwamba ufafanuzi wa upapa hauwezekani kurufaniwa "kwao wenyewe na sio kwa idhini ya kanisa" (*ex sese, non autem ex Consensu ecclesiae*) haimaanishi kuwa anaweza kufafanua fundisho peke yake pasipo jamii ya kanisa. Papa hatoi fundisho jipya ila hutoa mfano kamili wa mafundisho ambayo tayari yametokana na imani ya kanisa (*depositum fidei*).

**10.8** Kwa utafsiri wa kutosha wa ufafanuzi wa Baraza la Kwanza la Vatikani ni muhimu kujua historia ya hati hiyo (*Textgeschichte*), haswa historia ambayo ilielekeza uchaguzi wa maneno yaliyotumiwa. Kwa hali hii, ni muhimu kwa njia ya kusudi kushugulikia maelezo ambayo yalitangulia upigaki wa kura kuhusu hati hizo. Ni kwa njia hii tu iwezekanapo kufahamu maana halisi ya maneno yaliyokusudiwa na mababa wa baraza hilo. Juu ya hayo, historia ya mapokezi, au kwa maneno mengine., tafsiri iliyofuata ya maazimio yaliyosimamiwa na ofisi kuu ya Kanisa Katoliki, ni ya umuhimu mkubwa kwa ufahamu wa kutosha wa mafundisho ya baraza hilo. Katika historia ya mapokezi "Majibu ya maaskofu wa Ujerumani kwa ujumbe wa Bismarck wa 1875" ni ya muhimu sana, kwa sababu ilipokelewa kama tafsiri yake halisi na Pius IX, papa ambaye aliita baraza hilo. Kulingana na waraka huu, ukuu wa mamlaka ya papa haupunguzi mamlaka ya kawaida ya maaskofu, kwa sababu uaskofu huo unategemea "taasisi ileile ya Kimungu" sawa sawa na ofisi ya upapa. Zaidi ya hayo, kutokosea

kwa upapa "kunagusia uwanja huohuo kama ofisi isiyohitilafiwa ya mafundisho ya kweli ya Kanisa kwa ujumla, na ina upungufu dhidi ya yale yaliyomo kwenye Maandiko na Tamaduni na maamuzi ya mafundisho yaliyotolewa tayari na ofisi ya mafundisho ya Kanisa".

**10.9** Usumbufu na mwisho wa baraza - kama matokeo ya kuzuka kwa Vita vya Princo-Prussian mnamo 1870 na kizuizi kilichofuatia cha Roma kwa Ufalme wa Italia - kilichangia kukosekana kwa usawa katika ekaristi yake: matibabu ya ukuu wa upapaji bila uhuru episcopate na siri ya kanisa lote (cf. § 11.12). Kwa hivyo, Baraza la kwanza la Vatikani haitoi makanisa kamili, haswa kuhusu jukumu la maaskofu, jiji kuu, wazalendo, sinodi, washirika, nk baraza lilikuwa na mapungufu mengine pia: kwanza, matumizi yake ya maneno maalum ya kisheria mara nyingi hubeba maana tofauti katika maisha ya kila siku na kwa hivyo wanahusika na tafsiri potofu; pili, theolojia isiyoelimishwa vizuri na Maandishi Takatifu na historia ya kanisa.

**10.10** Uchunguzi wa kihistoria unaelekeza mtu kutizama kuwa njia nyingi ambazo Vatikani I ilipokelewa, hazikuwa aminifu kwa ufafanuzi wa baraza. Kwa mfano, kutoweza kuhitilafiwa kwa papa sio chanzo cha uwezo wa kanisa kutokuwa na waa ila ni kinyume chake. Mfano mwingine ni kwamba taarifa za mafundisho ya papa hazidai kutokosea kwake, isipokuwa kwa ufafanuzi wa *ex cathedra*. Ni pale tu mtu anapofahamu tofauti hizi kati ya nia ya asili na mapokezi yaliyotokea ambapo inawezekana kushinda mitazamo iliyofuata ya kupoza.

**10.11** Ingawa Baraza la Kwanza la Vatikani lilikuwa mwitikio wa matukio katika jamii ya Magharibi ambayo yametajwa hapo juu, mtu hapaswi kusahau hali yake dhidi ya Mashariki. Njia ya kikanisa ya Jumuiya ya Kikristo ya Mashariki, ambayo inatilia mkazo zaidi juu ya haki za makanisa, iliwekwa kwa mjadala kwenye baraza hilo na maaskofu wa Katoliki ya Mashariki waliokuwepo hapo. Ila wao, kwa kuwa wachache wa maaskofu wa Kilatino, walishindwa kuifanya baraza lizingatie wasiwasi wao.

**10.12** Mafundisho ya Vatikani I yaliyo katika katiba iitwayo *Pastor Aeternus* ya (1870) iliibua pingamizi kutoka kwa idadi kubwa ya maaskofu wa Katoliki, mapadri, na waaminifu. Ndani ya Kanisa Katoliki, ilikuwa ni baada ya miaka kadhaa kwamba maamuzi ya baraza yalikubaliwa na maaskofu wote licha ya kuwepo kwa mambo yaliyowasumbua bado. Baadhi ya makasisi wa Katoliki na watu kadhaa ambao walichukulia baraza hilo kama potovu kwa mapokeo ya tamaduni ya kanisa hilo baadaye walianzisha Kanisa Katoliki la Kale, ambalo baadaye lilikuwa na mazungumzo marefu na Kanisa la Orthodoksi la Urusi. Wakati wa mazungumzo haya, kwa mfano kwenye mikutano ya *Bonn* mnamo 1874 na 1875, ilionekana wazi kwamba tofauti nyingi kati ya makanisa ya Mashariki na Magharibi (kwa mfano, suala la *Filioque*) zaweza kutatuliwa kwa urahisi zaidi ikiwa zingejadiliwa kando na swali la Ukuu.

**10.13** Kuongezeka kwa heshima ya mapapa juu ya tamaduni za Ukristo wa Mashariki kunaweza kudhihirika baada ya Vatikani ya kwanza (taz. maandishi ya Papa Leo wa kumi na tatu (XIII) *Orientalium dignitas*, 1894). Ila hii ilibaki ndani ya mfumo wa umoja ambao haukubaliki kwa Orthodoksi na, kutoka kwa mtazamo wa kisasa, haikufaa kwa marejesho ya ushirika kati ya makanisa yetu (taz. barua ya papa huyo *Satis cognitum*, 1896). Misimamo za kulinganisha inaweza pia kupatikana katika maandishi rasmi ya Kanisa la Orthodoksi la wakati huo (taz. barua ya Patriaka Anthimos wa saba (VII) wa Konstantinopoli, 1895). Hati hizi zimeundwa juu ya msingi wa ukanisa wa undani wa "kurudi" na zinaonyesha mtazamo wa kudhoofisha unaoonyeshwa kwa imani kwamba kila kanisa ndilo pekee linayo ukweli kamili,

na kwamba kanisa lile lingine lina kasoro kwa njia fulani. Hakuna upande wowote ambao kwa wakati huo alikuwa tayari kutafakari kwa dhati msimamo wa yule mwingine.

**10.14** Sawa na huko Magharibi, pia katika Mashariki ule Uangazaji ulizipa taasisi za kanisa zilizokuwepo changamoto. Ulimwengu unaozungumza Kiyunani ulikuwa umegusana na Uangazaji ule katika karne ya 18. Mwanzoni, kulikuwa na athari nzuri, na wasomi wa upeo wa juu (ambao wengi wao walikuwa washiriki wa wachungaji wa Orthodoksi au watawa) walitafsiri safu za kazi za waandishi wa Magharibi juu ya sayansi, hesabu, unajimu na kadhalika, ili hali wengine walitunga kazi kama hizo. Wengi wa waandishi hawa walijihusisha na Uangazaji wa Ufaransa na Ujerumani, ili hali baadhi yao walirudi nyuma zaidi kwa *Descartes* (1596-1650) na *Leibniz* (1646-1716). Kwa upande mwingine, kulikuwa na mwamko wa taratibu wa upinzani dhidi ya baadhi ya mambo ya Uangazaji, kama vile uhuru wa mtu binafsi, kupinga utamaduni, uchumba wa mali, na pambano dhidi ya ukasisi, ambao hapo awali uliibuka katika duru za wapongezaji wa mafanikio ya kisayansi ya Uangazaji na mwishowe kumezua mtazamo hasi kwa upande wa uongozi wa kanisa. Kama matokeo, Uangazaji huo ulitilia shaka kwa wengi, na baadhi ya wafuasi wake hawakuruhusiwa kufundisha katika shule ku za kanisa. Kundi lingine la wanatheolojia liliibuka polepole ambao walikuwa wakichukia Uangazaji na utamaduni wa Magharibi kwa ujumla. Chembe za mzozo huu zaweza kupatikana katika ulimwengu wote wa Orthodoksi hata leo.

**10.15** Falsafa ya kidini ya Urusi ya karne ya 19 na mapema mwa karne ya 20 ikawa sehemu muhimu ya uamsho wa kiroho wa Orthodoksi ya wakati huo. Ililenga majadiliano kati ya "*Slavophiles*" na "*Westerners*" na ikaanzisha uelewaji mpana na ubunifu wa hali ya kisasa ya kisiasa, kijamii na mila ikiwa ni pamoja na dhana muhimu kama "*sobornost*" ya Khomiakov au falsafa ya Soloviev ya "pan-unity". Zaidi ya hayo, ilitoa msukumo muhimu kwa maendeleo ya baadaye ya mawazo ya kitheolojia kwa Warusi waliokuwa nje ya Urusi.

**10.16** Karibu mwanzoni mwa karne ya 20, Waorthodoksi katika Mashariki ya Karibu walihusika kikamilifu katika uamsho wa kitamaduni na kisayansi wa Ulimwengu wa Kiarabu, kwa kawaida ujulikanao kwa jina la Kiarabu *Nahda* (*uamsho mpya*). Wataalamu wa Orthodoksi walitetea wazo la kitambulisho cha Kiarabu kwa jumla bila kujali utofauti wa kidini na kueneza maoni ya Uangazaji wa Ufaransa kuhusu elimu, maendeleo, na sayansi. Mfumo huu wa hali ya juu wa kidunia ulikusudiwa kupatwaa jukwaa la kujumulisha Waislamu mbali na ulimwengu wa kidini na kuweka njia ya mfano wa kijamii iliyo jengwa juu ya fikra. Kwa kadiri kanisa lilivyohusika, Nahda ilithibitisha kuwa jambo la kushangaza: lilichangia, kwa upande mmoja, kuunda mabaraza ya kanisa yaliyo na watu wengi wasio makasisi na utekelezaji wa taasisi za elimu na za kibinadamu kama shule na makao ya mayatima, lakini, kwa upande mwingine, iliongeza pengo kati ya wasomi wasio makasisi na darasa la makasisi wasio na elimu au waliochukuliwa sana na ushawishi wa maandishi baina yao wamishonari wa-Katoliki na Waprotestanti.

**10.17** Uundaji wa makanisa huru ya kitaifa Kusini-Mashariki mwa Ulaya ulihusiana sana na uanzishwaji wa nchi za kitaifa katika karne ya 19. Vitu tofauti ila vinavyohusiana kama vile eneo, kabila, serikali, siasa, na lugha vyote vilichangia. Ufafanuzi zaidi unahitajika kuhusu kiwango cha umuhimu wao wa kikanisa. Makanisa ya kitaifa yalitarajiwa kusaidia katika kuunda serikali za kitaifa na uunganishaji wa vitambulisho vyao vya kitaifa.

**10.18** Ukuaji wa makanisa huru ya kitaifa huko Kusini-Mashariki mwa Ulaya (Kiyunani, Kiserbi, Kirumi na Kibulgari, na vile vile Kanisa la Albania katika karne ya 20) ulifuata mwelekeo tofauti, lakini pia ulionyesha mienendo kadhaa ya kawaida: idadi kubwa ya makabila ya Kusini mwa Ulaya waliishi katika zaidi ya nchi moja, na matokeo yake ni kwamba miundo kadhaa ya kanisa iliibuka kwa kila mmoja wao. Na Zaidi ni kuwa serikali za majimbo mapya ya kitaifa zilitaka makanisa huru kwenye eneo lao, ambayo ilisababisha majadiliano kana kwamba kanisa katika jimbo jipya linapaswa kumaliza uhusiano wake na Patriaketi ya Konstantinopoli. Wabulgari, hata hivyo, walifuata njia tofauti: kwa upande wao, uhuru wa kanisa, ambayo ni kuundwa kwa kikao tawala cha Kibulgari na Sultani, kulitangulia uhuru wa serikali ya Kibulgari.

**10.19** Kuhusiana na utambuzi wa makanisa huru, inapaswa kukumbukwa kwamba makanisa haya yote yaliyokuwa yalikuwa chini ya mamlaka ya Patriaketi ya Konstantinopoli hapo awali. Patriaka wa Ekiumeniki, pamoja na Mapatriaka wa Alexandria, Antiokia, na Askofu Mkuu wa Kipro, waliinukia matarajio ya Bulgari ya kuwa kanisa huru kwa kuhukumu *ethnophyletism* katika sinodi huko Konstantinopoli mnamo 1872; walikataa kukubali mamlaka tofauti kwa wa-Orthodoksi Wabugari ndani ya Milki ya Uturuki kwa sababu hiyo iliweka kanuni ya kikabila juu ya eneo hilo. Hii ilisababisha kukatika kwa ushirika ambako kulitatuliwa tu baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Baada ya uhuru kamili wa majimbo mapya ya kitaifa, uhuru wa makanisa mapya ya kitaifa ulitambuliwa mwishowe na Patriaketi ya Ekiumeniki kwa msingi wa kanuni ya mipaka ya ulimwengu.

**10.20** Hii yote ilisababisha mabadiliko katika uelewaji wa uhuru wa kanisa katika karne ya 19. Haikuzingatiwa tena kuwa suala la mangilio wa kanisa la ndani lakini ikawa ishara ya uhuru kutoka kwa Patriaketi a Ekiumeniki. Uhuru wa kanisa ilionekana kuwa sawa na uhuru wa serikali. Moja ya matokeo ya maendeleo haya yalikuwa ni kuchanganyikiwa kati ya kanuni za kikabila na za mipaka ya kitaifa katika muundo wa kanisa. Hili likawa shida kwa sababu mipaka ya kijiografia ya makabila na mipaka ya majimbo haikulingana kila wakati.

**10.21** Ndani ya theolojia ya Orthodoksi pamekuwapo na mijadala inayoendelea kuhusu maana ya kanuni ya kikabila kwa ukanisa. Hii imefanyika juu ya yote katika muktadha wa majadiliano juu ya njia ya kutwaa uhuru kwa kanisa la Orthodoksi la mkoa, na hapajakuwa na makubaliano hadi leo. Kwa sababu hiyo, mada hiyo iliondolewa kutoka kwa ajenda ya Baraza la Orthodoksi huko Kriti (2016), ambayo ilishughulikia utawala huru wa ndani ya kanisa lililo na uhuru.

## 11. Kipindi cha uamsho wa Ekklesia (Karne ya 20 -21)

Kauli ya Pamoja: *Katika karne ya 20, Wakatoliki wote na Waorthodoksi wamejitahidi kurudi kwenye vyanzo na kukuza ukanisa ambao unazingatia zaidi mfano wa Kanisa la Kwanza. Uchanganuzi wa Ukanisa wa Ukaristia katika Kanisa la Orthodoksi umesababisha kuhojiwa kwa kitheolojia juu ya ushawishi wa kanuni za kikabila na za kitaifa. Haja ya ushirikiano mkubwa wa Kiorthodoksi na mjadala juu ya maswala ya hali ya kisasa na mambo ya baadaye yamekuwa yakisikika zaidi katika duru nyingi za Kiorthodoksi. Kwa upande mwingine, uvumbuzi mpya wa mababa wa kanisa, Harakati za Kiliturughia, na mapokezi ya Ukanisa wa Ukaristia kumeiwezesha Kanisa Katoliki kuondokana na uelewaji mwembamba wa sheria ya kanisa. Hii inaonyeshwa haswa katika hati za Baraza la pili la Vatikani kama* Sacrosanctum

Concilium *na* Lumen Nationsum. *Maendeleo yote yana vitu ambavyo vinaweza kusaidia kushinda mgawanyiko wa kikanisa kati ya Wakatoliki na Waorthodoksi.*

**11.1** Baraza la Mtaa la Kanisa la Orthodoksi la Urusi la 1917-18 lilikuwa jibu kwa hali za kihistoria za nje ya kanisa (vuguvugu la kidemokrasia katika jamii, nk) na kwa umuhimu wa mageuzi ndani ya kanisa. Baraza hilo halikuwa na maaskofu tu, bali pia makasisi na watu wa kawaida. Umbali wa utengano kati ya maaskofu na parokia ulionekana kuwa mkubwa sana hivi kwamba maswali ya kichungaji ya haraka yalipaswa kujadiliwa na kuamuliwa kwa ushiriki wa makasisi na raia. Wakati huo huo ilikubaliwa, hata ndani ya uongozi, kwamba makasisi na raia walihitaji kuhusika katika mchakato wa mageuzi ya kanisa. Ushiriki huu ulianzishwa kitheolojia juu ya wazo la *Sorbonost* na picha ya Mtume Paulo ya kanisa kama Mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:27).

**11.2** Kinyume na historia ya miaka 200 ya kutawaliwa kwa kanisa na taifa (Kipindi cha Usawa) Baraza la Mtaa la Urusi la 1917-18 lilitengeneza muundo wa uongozi wa kanisa ambao ulichanganya hali ya ukuu (kurejeshwa kwa Patriaketi) na mambo ya kusawazisha. Kwa sababu ya mapinduzi ya Bolshevik, mtindo huu haukuweza kutekelezwa katika Kanisa la Urusi. Walakini, bado inaweza kutumika kama kielelezo kwa uhusiano kati ya Ukuu na Usawa.

**11.3** Makanisa yaliyopo ya Orthodox yanatofauti katika uongozi wao wa ndani, kama inavyofafanuliwa katika kanuni za kila kanisa la mahali. Wote wana muundo wa kibaraza, wakiwa na mkutano wa baraza mara kwa mara ukisimamiwa na aliye mkuu kati yao. Walakini, makanisa mengine yamejumulishwa sana, yenye mamlaka kubwa iliyopewa Patriaka, wakati mengine hupeana mamlaka kubwa kwa Baraza la kanisa. Uchaguzi wa Mkuu wa kanisa hufanyika kwa njia tofauti, wakati mwingine na baraza la maaskofu peke yake, wakati mwingine na mkutano wa baraza linalojumuisha wachungaji wa chini na waumini pia. Vivyo hivyo, njia ambayo maaskofu huchaguliwa hutofautiana sana, kutoka kwa uchaguzi wa pekee na baraza la maaskofu hadi uteuzi wa mkutano wa dayosisi, uliojumulisha na makasisi na waumini, na uthibitisho ukafuatia wa baraza. Katika makanisa mengine, waumini raia hawana jukumu katika utawala wa kanisa, wakati kwingine kanisa huweka watu, pamoja na makasisi kuwa na jukumu kubwa.

**11.4** Kama vile kunayo miundo kadhaa ya eneo, vivyo hivyo kuna tofauti ya maoni katika Makanisa ya Orthodoksi ya mtaa kuhusu ukuu wa ulimwengu. Kuhusu suala hili, Orthodoksi kwa kawaida hurejelea usemi "ukuu wa heshima" (presbeia tēs timēs), ila hutofautiana kwa jinsi wanavyo elewa neno hili. Kwa mfano, Kanisa la Orthodoksi la Urusi huelewa ukuu wa ulimwengu kama heshima pekee, wakati Patriaketi ya Konstantinopoli huiona kama wadhifa wa kuita mabaraza, kutwaa uhuru wa kanisa na kusikiliza rufaa, nk. Kwa njia kubwa, kutoelewana huku kumeibuka katika muktadha wa majadiliano na Kanisa Katoliki juu ya ukuu na usawa, ikionyesha kuwa ina umuhimu sio tu kwa Orthodoksi ndani, bali pia katika majadiliano ya Orthodoksi na Katoliki juu ya mambo ya kikanisa.

**11.5** Mikutano ya kibinafsi na wawakilishi wa makanisa ya Magharibi - kwa sehemu moja kama matokeo ya uhamiaji wa Urusi baada ya mapinduzi ya Bolshevik na sehemu fulani katika muktadha wa harakati za ki-ekiumeniki - iliongoza wanatheolojia wa Orthodoksi katika karne ya 20 kutafakari kwa undani kuhusu jinsi Kanisa la Orthodoksi linajielewa. Moja ya matokeo muhimu zaidi ya kipindi hicho ni dhana ya *Ukaristia wa Kikanisa* – ambapo kati ya wawakilishi

wakuu ni Nikolaj Afanas'ev (1893-1966), Alexander Schmemann (1921-83), na John Zizioulas (aliyezaliwa. 1931) - ambayo inaona kanisa la mtaa, likusanyikapo karibu na Askofu wake, kama chanzo cha msingi na mtazamo wa tafakari ya kikanisa. Maono haya yalisababisha kuzingatia kwa undani uhusiano kati ya umoja na tofauti ndani ya Kanisa la Orthodoksi, ambayo yalichangia kuhoji maoni membamba, ya karne ya 19 kuhusu makanisa ya kitaifa.

**11.6** Ndani ya Kanisa la Orthodox wakati wa karne ya 20, mwamko uliibuka na kukua juu ya hitaji la ushirikiano wa U-Orthodoksi wote duniani. Barua ya Patriaka wa Kiekumeni kwa makanisa yote ya Orthodoksi ya (1902) tayari inatoa ushahidi kwa hili. Adhimisho la kumi na sita la Baraza la kwanza la Nicaea (1925) lilitoa msukumo mpya kwa majadiliano kana kwamba itawezekana kukusanya baraza la kiekiumeniki katika karne ya 20. Jibu, baada ya mijadala mikali wakati wa Kongamano la Kwanza la Wanatheolojia wa Orthodoksi huko Athina (1936), lilikuwa hasi. Hitaji la ushirikiano wa dharura wa Orthodoksi uliibuliwa tena katika Mikutano ya U-Orthodoksi wote katika miaka ya (1961-68) iliyokusanyishwa na Patriaka Athenagoras. Hapa na katika mfululizo wa Mikutano mingine ya U-Orthodoksi iliyofuata, wazo la baraza la siku zijazo la Makanisa yote ya Orthodoksi liliundwa. Mkutano wa wakuu wa makanisa kumi na manne ya kanisa la Orthodoksi, uliofanyika Chambésy mnamo Januari 2016, uliamua kukusanyisha "Baraza Kuu na Kuu la Kanisa la Orthodoksi", ila muda mfupi kabla ya kukusanyika makanisa manne (Antiokia, Urusi, Bulgaria, Georgia) yalijiondoa kwa sababu tofauti. Walakini, makanisa mengine kumi yaliyo huru yalikutana siku ya Pentekoste 2016 huko Kurete, na hati sita zilizotengwa kujadiliwa huko Chambésy zilikubaliwa ila kwa marekebisho kadhaa. Wakati nyaraka na barua za baraza hilo huangazia baadhi ya matatizo ambayo U-Orthodoksi unakabiliwa nayo katika karne ya 21, jambo dhahiri muhimu la baraza huko Kurete lilikuwa juhudi kubwa ya kutekeleza usawazishaji katika nadharia na vitendo. Wakati wa baraza, mapendekezo yalitolewa ya kuita mkutano wa aina hii kila baada ya miaka saba au kumi, na hii inaweza kuwa moja ya michango muhimu zaidi ya mkutano huo.

**11.7** Katika Kanisa Katoliki, nusu ya kwanza ya karne ya 20 ilikadiliwa, kwa upande mmoja, kwa kuongeza ujumuishaji kulingana na ufafanuzi wa juu wa mafundisho ya kipapa ya Baraza la Kwanza la Vatikani. Hii ilielezwa, kwa mfano, katika kutangazwa kwa mfumo ya sheria ya kanuni (*Codex iuris canonici*, 1917) ambayo ilikuwa lazima kufuatwa na Wakatoliki wote ulimwenguni (na kwa Wakristo wote kulingana na maoni ya Warumi). Kwa upande mwingine, mwelekeo mpya wa kanisa na mienendo ya kitheolojia uliibuka katika makanisa binafsi (kwa mfano, Harakati ya Liturujia huko Ufaransa, Ubelgiji, Austria, na Ujerumani, au *Nouvelle Théologie* huko Ufaransa) ambayo ilisababisha kupatikana tena kwa ibada ya Kanisa la Mwanzo na theolojia ya Mababa wa Kanisa. Wahusika wakuu wa ufufuaji huu wa kitheolojia (kwa mfano, Lambert Beauduin, Odo Casel, Romano Guardini, Pius Parsch wa Harakati ya Liturujia; na Yves Congar, Jean Daniélou, Henri de Lubac wa *Nouvelle Théologie*) hawakuchochewa kwa njia duni na mawasiliano yao na wanatheolojia wa Orthodoksi ambao walikuwa wamepata makao mapya Magharibi. Chochezi za kitheolojia zilivyotokana na uhusiano huu zimechangia pole pole kushinda mtazamo finyu kwa upapa katika mafundisho ya kanisa Katoliki ya karne ya 19, na hivyo kuandaa uwanja wa Baraza la Pili la Vatikani.

**11.8** Baraza la Pili la Vatikani lilikadiliwa na hamu ya mababa wa baraza "kutwaa nguvu isiyopungua kwa maisha ya Kikristo ya waaminifu" na "kukuza chochote kinachoweza kukuza umoja kati ya wote wanaomwamini Kristo" (*Sacrosanctum Concilium* 1). Hati hii, "Katiba ya Liturujia Takatifu", ilikuwa hati ya kwanza iliyopitishwa na Baraza la Pili la Vatikani. Ilichukua

hisia za kiliturujia ambazo zilikuwa tayari zimeandaliwa kwa kipindi kirefu na kuelezea hamu ya kufanywa upya kwa maisha ya Kikristo. Kwa njia hii hili baraza lilijielewa kama baraza la kichungaji, bila kutafuta kutoa lawama (*anathemata*) lakini badala yake kuwasilisha mafundisho ya kanisa kwa ulimwengu wa kisasa kwa njia nzuri. Ingawa hakukuwa na fafanuzi mpya za mafundisho ya undani, nyaraka za baraza hilo zinafunga na kutoa mwongozo kwa Kanisa Katoliki, lakini zaidi ya hapo pia zina umuhimu wa ki-ikiumeniki.

**11.9** Mojawapo ya maamuzi makuu katika muktadha wa Vatikani II ilikuwa kile kinachoitwa kuondoa lawama za mwaka wa 1054. Usiku wa mwisho wa kumalizika rasmi kwa Vatican II (Desemba 7, 1965), Papa Paulo wa sita (VI) na Patriaka Athenagoras walijiunga na kufutilia mbali lawama hizo katika sherehe ya pamoja huko Vatican na Phanar. Tendo hili la uashirivu, ingawa lilikuwa muhimu, halikutosha kutatua utengano ikiwa ni kwa sababu tu hakuna kuvunjwa kwa ushirika wa kanisa kwa kweli kulikotokea mnamo 1054 (tazama § 8.3).

**11.10** Katiba ya Kanisa, *Lumen gentium*, inarejelea kanisa la kwanza na inasisitiza sakramenti ya kutawazwa kwa askofu na umuhimu wa ushirika wa maaskofu, na hivyo kuongoza kanisa katoliki karibu na msimamo wa Orthodoksi (taz. LG 21 -22). Wakati ikisisitiza kwamba papa anashikilia haki zote muhimu za ofisi yake, katiba hii, kupitia mabadiliko ya muundo, iliimarisha ofisi ya askofu. Walakini, umahiri wa vikao vya maaskofu haujafafanuliwa wazi. Hii ndiyo sababu wanatheolojia wengi Wakatoliki wanaona wezo hizi katika hali yao ya sasa kuwa haziridhishi. Zaidi ya hayo, utekelezaji wa *Lumen gentium* katika sheria ya kanuni inalingana kidogo na maadili ya baraza hilo. Tofauti hizi zimesababisha mjadala unaoendelea ndani ya Kanisa Katoliki juu ya uhusiano kati ya ukuu na usawa.

**11.11** Katika Amri lake juu ya Makanisa Katoliki ya Mashariki, *Orientalium Ecclesiarum*, Baraza la Pili la Vatikani liliimarisha wazi hadhi yao ndani ya Kanisa Katoliki. Walakini, amri hii haikufanikiwa kufafanua wazi umuhimu wa Makanisa Katoliki ya Mashariki na uhusiano wao na Kanisa la Kilatini. Kama matokeo, matakwa ya Patriketi za Katoliki ya Mashariki na Maaskofu wake wakuu kupanua mamlaka yao zaidi ya mipaka yao, ili kuhifadhi tamaduni ya kiroho ya waaminifu wao ambao walikuwa wamehama, bado ni ya kutatanisha hadi wa leo. Hii inalinganishwa na shida zinazohusu mamlaka ya eneo ambayo kanisa la Orthodoksi lililoko Magharibi linakumbwa nayo. Ni bayana kuwa *Orientalium Ecclesiarum* inaonyesha tabia ya muda ya sheria hadi umoja na Waorthodoksi upatikane (rej. OE 30).

**11.12** Vatikani ya pili (II) iliuliza swali ni jinsi ipi uaskofu anaeleweka na jinsi unavyohusiana na huduma ya papa, suala ambalo halikushughulikiwa huko Vatikani ya Kwanza (I), na kujaribu kupata jibu. Kwa kufanya hivyo, mababa wa baraza walichukua ufafanuzi wa Vatikani ya Kwanza (I) juu ya ukuu wa upapa na kuiongezea kwa kusisitiza jukumu la maaskofu. Mambo kadha yakutoridhishwa juu ya ukuu wa upapa ambao yalikuwa yameonyeshwa na wachache huko Vatikani ya Kwanza (I) pia sasa yalizingatiwa. Hii ilikusudiwa kuunda usawa kati ya ukuu na ushirikiano.

**11.13** Mapokezi ya Vatikani ya Kwanza (I) na Baraza la Pili la Vatikani yanaonyesha usawa mpya ambao unathamini tena uaskofu na ushirika wa makanisa ya mahali hapo. Amri juu ya Uekiumeni, *Unitatis redintegratio*, ambayo inaonyesha heshima kubwa kwa Makanisa ya Orthodoksi, inahimiza mazungumzo "kwa usawa" unaolishwa na njia ya kihistoria. Zaidi ya hayo, maandishi ya *Ut Unum Sint* (1995) yaliyotolewa na Papa John Paul II (1978-2005)

inapendekeza "mazungumzo ya subira na ya kindugu" na makanisa mengine juu ya miundo ambayo zoezi la ukuu wa Kirumi linaweza kuchukua katika kanisa lililounganika tena.

**11.14** Vatikani ya Pili (II), ambayo waangalizi wa Orthodoksi walishiriki na kutwaa maoni ya theolojia ya Orthodoksi katika majadiliano ya rasimu, kwa jumla ilikaribishwa na Orthodoksi kama hatua nzuri katika mwelekeo wa umoja. Hata hivyo, kwa maoni ya Waorthodoksi, haikufika mbali katika kutafakari tena mafundisho ya Vatikani ya kwanza (I) ya kutokuhitilafiwa na ukuu wa papa. Vatikani ya Pili (II) pia ilikuwa na athari ya kuchochea tafakari kwa wanatheolojia wa Orthodoksi juu ya maswala ambayo kanisa lao lilikuwa linakabiliwa nayo, kama vile kusanyiko la Baraza la U-Orthodoksi wote ulimwenguni, na mwishowe ilifanya mazungumzo ya kitheolojia rasmi na Kanisa Katoliki iwezekane.

**11.15** Historia ya upokeaji wa Vatikani ya pili (II) hadi sasa inaonyesha kwamba baraza hili bado halijafanikiwa kikamilifu kusawazisha mwelekeo uliopo wa kujikita sana katika Kanisa Katoliki. Ugumu wa kukumbatia usongamano wenye nguvu umesababisha Papa Francis kuweka msisitizo zaidi juu ya mashauriano ya sinodi huru, haswa kwa kutambua jukumu muhimu la mikutano ya maaskofu na Sinodi ya Maaskofu. Na zaidi, tunatambua kuwa Makanisa ya Orthodoksi na yaliyo huru yenyewe pia wanakabiliwa na shida katika ushirikiano wao wa pamoja na katika utekelezaji wa usawa. Kwa hivyo, Waorthodoksi na Wakatoliki wote wanakabiliwa na changamoto ya kujumuisha ukuu na usawa, na itakuwa muhimu na yenye tija kwa makanisa yote mawili kushughulikia maswala haya kwa pamoja, ili kufikia suluhisho linalokubalika kwa pande zote.

## *IV. Makadirio ya kimfumo*

### 12. Jamii / Ushirika kama msingi wa ekklesia

Kauli ya Pamoja: *Ugunduzi wa vyanzo vya kale vya kanisa katika karne ya 20 umesababisha Wakatoliki na Waorthodoksi kutambua kiwango ambacho kanisa linatimizwa katika Ukaristia. Hii inajidhihirisha katika neno la Kiyunani "koinonia", ikimaanisha ushirika wa kisakramenti (communicatio in sacris) na pia ushirika wa watakatifu (communio sanctorum). Ushirika wa Ukaristia ni kielelezo cha asili ya kanisa. Katika adhimisho la Ukaristia, kanisa linajionyesha kuwa watu wa Mungu, mwili wa Kristo, na hekalu la Roho Mtakatifu. Wakati Ukaristia inaadhimishwa, kanisa lipo kabisa lakini sio kanisa lote. Kwa hivyo Ukaristia pia inaashiria umoja mkuu wa kanisa lote. Uelewaji huu wa sakramenti ya kanisa hutoa msingi wa kitheolojia kwa uhusiano kati ya ukuu na usawa kama kanuni ya muundo wa kanisa katika ngazi za mitaa, mkoa, na ulimwengu.*

**12.1** Katika Agano Jipya, kanisa linaelezewa kama watu wapya wa Mungu (taz. Matendo 13: 16-39; 15: 13-21; Warum 9: 24-30), mwili wa Kristo (taz. 1 Kor 12: 12-27), na hekalu la Roho Mtakatifu (taz. 1 Kor 6:19). Mwili wa Kristo ni picha inayopendwa sana na Mtume Paulo kwa kanisa na anaielezea na mwili wa Ukaristia ya Kristo: "Kwa sababu kuna mkate mmoja, sisi tulio wengi ni mwili mmoja, kwa maana sisi sote tunashiriki mkate huo" Wakorintho 10:17). Katika barua kwa Wakolosai, neno hilo pia linatumika moja kwa moja kwa kanisa: "Yeye ndiye kichwa cha mwili lakini mwili ni kanisa" (Kol 1:18). Waraka wa Kwanza wa Mtume Yohana hufanya ufahamu wa *koinonia/communio* katika Agano Jipya wazi wazi: "yale ambayo tumeona na kusikia tunatangaza pia kwenu, ili muwe na ushirika (*koinonia*) na sisi; na ushirika wetu uko pamoja na Baba na pamoja na Mwanawe Yesu Kristo " (1 Yn 1: 3).

**12.2** Neno la Agano Jipya koinonia lina mambo anuwai. Inajumuisha ushirika na Mungu kupitia Kristo ambao waaminifu wanakuwa watoto wa Mungu ambao wanashiriki Roho yule yule, na pia ushirika kati yao wenyewe. Ushirika huu na Mungu na kati yao wenyewe unatimizwa katika *koinonia* ya Ukaristia. Kushiriki Ukaristia ni ishara inayoonekana ya umoja kamili katika Kristo kupitia kwa Roho.

**12.3** Fumbo ya Kanisa imejikita katika fumbo la Utatu Mtakatifu (Taz. Yn 17). Ushirika na Mungu wa Utatu ni msingi wa maisha ya kanisa. Roho Mtakatifu kama chanzo na mpaji wa karama tofauti kwa ajili ya kujenga jamii (taz. 1 Kor 12: 1-11) ndiye wakala mkuu wa *koinonia*. Mizizi ya Utatu ya *koinonia* ni somo la mara kwa mara katika maandishi ya mababa wa kanisa. Alama mbili za kwanza kati ya nne za kanisa zilizotajwa katika Imani ya Nikea (moja, takatifu) pia zinatokana na ushirika wa kanisa na Mungu wa Utatu.

**12.4** *Koinonia* ya kanisa inalishwa na tangazo la Injili na maadhimisho ya sakramenti, chini ya uongozi wa wahudumu wa kanisa waliochaguliwa kutumikia zote mbili. Ukweli wa kanisa kama ushiriki wa Kristo kupitia Roho Mtakatifu unadhihirika kikamilifu kwa nuru ya fumbo la Ukaristia ambayo *koinonia* ya kanisa inapatikana.

**12.5** Kulingana na imani ya pamoja ya Waorthodoksi na Wakatoliki, kanisa ni ushirika wa waumini waliobatizwa waliokusanyika katika Roho Mtakatifu wakimzunguka Kristo aliyepo kwenye mkutano. Hii inahitaji ushirika kati ya makanisa yote ya mtaa, inayoongozwa na askofu. Kila kusanyiko ambalo linaadhimisha Ukaristia chini ya uongozi wa askofu au kasisi kwa ushirika naye hatimaye linajua kuwa iko ndani ya *koinonia* ya kanisa lote.

**12.6** Kutambuliwa kwa ukweli kamili wa fumbo la Ukaristia ni msingi wa kutambuliwa kwa makanisa kama Kanisa la Yesu Kristo. Kwa mtazamo wa Kikatoliki, "kupitia maadhimisho ya Ukaristia katika kila moja ya haya [makanisa ya Orthodoksi na ya Mashariki], Kanisa la Mungu linajengwa na kukua katika kimo" (*UR* 15). Katika Kanisa la Orthodoksi, kuna maoni tofauti kuhusu utambuzi wa hadhi ya kanisa na uhalali wa sakramenti za Kanisa Katoliki; hadi sasa, hakuna makubaliano kamili juu ya hili kati ya makanisa kadhaa ya Orthodoksi.

**12.7** Uelewaji wa kanisa kama *koinonia* hauna tu athari kwa kanisa lenyewe na maisha yake ya ndani, au kwa uhusiano kati ya kanisa. Inamaanisha pia uhusiano na "ulimwengu", yaani, na jamii na wale ambao hawako ndani ya jamii ya Kanisa. Wanatheolojia wengine wa Orthodoksi wamepokea dhana ya "liturujia baada ya liturujia" kwa hili, ambayo inamaanisha kuwa *koinonia* inajidhihirisha pia katika maisha ya kila siku ya Mkristo, na kwamba mkutano wa Ukaristia unaendelea - ingawa kwa njia tofauti - katika Maisha ya Wakristo ulimwenguni: *Koinonia* ya Kanisa huwawezesha Wakristo kutenda kama Wakristo. Kuishi kama Mkristo ulimwenguni hakutenganishwi na uzoefu na kuwepo katika Ukaristia, lakini ni upanuzi wake katika uumbaji wa Mungu. Kanisa Katoliki limetoa maoni kama hayo katika Katiba ya Kichungaji ya Vatikani ya pili (II) juu ya Kanisa katika Ulimwengu wa Kisasa *Gaudium et Spes*

## 13. Mamlaka kanisani katika huduma ya jamii

Kauli ya Pamoja: *Kila huduma kwa umoja wa kanisa inahitaji mamlaka ambayo inaweza kutumika kwa njia ya ukuu na ya ki-sinodi au usawa. Mamlaka ya aina hii yanategemea kipaji kutoka kwa Mungu, karama ya uongozi (taz. Warumi 12: 3-8, 1 Wakor 12: 4-11; Waefe 4: 7-12), na majukumu yake ni pamoja na kutangaza kwa imani, maadhimisho ya sakramenti, kuhifadhi mafundisho, na mwongozo wa watu wa Mungu. Mamlaka ya "Wa Kwanza" (Primus / Protos) ni aina ya kibinafsi ya mamlaka katika huduma ya jamii. Kristo mwenyewe ametupa mfano wa jinsi mamlaka inavyopaswa kueleweka: kama huduma ambayo inajumuisha kuwa tayari kujinyima ("kenosis", taz. Wafilipi 2: 5-11; Mt 23: 8-12). Aina kuu za Ukuu na usawa hutambuliwa kama hivyo kupitia mchakato wa mapokezi ambayo hufunua mamlaka ya watu*

*wote wa Mungu (plērōma) inayohifadhi mafundisho ya kweli kwa "hali ya imani" (*sensus fidelium*).*

**13.1** Katika kila jamii ya wanadamu, matukio ya mamlaka na nguvu yapo. Tofauti inapaswa kufanywa kati ya matukio haya mawili. Mamlaka yanahusu ushawishi wa mtu au taasisi ambayo msingi wake ni utamaduni au umahiri na heshima inayopatikana kutoka kwake. Nguvu, kwa upande mwingine, inahusiana na uwezo wa kutumia njia na taratibu fulani ili kuleta maamuzi. Zote mbili zinaweza kutumiwa vibaya kwa urahisi.

**13.2** Mawazo ya mamlaka na nguvu hupata umuhimu fulani ndani ya Kanisa. Nguvu (*dynamis*) inaonekana kwanza kama sifa ya Mungu (taz. Ufu. 7:12). Maandiko ya kiroho yanaonyesha nguvu zake juu ya "miungu" yote na juu ya uumbaji (taz. Zab 82:1). Kwa maana hii, nguvu yake kuu inaweza kutambuliwa na utukufu wa Mungu (taz. Zab 63:2; Waebr 1:3). Nguvu hii daima inahusiana na upendo wake kwa Israeli na wanadamu wote, zawadi yake ya wokovu, msamaha wake, na, haswa, rehema yake (taz. Hosea 2:19). Agano Jipya linaona nguvu za Mungu kama kutenda kazi katika Yesu (taz. 1 Wakor 1:24). Kristo aliyefufuka, ambaye alikuwa amepokea kutoka kwa Mungu mamlaka kamili (exousía), aliwatia nguvu mitume ndani na kupitia kwa Roho wake Mtakatifu (taz. Mt 28:18-19). Kufuata amri ya Yesu, mamlaka katika Kanisa haipaswi kueleweka kama kutawala lakini kama huduma kwa watu wa Mungu kulingana na nguvu ya Msalaba.

**13.3** Katika Kanisa, kuna watu wenye karama tofauti wanaopokea na kutumia mamlaka katika maeneo tofauti tofauti, kama vile Waefeso 4:11 inavyoonyesha: "Na karama zake zilikuwa kwamba wengine wawe mitume, wengine manabii, wengine wainjilisti, wengine wachungaji na waalimu." Hii inaonyesha kwamba mamlaka katika kanisa inapaswa kuunganishwa kila wakati na jamii. Hii inatumika kwa huduma ya utawazaji, haswa kwa huduma ya askofu ambayo imepata umuhimu wa pekee kwa maisha ya kanisa kwa karne zote. Walakini, wabambe kama vile Mkuu Silouan wa Mlima Athos na Mama Teresa zinaonyesha kuwa mamlaka ya kiroho haionyeshi huduma iliyowekwa juu ya huduma iliyotawazwa.

**13.4** Kwa kuwa Kristo ndiye kichwa cha Kanisa, ndiye chanzo cha mamlaka yote ndani ya Kanisa, bila kujali ikiwa hii inatekelezwa na mmoja (Kasisi Mkuu), na wengine (sinodi), au na wote (watu wa Mungu). Mamlaka ya sinodi na ya yule anayeisimamia ni msingi wa fumbo la Kanisa kama mwili wa Kristo katika Roho Mtakatifu. Usawa, kama mwelekeo muhimu wa Kanisa, unaonyesha siri yake, na, kwa hivyo, imeunganishwa na mamlaka ya watu wote wa Mungu ambao, kupitia "hisia yao ya imani", wakiamshwa na kudumishwa na Roho Mtakatifu, wanaweza kutambua ni nini kweli kilicho cha Mungu.

**13.5** Matumizi yoyote ya nguvu katika Kanisa yana maana tu ikiwa yanatekelezwa kulingana na mfano wa Kristo aliyesulubiwa, kama huduma na sio njia ya kuwatawala wengine (taz. Marko 10: 42-45 na kiasi; Yoh 13: 1- 17). Hii inatumika pia kwa zoezi la ukuu katika viwango vyake tafauti tafauti. Njia ambazo wanapewa wale wanaotumia ukuu zapaswa kutumiwa tu kwa roho hii. Hii ni pamoja na kuwajibika kwa jamii katika ngazi tofauti.

## 14. Utafsiri wa kitheolojia wa usawazishaji

Kauli ya Pamoja: *Kristo ndiye kichwa pekee cha kanisa. Yeye ni mfano kwa wale wote wanaotumia huduma ya utawala kanisani. Maandiko Matakatifu yanashuhudia kwamba, hata kama aina ya utawala iliweza kuwa shwari aje, ilikuwa muhimu kwa jamii za Kikristo tangu mwanzo. Ushuhuda wa mababa kutoka karne ya pili na kuendelea unaonyesha ukweli kwamba haiba ya kusimamia ilikabidhiwa kwa mtu ambaye jukumu lake lilikuwa kushuhudia, kukuza, na kulinda umoja wa kanisa. Kazi hii inafanywa katika viwango tofauti tofauti vya maisha ya kanisa kwa njia tofauti na kwa msisitizo tofauti.*

**14.1** Katika Agano Jipya, safu ya vifungu inaonyesha kwamba jamii za Kikristo zilikuwa na viongozi tangu mwanzo. Katika moja ya maandishi ya zamani kabisa, Mtume Paulo anawahimiza wanajamii kuwatambua na kuwaheshimu viongozi wao (*proistamenoi*): "Lakini tunawasihi, ndugu, waheshimu wale wanaofanya kazi kati yenu na ambao wako juu yenu katika Bwana na kuwashauri."(1 Wathesalonike 5:12). Maandiko mengine yanaonyesha uwepo wa aina za huduma za mapema zilizotumiwa na watu walioitwa maaskofu na mashemasi (kwa mfano, Matendo 20:28; Wafilipi 1: 1). Agano Jipya haitoi picha thabiti ya huduma hizi na huacha maswali mengi wazi juu ya kazi zao sahihi.

**14.2** Kulingana na Agano Jipya, wakati wa huduma yake ya kidunia Yesu alichagua kama wenzake wa dhati wale Kumi na Wawili, akawapa nguvu (*Dinamis*) na mamlaka (exousia) kuhubiri Injili, kuponya na kutoa pepo wabaya (Lk 9: 1) , na kuahidi kwamba watakuwa waamuzi wa maisha yajayo juu ya Israeli (taz. Mt 19:28; angalia pia Ufu. 21:12). Watatu kati yao, Petero, Yohana, na Yohana, Yakobo walikuwa na nafasi maalum kwa kadri walivyochaguliwa kuwa na Yesu katika hafla maalum kama vile kugeuzwa sura kwake (Mk 9: 2-10), au katika bustani ya Gethsemane kabla ya yeye kukamatwa (Mk 14: 32-42). Paulo anashuhudia kwamba Yakobo, "ndugu wa Bwana", pamoja na Petro na Yohana, walitazamwa kama "nguzo" za jamii huko Yerusalemu (Wagalatia 2: 9).

**14.3** Petro hufanya kazi kama shahidi maalum wa ufufuo katika muktadha wa imani ya Kikristo ya zamani kabisa ambayo inaweza kupatikana katika barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorintho: "na kwamba yeye (yaani Kristo aliyefufuka) alimtokea Kefa, kisha kwa wale kumi na wawili" (1 Wakorintho 15: 5). Licha ya tofauti zilizo wazi, Injili zinakubali kwamba jukumu maalum lilikabidhiwa Petro katika kikundi cha wanafunzi. Kwa hivyo, katika Injili ya Luka Yesu anamwagiza awatie nguvu ndugu zake (Lk 22:32) na katika Injili ya Yohana anamwamuru awachunge wana-kondoo na kondoo (Yn 21: 15-19). Katika kifungu cha kwanza, maneno ya Kristo yamewekwa ndani ya Karamu ya Mwisho, na kifungu cha pili huamsha hisia za Ukaristia. Wakati huo huo Wainjilisti kwa njia yoyote hawafichi udhaifu wa Petro, lakini hata wausisitiza: Petro anamkana Bwana mara tatu na anahitaji msamaha (Lk 22:34 na 61-62). Katika Injili ya Mathayo lahaja ya hali maalum na udhaifu hufikia kilele chake: Petro, ambaye ameteuliwa kupokea funguo za ufalme wa mbinguni (Mt 16:19), anaitwa "Shetani" anapojaribu kumzuia Bwana kwenda njia ya msalaba (Mt 16: 21-23). Ingawa alihusika katika mjadala na Paulo juu ya ushirika na Wakristo wasio Wayahudi (taz. Wagalatia 2: 11-21), Petro anafurahia heshima maalum na anaonyeshwa kama mpatanishi wakati wa mivutano na mizozo (taz. Matendo 15: 6-14).

**14.4** Mapema sana Kanisa la Roma lilihusishwa na Petro na Paulo, ambao walimshuhudia Kristo na kuuawa kama shahidi huko Roma (taz. § 7.2). Kuheshimiwa kwa makaburi yao huko Roma, pamoja na umuhimu wake kama mji mkuu wa kifalme, kuliunda msingi wa msimamo maalum uliopewa Kanisa la Roma na, kama matokeo, kwa askofu wake, kutoka karne ya tatu na kuendelea.

**14.5** Msimamo maalum wa Petro ndani ya chuo cha wale Kumi na Wawili, kama inavyoshuhudiwa na Maandiko Matakatifu, pia inaonyeshwa katika tamaduni ya kiliturujia na kawaida inahusishwa na jukumu la kipekee la Paulo kwa sababu ya utume wake kati ya watu wa mataifa. Ibada zote mbili za Kirumi na Ki-Bizantini zinamkumbuka Mtume Petro pamoja na Mtume Paulo mnamo Juni 29. Katika ibada ya Kirumi ni sherehe; katika jadi ya baadaye ya Ki-Bizantini, sikukuu ya Mitume inatanguliwa na kipindi maalum cha kufunga ambacho kinasisitiza heshima ya Mitume hawa wote.

**14.6** Katika barua za Ignatios wa Antiokia, ambazo zilianzia karne ya 2, askofu anaonekana kama mdhamini wa umoja wa kanisa. Hii labda inapaswa kueleweka kwa kuzingatia wasiwasi wa mwandishi kwamba kizazi cha mitume na wanafunzi wao wa karibu kilikuwa

kimeshakwisha. Zaidi ya hayo, kulingana na Kipriano wa Carthage (d. 258) kila askofu, kama mrithi wa mitume, anakaa kwenye "Kiti cha Petro". Kwa Kipriano, hali maalum ya Petro, ambayo Injili ya Mathayo inashuhudia, inamaanisha umoja wa maaskofu. Huduma ya maaskofu mwishowe ilionekana kama njia ya kuendeleza urithi wa kitume na kuufanya kuwa ukweli wa sasa.

**14.7** Hadhi ya kanisa kwa ukuu katika kiwango cha mkoa imeelezewa katika Kanuni ya Kitume ya 34 (taz. § 7.4). Ingawa kanuni yenyewe imeundwa kwa njia isiyo wazi, haswa kwa sababu hali hiyo ilitofautiana kutoka mkoa hadi mkoa (kwa mfano, mazoezi tofauti ya ukuu huko Alexandria na Antiokia), inaonyesha matumaini na matarajio ya karne ya 4. Kutoka kwa Kanuni ya 34 tunajifunza jambo muhimu juu ya mienendo ya Ukuu - utegemezi kwa Kasisi wa Kwanza na sinodi yake.

**14.8** Kudumisha umoja wa kanisa ni jukumu la washiriki wake wote. Walakini, "wa kwanza" kati yao anapaswa kuitunza kwa ubora. Kazi kama hiyo ya utawala ni pamoja na upatanishi, kuhifadhi usawa kati ya umoja na utandawazi, na kutoa hesabu ya hii. Maneno ya Yesu yanahusu utekelezaji wa huduma hii: "Ikiwa mtu yeyote atakuwa wa kwanza, lazima awe wa mwisho kwa wote na mtumishi wa wote" (Marko 9:35).

**14.9** Pamoja na mabadiliko ya miundo ya kanisa na kutofautisha kwa viwango vyake tofauti tofauti, zoezi la ukuu pia likawa la kuhitajika zaidi. Hata hivyo bado ni muhimu kwa kila ngazi ya kanisa hadi leo: mkutano wa mtaa, dayosisi, mkoa wa kanisa / mji mkuu, Patriaketi, na kanisa zima ulimwenguni. Utekelezaji wa ukuu hutofautiana kulingana na viwango tofauti kanisani. Kwa hivyo, ukuu katika kanisa la mkoa sio sawa na ule wa askofu katika dayosisi yake, kwa sababu, katika jimbo hilo, askofu ana huduma maalum kama yule anayehakikisha ushirika kati ya kanisa lake na makanisa mengine ya eneo hilo.

**14.10** Ni muhimu kabisa kuzingatia muktadha fulani wa kihistoria wa kila taarifa juu ya ukuu, historia ya ukuzaji wake, umuhimu wake kwa wakati wake mwenyewe, na pia historia ya athari zake. Kwa mfano, kwa askofu wa Roma, tofauti inapaswa kufanywa kati ya ukuu wa enzi ya mamlaka na kutokosea kwake. Kama matokeo ya ufafanuzi wa ukuu wa mamlaka ya eneo, Eneo la utawala la Roma liliongezeka kwa umuhimu katika kipindi cha baada ya Vatikani ya Kwanza (I). Kuhusu kutokukosea, ni muhimu kutambua kwamba, katika kipindi cha takriban karne na nusu tangu Vatikani ya Kwanza (I), mapapa wa Roma wametegemea mara moja tu kwa tangazo la zamani la kanisa kuu, ambayo ni kutangaza fundisho la Kuingia kwa Maria Mbinguni (1950).

**14.11** Uelewaji bora wa dhana ya Katoliki ya ukuu katika kiwango cha ulimwengu wote inaweza kupatikana kupitia tofauti iliyo wazi kati ya nafasi ya kipekee ya papa katika Kanisa Katoliki na kazi yake kama mkuu ndani ya jamii pana ya Kikristo. Jukumu la askofu wa Roma katika milenia ya kwanza, kama ilivyoelezewa katika sura ya 7 ya utafiti huu na katika hati za Ravenna na Chieti za tume ya kimataifa ya Orthodoksi na Katoliki, inatoa hoja muhimu ya kuondoka kwa swali hili.

## 15. Utafsiri wa kitheolojia wa usawazishaji

Kauli ya Pamoja: *Maandiko Matakatifu na tamaduni ya kanisa hushuhudia ukweli kwamba utawala wa kanisa unategemea kanuni ya sinodi kama ilivyoonyeshwa, kwa mfano, katika ushirika wa mitume na sinodi za kanisa la kwanza. Kanuni hii ya sinodi lazima pia ifikie viwango vyote vya maisha ya kanisa kulingana na eneo husika la uwajibikaji.*

**15.1** Kanuni ya sinodi ina mfano wa baraza la mitume la Yerusalemu (Matendo 15). Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaelezea jinsi "mitume na wazee" (Matendo 15: 6), walipokabiliwa na shida ya usumbufu wa tohara, walivyokusanyika Yerusalemu na Yakobo akiongoza. Huko,

shida ilijadiliwa waziwazi. Uamuzi wa mwisho kwamba tohara haingewekwa kama sharti ilitumika kujenga jamii (Matendo 15:28). Mtu anaweza pia kuona kanuni ya sinodi iliyotarajiwa katika kukusanyika kwa "ndugu 120" wakati ambao Mathia alipokelewa kwenye muungano wa mitume kuchukua nafasi ya Yuda (Matendo 1: 15-26).

**15.2** Sinodi za mkoa zinaweza kufuatiwa kurudi nyuma hadi kwa mijadala juu ya *Montanism* karibu mwisho wa karne ya 2. Ireneo wa *Lyons* anaona umitume ukidhihirika katika makubaliano ya makanisa yaliyotawanyika ulimwenguni. Ilionyeshwa na maaskofu husika, ambao aliwachukulia kama warithi wa mitume. Kipriano wa *Carthage* anabadilisha msisitizo kutoka kwa tamaduni iliyolindwa na maaskofu kwenda kwa tabia ya ushirika wa uaskofu, ambayo ofisi yake ya kitume hudhihirishwa, wakati inapofaa, katika mabaraza. Kulingana na Kipriano, kanisa "limeunganishwa na kushikiliwa pamoja na gundi ya mshikamano wa pamoja wa maaskofu". Kufikia karne ya tatu Masharika na Magharibi vile vile, baraza la kanisa (liwe la nyumbani au la mkoa) linatambuliwa ulimwenguni kama njia kuu ambayo umoja wa kanisa katika mila ya kimitume inapaswa kutekelezwa na kulindwa wakati hali inahitajika. Na baada ya kushindwa kwa Mfalme Licinius kwa mkono wa Konstantino, kusanyiko la baraza la kiekumeniki liliwezekana (324).

**15.3** Sinodi za kanisa la kwanza, haswa baraza saba za kiekumeniki zilizotambuliwa na Waorthodoksi na Wakatoliki sawa, zilikuwa za kushangaza, hafla za dharura zilizoletwa na mazingira magumu, haswa hitaji la kujibu maunzo yasiyo kweli na kushughulikia shida kuu za umoja wa kanisa. Mabaraza kama hayo hayapaswi kuzingatiwa kimsingi katika hali ya kitaasisi, lakini kama maoni ya sauti au akili ya kanisa juu ya maswala fulani. Sinodi kwa ujumla zinaonekana kuwa na mamlaka katika masuala ya mafundisho, liturujia, na nidhamu kwa kadri zinavyoonyesha imani ya Kanisa.

**15.4** Sinodi ni tukio kuu ambalo umoja muhimu wa kanisa unaweza kudhihirika katika mazingira fulani na kwa mujibu wa hali maalum. Maaskofu kama warithi wa mitume walipewa jukumu la kuelekeza juu ya mambo ya mafundisho na utaratibu wa kanisa, wakielezea haswa imani ya jamii zao. Watu wote wa Mungu, na maaskofu haswa, wamepewa jukumu la utunzaji na usambazaji wa mahubiri ya kitume kulingana na 1 Yohana 1: 3: "yale ambayo tumeona na kusikia tunawatangazia pia".

**15.5** Maaskofu waliokusanyika katika sinodi hawana dhamana ya kupita zaidi ya mafundisho ya kimitume (depositum fidei / *paradosis*). Kazi yao kimsingi ni ya utambuzi, uthibitisho, na usemi: kutambua mila ya kimitume juu ya mada fulani, kuithibitisha tamaduni hiyo, na kuitangaza.

**15.6** Hati za mwanzo kabisa za kikanuni (kuanzia karne ya 4) yanaelezea kanuni ya usawazishaji katika njia nyingi, kwa mfano: kusisitiza kwamba askofu lazima atawazwe na angalau maaskofu watatu; hitaji la maaskofu katika kila eneo kutambua mamlaka ya "wa Kwanza" ili umoja udumishwe kati yake na maaskofu wengine; au maagizo ya kwamba mabaraza ya mara kwa mara yafanyike ndani ya kila dayosisi ya mji mkuu "kwa faida ya kanisa na kutatua mizozo".

**15.7** Kwa mwendo wa nyakati, makanisa pia yameanzisha aina zingine za mashauriano ya sinodi ambayo hushughulikia, kama tukio linavyotokea, maswala ya mafundisho na utaratibu wa kanisa na inapaswa kutofautishwa na sinodi (ziwe za mitaa, za mkoa au za ulimwengu). Hii ni pamoja na, kwa mfano, sinodi iliyopo au ya mji wa - sinodos endēmousa - inayojumuisha maaskofu waliopo huko Konstantinopoli kwa sababu anuwai na kwa hivyo wanauwezo wa kukusanyika kwa taarifa fupi wakati jibu la jopo linahitajika. Makanisa kadhaa ya Orthodox yaliyo huru katika nyakati za kisasa yamepitisha mfumo ambao makanisa husika husimamiwa na kuongozwa na sinodi ya kudumu ya maaskofu na wateule wengine.

**15.8** Maneno na michakato ya sinodi ni ya uelewaji wa kibinafsi wa Makanisa Katoliki na Orthodoksi. Katika historia, licha ya tofauti zilizoonekana kwa muda na kati ya mila zetu mbili, Kanisa halijawahi kuishi bila ufahamu wa umoja.

**16. Ukuu wa Ki-ekklesia na Usawazishaji kwa huduma ya ushirika**

Kauli ya pamoja: *Ueklessia unaoegemea Ukaristia lazima ufahamu usawa wa asili na uelewano kati ya sharia za ukuu na usawa. Kwa mfano, katika mila ya kanuni, hii inaonyeshwa katika Kanuni ya Kimitume ya 34. Ukuu na Usawazishaji sio njia za hiari za usimamizi wa kanisa, lakini ni mbinu za asili ya kanisa kwa sababu zote mbili zinakusudiwa kuimarisha na kuimarisha ushirika katika ngazi zote. Wote kitheolojia na kikanuni, kwa hivyo haiwezekani kushughulikia suala la ukuu bila kuzingatia usawazishaji, au kupuuza ukuu wakati wa kushughulika na usawazishaji.*

**16.1** Yesu Kristo ndiye kichwa cha kanisa (taz. Efe 1:22), na kwa hivyo "katika kila kitu anaweza kuwa maarufu" (Kol 1:18). Umoja huu ulio hai, baina ya kichwa na mwili huonyeshwa katika maisha ya kanisa katika mwingiliano kati ya Uaskofu na sinodi. Kila aina ya ukuu wa kanisa, kwa asili, sio nguvu juu ya kanisa, lakini ndani yake kama huduma iliyo chini ya Yesu Kristo aliye kichwa chake (taz. § 13.2 na 5).

**16.2** Uzoefu wote wa Ukaristia na mila ya kikanuni zinaonyesha kuwa Ukuu na usawazishaji hutegemeana. Katika Ukaristia, ashirio la kimsingi la maisha ya kanisa kwa ujumla, jamii na wasimamizi wanaosimamia (askofu au kasisi aliyepewa mamlaka naye) wako katika uhusiano wa kutegemeana: jamii haiwezi kusherehekea Ukaristia bila *proestos (Kasisi)*, ambaye, kwa upande wake, hapaswi kusherehekea bila jamii. Katika tamaduni ya kanuni, maelezo ya uhusiano kati ya "wa Kwanza" na maaskofu wengine yamewekwa rasmi katika ngazi ya mkoa kwenye kanuni ya Kimitume ya 34 (taz. §§ 7.4 na 14.7): maaskofu wa kila mkoa hawawezi kufanya jambo lolote muhimu bila idhini ya kichwa chao, ambaye, kutoka upande wake, hawezi kufanya chochote bila idhini ya wote. Ukuu na usawazishaji hazipaswi kupiganishwa kamwe. Ila, lazima zichukuliwe kama zisizoweza kutenganishwa na kama zinazosaidiana katika utumishi wa umoja wa kanisa la Mungu.

**16.3** Wakati wa milenia ya kwanza, taasisi zote za ukuu wa kidini katika kila ngazi ya kanisa zilikita mizizi kwenye miundo ya sinodi. Katika miktadha kadhaa ya kihistoria, ukuu ulibaki kuwa ukweli uliokubalika ulimwengu wote unaodhihirisha uhusiano kati ya mkutano na yule anayesimamia, na misingi na njia tofauti za utendaji katika viwango tofauti ambavyo ushirika katika kanisa unatendeka. Kwa hivyo, mtu hawezi kuelewa ukuu pasipo usawazishaji, au kushughulika na usawazishaji wakati anapuuza ukuu.

**16.4** Kuna ulinganifu lakini hakuna kitambulisho katika uhusiano baina ya ukuu na usawazishaji katika viwango tofauti vya kanisa: mitaani, mkoani, na ulimwengu wote. Kwa sababu asili ya ukuu na usawazishaji hutofautiana katika kila ngazi, mienendo kati ya ukuu na usawazishaji pia hutofautiana ipasavyo. Kwa mfano, ukuu na usawazishaji katika kiwango cha mkoa sio za aina sawa na zile zilizo kwenye kiwango cha dayosisi. Katika usawazishaji wa dayosisi, askofu wa dayosisi ana karama maalum, inayomwezesha kuwa mdhamini wa ushirika kati ya kanisa lake na makanisa mengine ya mahali hapo. Vivyo hivyo, uhusiano wa ukuu na usawazishaji katika kiwango cha ulimwengu hauangazi moja kwa moja ule ulio katika kiwango

cha mitaa au mkoa na hivyo inahitaji uchunguzi zaidi wa kitheolojia. Ukosefu wa msimamo wa pamoja wa Orthodoksi juu ya ukuu katika kiwango cha ulimwengu wote unachanganya mazungumzo ya Orthodoksi na Katoliki katika suala hili, na vile vile ukosefu wa muundo wazi wa sinodi katika Kanisa Katoliki pia wachanganya mazungumzo.

**16.5** Kipengele muhimu cha uhusiano kati ya ukuu na usawazishaji ni swali la jinsi ya kulinda uhusiano wa karibu kati ya ushirika wa makanisa na ujamaa wa maaskofu. Maaskofu ni mashahidi wa imani ya makanisa yao, lakini pia wana jukumu la kanisa kwa ujumla. Haki hii, inayoonyeshwa katika sakramenti ya kutawazwa kwa maaskofu, huwafanya maaskofu kuwa watumishi wa ushirika wote - sio tu katika kanisa lao, bali pia kati ya makanisa yaliyo mitaani kwao, kama inavyoashiria kwa kuwekelewa mikono na maaskofu waadhimishao ibaada ya kutawazwa.

**16.6** Usawazishaji, kama kielelezo kinachoonekana cha ukatoliki wa kanisa, haihusiani tu na uongozi wa kanisa ila pia kwa watu wote wa Mungu. Kwa njia hii, umoja wa walio wa "Kwanza" na waaminifu wao unaweza kuonyeshwa katika viwango tofauti katika maisha ya kanisa, kwa sababu jukumu la kanisa linakaa na washiriki wake wote. Watu walei wamealikwa kama washauri kwenye sinodi za maaskofu wa Kanisa Katoliki juu ya maswala ya kifamilia (2015 na 2016) na pia kwa Baraza la Orthodox huko Krete (2016) inathibitisha hii. Walei wanaweza kutajirisha mazungumzo ya sinodi na hali yao ya kiroho na utaalam.

**16.7** Historia ya Kanisa inaonyesha mieelekeo miwili ya ki-eklesia: kwa upande mmoja, hasa lakini sio pekee, mwelekeo wa sinodi wa Mashariki, na upande mwingine, hasa lakini sio pekee, mwelekeo wa Ukuu (wa ki-ekklesia) wa Magharibi; ingawa hizi zinaweza kuishi pamoja kwa mvutano wa ubunifu. Kurejeshwa kwa ushirika kamili kati ya Kanisa Katoliki na la Orthodoksi kutahitaji, pande zote mbili, kuimarishwa kwa miundo ya sinodi na kuelewa upya Ukuu (wa ki-ekklesia) ya ulimwengu mzima – yote yakihudumia umoja kati ya makanisa.

## *V. Hitimisho*
### *Muhtasari*

**17.1** Katika kazi yao hadi sasa, wanachama wa Orthodoksi na Katoliki wa Kikundi cha utenda Kazi cha Mtakatifu Irineo wamekuwa wakishirikiana kwa roho ya urafiki na kubadilishana mawazo. Wanajua kuwa, katika kipindi cha miaka 14, wamefanya maendeleo makubwa katika juhudi zao za kujenga imani ya pamoja, kuelewana kwa undani zaidi, na kuona zaidi ya vizuizi ambavyo vimekuwa vikiwakwamisha kurejesha ushirika kamili kati ya makanisa yao.

**17.2** Hii pia imewezekana kwa sababu wanachama wamejitahidi kupitisha mbinu ambayo inahusisha tafsiri ya *data* za kihistoria kwa njia inayoangalia muktadha wao kikamilifu; tafsiri zisizo sahihi zinazotafsiri migogoro ya baadaye kama vile zilikuwa katika nyakati za kale zinakwepwa; na thamani ya kudumu ya maelezo kama yalivyoeleweka awali inatafutwa.

**17.3** Wanachama wamepitisha mbinu hii katika utafiti wao wa maswali mbalimbali ambayo yamepangwa katika kauli 16 za pamoja, zikianza na umuhimu wa Tafsiri ya maandiko kwa mazungumzo ya umoja yenyewe. Katika kufanya hivyo, wamefuata kanuni kuu zifuatazo: 1) Lugha ni muhimu, na maneno huchukua maana tofauti katika vipindi mbalimbali vya wakati;

2) Misingi ya imani ambayo Orthodoksi na Katoliki wanayo inapaswa kusomwa katika muktadha wao, kwa juhudi ya kugundua kile kinachosemwa na kile kilichokusudiwa kusemwa; 3) Mielekeo tofauti ya sheria za kanuni pia inapaswa kuzingatiwa, pamoja na kiwango cha utekelezaji wa baadhi ya kanuni zilizotungwa karne nyingi zilizopita katika dunia ya leo; 4) Aidha, jukumu la mambo yasiyo ya ki-theolojia lazima lizingatiwe katika utafiti wa migawanyiko yetu; na 5) Kwa hakika, ufahamu wa historia ni muhimu kwa kuelewa vyema mila za ki-theolojia za Mashariki na Magharibi. Historia isingeweza kuonyeshwa kwa kubuni au kupuuziliwa mbali, na mgawanyo sahihi unapaswa kufanywa kati ya mambo yaliyoelezwa na makanisa na hali halisi ya kibinadamu ambamo hayo mambo yanaishi.

**17.4** Kikundi cha Irineo kimekalia mbinu hii hii katika utafiti wake wa historia ya mwelekeo unaoendelea wa utofauti kati ya Mashariki na Magharibi katika milenia ya kwanza, na kwa mwelekeo tofauti kila upande uliochukua baada ya kupoteza ushirika kamili na mwingine. Kipindi cha kabla ya Mkutano wa Nikea (325) ni muhimu hasa na kinaweza kutoa vipengele vya mfano muhimu kwa kushughulikia maswali magumu katika makanisa leo. Misingi ya Ukuu (wa ki-ekklesia) na usawazishaji zilikuwa zote zinatumika katika karne za mwanzo, lakini hakuna mfano mmoja wa uhusiano kati ya hizi uliokubaliwa kimataifa. Kipindi cha kutoelewana kati ya Wakatoliki na Waorthodoksi kuanzia karne ya 9 hadi ya 15 kilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kutoelewana kwa kitamaduni, na maendeleo waliyoyapata yaliguswa na hali halisi za kisiasa na kijamii walizokutana nazo. Vitambulisho vya kidini vya Wakatoliki na Waorthodoksi vilikua ngumu katika kipindi cha kujiweka wazi kidini (karne za 16 hadi 18), wakati ambapo Wakatoliki na Waprotestanti walizidisha juhudi zao za uinjilisti. Mchakato huu ulifikia kilele katika karne ya 19 wakati Wakatoliki na Waorthodoksi walilazimika kukabiliana na changamoto tofauti kabisa. Kikundi cha Irineo kilitolea muda mwingi muktadha wa kihistoria na wa ki-theolojia kuhusu mafundisho yanayojulikana kuhusu kutohitilafiwa kwa Papa na mamlaka ya ulimwengu kutoka Mkutano wa Vatican I. Katika kipindi hicho hicho, makanisa mapya na huru yalizaliwa Mashariki kama jibu kwa machafuko ya kisiasa huko Ulaya ya Kusini-Mashariki. Ilikuwa ni kwa ufanisi wa eklesiaolojia wa karne ya 20 ambapo Makanisa ya Katoliki na ya Orthodoksi yaliona mchakato wa upatanisho ambao ulikuwa ukizidi kupata nguvu kutokana na mafundisho ya Mkutano wa Pili wa Vatican na maendeleo yanayoendana katika theolojia ya Orthodoksi. Wanachama wa Kikundi cha Irineo wanaamini kuwa kipindi cha sasa cha uhusiano wa pamoja ni cha matumaini zaidi kwa karne nyingi.

**17.5** Kwa kuzingatia haya, Kikundi cha Irineo kimefikiria maswali fulani ya kimfumo yanayohusu uhusiano kati ya Kanisa Katoliki na Kanisa la Orthodoksi. Kikundi kinakubali kuwa Ekaristi ni kiashiria cha msingi cha Kanisa, kikiwa na umoja wake na majukumu tofauti yanayozingatiwa na wanachama wake. Uhusiano kati ya anayeongoza (presider) na washirika wa Ekaristi pia hutoa msingi wa ki-theolojia wa kuelewa upya Ukuu (wa ki-ekklesia) na usawazishaji katika Kanisa, na mamlaka ambayo, iwe inatekelezwa kwa njia ya Ukuu (wa ki-ekklesia) au usawazishaji, inapaswa kuwa daima huduma kwa jamii. Biblia na Tamaduni zote zinathibitisha haja ya huduma ya Ukuu (wa ki-ekklesia) kuhudumia umoja wa Kanisa katika viwango mbalimbali. Lakini pia zinathibitisha haja ya usawazishaji katika ngazi zote za maisha ya kanisa. Ulinganifu wa misingi hii miwili utakuwa muhimu kwa kuelewa kwa kina theolojia ya Kanisa ambayo itasaidia upatanisho kati ya Orthodoksi na Katoliki.

**17.6** Wanachama wa Kikundi cha Irineo wanajua kuwa hawajafikia hatua ya kutoa mapendekezo ya moja kwa moja ambayo yatakuwa msingi wa kurejesha ushirika kamili. Hata hivyo, wanaamini kuwa mazungumzo ya Orthodoksi-Katoliki yako kwenye njia ya umoja, na

kwamba hata sasa inawezekana kuona muhtasari wa Kanisa la Katoliki na la Orthodoksi lililo na umoja kamili. Wanayo imani kuwa maono yoyote ya siku za usoni yanapaswa kuonyesha mfano wa umoja wenye maelezo ya kina, ukizingatia kuwa utekelezaji wa mfano huu utakuwa hatua kwa hatua. Harakati kuelekea upatanisho kati ya Wakatoliki na Waorthodoksi haitalazimisha suluhisho la papo hapo kwa masuala yote yaliyo mbele, bali mfumo wa pamoja wa mbinu kuelekea lengo hili.

**17.7** Katika tafakari zao, wamezingatia kazi ya Mkutano wa Theolojia wa Orthodoksi-Katoliki wa Amerika Kaskazini, hasa kauli yao ya makubaliano ya mwaka 2010, "Hatua kuelekea Kanisa lililorudi pamoja: Muhtasari wa Maono ya Orthodoksi-Katoliki kwa Siku za Usoni". Pamoja na Mkutano wa Amerika Kaskazini, wanachama hawa hawaamini kuwa tofauti zozote ambazo zimewagawanya makanisa yao kwa karne nyingi ni lazima ziwe za kushindwa kuzitatua. Tofauti zote hizo tofauti zitahitaji utafiti wa kina zaidi kwa mbinu ya tafsiri ya maandiko ili kubaini kama kweli zinazuia kurejeshwa kwa ushirika kamili, au kama ni mifano ya utofauti halali. Zaidi ya yote, makanisa yatahitaji kujitahidi kufikia usawa mkubwa kati ya usawazishaji na Ukuu (wa ki-ekklesia) katika ngazi zote za maisha ya kanisa, kwa kuimarisha miundo ya usawazishaji katika Kanisa Katoliki na kukubaliana katika Kanisa la Orthodoksi dhidi ya Ukuu (wa ki-ekklesia) Fulani, ndani ya ushirika wa makanisa katika kiwango cha ulimwengu.

**17.8** Kikundi cha Irineo kinajua kuwa kufafanua jukumu halisi la askofu wa Roma katika ushirika utakaorejeshwa kati ya makanisa yetu kutakuwa ni kipengele kigumu zaidi cha mchakato huu. Wanachama wa kikundi chetu wana imani kuwa askofu wa Roma anaweza na anapaswa kucheza jukumu kubwa katika kuonyesha umoja wa Wakristo duniani leo. Ili kufanya hivyo, uhusiano kati ya Kanisa la Roma na makanisa ya Mashariki unahitaji kufasiliwa kwa namna ambayo inaheshimu kikamilifu urithi wa kanisa lisilogawanyika na pia kukubalika na Wakatoliki na Waorthodoksi kwa pamoja. Hii itahitaji upya wa tafsiri ya mafundisho ya Mkutano wa Kwanza wa Vatican. Katika muktadha huu, tofauti inapaswa kufanywa kati ya utendaji wa Ukuu (wa ki-ekklesia) kama ulivyokua ndani ya muktadha wa kihistoria maalum, na asili ya Ukuu (wa ki-ekklesia) yenyewe. Njia inapaswa kupatikana ya kushinda baadhi ya mitazamo ya zamani na kuunganisha vipengele muhimu ambavyo vimehifadhiwa katika mapokeo yote mawili katika ufahamu wa pamoja wa Ukuu (wa ki-ekklesia).

**17.9** Itakuwa pia ya manufaa kubwa kuchunguza tena uhusiano kati ya Kanisa la Roma na Makanisa ya Mashariki katika milenia ya kwanza, hasa katika kipindi cha kabla ya Mkutano wa Kwanza wa Nikea mwaka 325, na hasa uhusiano ulioainishwa katika masharti ya Mkutano wa Sardica mwaka 343. Huu ulianzisha aina ya korti ya Papa ambapo mizozo kati ya makanisa ingeweza kuhamishiwa Roma, ambayo kisha ingeandaa usuluhishi na jopo lingine ambalo askofu wa Roma angeweza kutuma wajumbe. Mpango kama huu ungeheshimu kikamilifu uhuru wa Makanisa ya Orthodoksi wakati huo huo ukihakikisha huduma ya umoja ya kimataifa kwa askofu wa Roma.

**17.10** Wakati kazi yetu hadi sasa imejikita zaidi katika uchunguzi wa pamoja wa muktadha wa kihistoria ambao umeleta makanisa yetu hadi hapa tulipo leo, tunajua kuwa kazi hii ya kihistoria, ingawa ni muhimu na lazima, haijatoa majibu yote kwa ajili ya siku za usoni. Uchambuzi wetu hadi sasa unaonyesha wazi kiwango ambacho maendeleo ya kimuundo katika makanisa yetu yameathiriwa na mchanganyiko wa mambo mbalimbali – ki-theolojia, kihistoria,

na kijamii. Changamoto zinazokabili makanisa leo si sawa na zile zilizokuwepo katika milenia ya kwanza – wala hata katika karne ya 19. Kwa hivyo tunatambua kwamba kurejea tu kwa historia si suluhisho, kwa Waoorthodoksi wala kwa Wakatoliki.

**17.11** Pamoja, tunakiri kwamba tuna mengi ya kujifunza kutoka kwa kila mmoja kuhusu masuala ya Ukuu (wa ki-ekklesia) na usawazishaji. Kanisa la Katoliki limeweza kudumisha Ukuu (wa ki-ekklesia) wenye nguvu, ingawa baadhi ya matokeo yake yanaonekana kuwa na matatizo kwa Waorthodoksi. Waorthodoksi, kwa upande mwingine, wameweza kwa kiasi kikubwa kuhifadhi miundo ya usawazishaji imara katika viwango vya kitaifa, kikanda, na kwa hivi karibuni, kimataifa, ingawa wakati mwingine hii husababisha hali ngumu zinazowatia wasiwasi Wakatoliki. Hivyo kila upande unadhihirika kuwa na nguvu na udhaifu, ambayo tunaweza kukubali wote.

**17.12** Tunapotafuta umoja wa Kanisa, inaendelea kuwa wazi kwetu kuwa suluhisho la pamoja, linalokubalika kwa makanisa yote mawili, linahitajika, suluhisho litakalojengwa juu ya nguvu za pande zote mbili. Si kuwa tu kwamba suluhisho hili linapaswa kukubalika kwa pande zote, bali linapaswa kujibu mahitaji ya karne ya 21, na enzi ya mawasiliano ya papo hapo ambayo inahitaji uwazi na uwajibikaji. Hii inamaanisha, miongoni mwa mambo mengine, kwamba mifano ya kifalme au ya kifalme ya kale huenda isiwe na nafasi tena. Zaidi ya yote, hii inahitaji nia njema, hamu ya kushirikiana na kufanya kazi pamoja katika kujenga madaraja – si tu miongoni mwa wanatheolojia wa kitaaluma, bali pia miongoni mwa mapadri, wanaohudumia maisha ya kila siku ya kanisa, na miongoni mwa waumini wote, ambao wanapaswa kupata sauti yao kama washirika wa Mwili wa Kristo. Hii ni kweli hasa kwa maaskofu wetu, wanaosimamia maisha ya makanisa yetu, na ambao hivyo ndivyo watakuwa na jukumu la kutekeleza na kufikia umoja unaotamaniwa. Kikundi cha Irineo kwa hiyo kinasaidia utekelezaji wa hatua kadhaa za kati ambazo zinaweza kufanyika hata kabla ya kurejeshwa kwa ushirika kamili, ikiwa ni pamoja na maaskofu kutoka makanisa yote mawili kukutana mara kwa mara, kama ilivyopendekezwa katika kauli ya makubaliano ya Mkutano wa Theolojia wa Orthodoksi-Katoliki wa Amerika Kaskazini wa mwaka wa 2010.

**17.13** Kama wanachama wa Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo, tunajitolea kuendelea na uchunguzi wa maswali haya kwa matumaini ya kutoa mchango mkubwa katika mchakato wa upatanisho kati ya Makanisa ya Katoliki na ya Orthodoksi. Hii sasa inasisitizwa na juhudi mbalimbali, hasa kupitia mazungumzo rasmi. Tunatambua kikamilifu kuwa mchakato huu utafanikiwa pekee ikiwa ubadilishanaji wa mawazo hautakuwa na mipaka kwa wanatheolojia pekee, bali pia utahusisha waumini kwenye pande zote mbili.

**Kiambatanishi:**

Wanachama wa sasa (2018) wa Jopo la Orthodoksi-Katoliki la Mtakatifu Irineo ni:

| **Wa Katoliki** | **Wa Orthodoksi** |
|---|---|
| Bishop Dr. **Gerhard Feige** of Magdeburg (from Germany, member and Catholic Co-president since 2004) | Metropolitan Dr. **Serafim (Joantă)** of Germany, Central and Northern Europe (from Romania, member and Orthodox Co-president since 2018) |
| Dr. Johannes **Oeldemann** (from Germany, member and Catholic Co-secretary since 2004) Johann-Adam-Moehler-Institute for Ecumenics, Paderborn | Rev. Prof. Dr. Nikolaos **Loudovikos** (from Greece, member and Orthodox Co-secretary since 2004) University Ecclesiastical Academy, Thessaloniki |
| Prof. Dr. Dr. Pablo **Argárate** (from Argentina, member since 2016) Faculty of Catholic Theology, University of Graz | Rev. Prof. Dr. Daniel **Benga** (from Romania, member since 2008) Institute of Orthodox Theology, University of Munich |
| Prof. Dr. Thomas **Bremer** (from Germany, member since 2004) Faculty of Catholic Theology, University of Münster | Rev. Prof. Dr. Cyril **Hovorun** (from Ukraine, member since 2008) Huffington Ecumenical Institute, Loyola Marymount University, Los Angeles, CA |
| Rev. Prof. Dr. Hyacinthe **Destivelle** OP (from France, member since 2006) Pontifical University of St Thomas Aquinas, Rome | Prof. Dr. Assaad Elias **Kattan** (from Lebanon, member since 2006) Chair for Orthodox Theology, Center for Religious Studies, University of Münster |
| Rev. Prof. Dr. Edward G. **Farrugia** SJ (from Malta, member since 2005) Pontifical Oriental Institute, Rome | Rev. Dr. Vladimir **Khulap** (from Russia, member since 2012) Orthodox Theological Academy, Saint Petersburg |
| Prof. Dr. Basilus J. **Groen** (from the Netherlands, member since 2004) Faculty of Catholic Theology, University of Graz | Prof. Dr. Paul **Meyendorff** (from the USA, member since 2004) Saint Vladimir's Orthodox Theological Seminary, Crestwood, NY |
| Rev. Dr. Michel **Jalakh** OAM (from Lebanon, member since 2017) Antonine University, Beirut | Rev. Prof. Dr. Grigorios **Papathomas** (from Greece, member since 2004) Faculty of Orthodox Theology, University of Athens |
| Rev. Prof. Dr. Hervé **Legrand** OP (from France, member since 2004) Institut Catholique, Paris | Rev. Prof. Dr. Vladan **Perišić** (from Serbia, member since 2004) Faculty of Orthodox Theology, University of Belgrade |
| Fr. Adalberto **Mainardi** (from Italy, member since 2012) Bose Monastery, Magnano | Dr. Evgeny **Pilipenko** (from Russia, member since 2014) Ss. Cyril and Method Institute of Post-Graduate and Doctoral Studies, Moscow |
| Rev. Prof. Dr. Rudolf **Prokschi** | Prof. Dr. Marcus **Plested** |

| | |
|---|---|
| (from Austria, member since 2004)<br>Faculty of Catholic Theology, University of Vienna | (from Great Britain, member since 2014)<br>Department of Theology, Marquette University, Milwaukee, WI |
| Rev. Dr. Ronald G. **Roberson** CSP<br>(from the USA, member since 2004)<br>Secretariat for Ecumenical Affairs of the US Conference of Catholic Bishops, Washington, DC | Rev. Prof. Dr. Mihail-Simion **Săsăujan**<br>(from Romania, member since 2012)<br>Faculty of Orthodox Theology, University of Bucharest |
| Prof. Dr. Wolfgang **Thönissen**<br>(from Germany, member since 2004)<br>Johann-Adam-Moehler-Institute for Ecumenics, Paderborn | Prof. Dr. Mariyan **Stoyadinov**<br>(from Bulgaria, member since 2004)<br>Faculty of Orthodox Theology, University of Veliko Tarnovo |

Na waliokuwa wanachama wa hapo awali wa kikundi cha Mtakatifu Irineo ni:

| **Ma Katoliki** | **Wa Orthodoksi** |
|---|---|
| Rev. Prof. Dr. Brian E. **Daley** SJ, Notre Dame, IN<br>(from the USA, member 2014 – 2016) | Bishop Dr. **Ignatije (Midić)** of Braničevo<br>(from Serbia, member and Orthodox Co-president 2004-2008) |
| Rev. Prof. Dr. Zygfryd **Glaeser**, Opole<br>(from Poland, member 2004 – 2014) | Metropolitan Dr. **Youhanna (Yazigi)** of Western and Central Europe, Paris<br>(from Syria, member and Orthodox Co-president 2009-2012,<br>now Patriarch of Antioch and all the East) |
| Pieter **Kohnen**, ’s-Hertogenbosch<br>(from the Netherlands, member 2004 – 2013,<br>† 2018) | Archbishop **Dr. Job (Getcha)** of Telmessos<br>(from Canada, member 2004-2017,<br>Orthodox Co-president 2013-2017,<br>now Co-president of the International Catholic-Orthodox Commission for Theological Dialogue) |
| Rev. Antoine **Lambrechts** OSB, Chevetogne<br>(from Belgium, member 2004 – 2007) | Prof. Dr. Marios **Begzos**, Athens<br>(from Greece, member 2004 – 2011) |
| Rev. Prof. Dr. Lorenzo **Lorusso** OP, Bari<br>(from Italy, member 2008 – 2011) | Rev. Prof. Dr. Viorel **Ioniţă**, Geneva<br>(from Romania, member 2004 – 2007) |
| | Rev. Dr. Andrzej **Kuzma**, Warsaw<br>(from Poland, member 2006 – 2011) |
| | Rev. Viktor **Savik**, Smolensk<br>(from Russia, member 2004 – 2007) |
| | Rev. Dr. Vladimir **Shmaliy**, Moscow<br>(from Russia, member 2009 – 2011) |
| | Rev. Prof. Dr. Jan **Zozul’ak**, Prešov<br>(from Slovakia, member 2005 – 2007) |